


# UKWELI KUHUSU
# UKAFIRI WA USHIA

## حقيقة كفر الشيعة

1447 = 2026

Mwandishi: *Abuu Ayman Othman Iddy, Allah Amuhifadhi*

بسم الله الرحمن الرحيم

# حَقِيقَةُ كُفْرِ الشِّيْعَةِ

## UKWELI KUHUSU

# UKAFIRI WA USHIA

**Mwandishi: Abuu Ayman Othman Iddy**

CHAPA YA KWANZA

NB: NI RUHUSA KUTOA NAKALA NA KUKISAMBAZA.

USIBADILI WALA KUONGEZA CHOCHOTE BILA IDHINI

YA MWANDISHI.

# YALIYOMO


Utangulizi ........ 7
Sababu za kuandika kitabu hiki ........ 7
Misingi ya kitabu hiki ........ 8
**SEHEMU YA KWANZA** ........ 9
Maana ya Ukafiri ........ 9
Je, inafaa kumuita Muislamu Kafiri? ........ 9
Ni wakati gani ukafiri unathibiti kwa mtu? ........ 10
Ni zipi Sharti za kumkufurisha mtu maalum? ........ 10
Vizuizi vya kumkufurisha mtu maalum ........ 10
Je, inafaa kulikufurisha kundi lolote katika yale yanayojinasibisha na Uislamu? ........ 11
**SEHEMU YA PILI** ........ 13
Vitenguzi vya Uislamu ........ 13
Kitenguzi cha Kwanza ........ 15
Maana ya ibada ........ 16
Maana ya Ushirikina ........ 20
Tofauti kati ya Mshirikina na Kafiri ........ 21
Kitenguzi cha pili ........ 24
Kitenguzi cha tatu ........ 31
Kitenguzi cha Nne ........ 35
Hukumu ya aliyedharurika kuhukumiana kwa kanuni ........ 38
Kitenguzi cha tano ........ 39

Kitenguzi cha Sita ........ 42
Hukumu ya kukaa na watu wanaoifanyia mzaha dini ........ 45
Kitenguzi cha Saba ........ 45
Kitenguzi cha Nane ........ 48
Je, kafiri apendwe endapo atawapenda Waislamu? ........ 52
Kitenguzi cha Tisa ........ 52
Kitenguzi cha Kumi ........ 54
Vizuizi vya kumkufurisha mtu Maalum ........ 58
Je anapewa udhuru aliyefanya jambo la kufuru kwa sababu ya ajira? ... 61
Je ujinga ni udhuru kwa kila mtu? ........ 62
Ni mambo yapi ambayo husimama hoja kwa mtu? ........ 63
Kizuizi cha kukosea ........ 64
**SEHEMU YA TATU** ........ 65
Ushia ni nini? ........ 65
Je, Ushia ulianza lini? ........ 68
Je, neno Shia lililokuja ndani ya Qur'ani linamaanisha Ushia? ........ 72
Je, Ushia ni dhehebu au ni Dini? ........ 74
Je, Ushia ulipandikizwa na nani ndani ya Uislamu? ........ 76
Ni kauli zipi hasa zilikuwa ndio msingi wa mwanzo wa Ushia? ........ 77
Ni wapi Mashia wanapatikana hasa Afrika Mashariki? ........ 78
Tahadhari dhidi ya kuwasikiliza Mashia ........ 79
Ni akina nani Raafidhwa? ........ 80
Shia Ithna-asheria ni akina nani? ........ 82
Je, ni kweli Maimamu hawa walikuwa Mashia? ........ 83
Kwa nini Ushia na Iran?, na kwa nini Ali tu na si Maswahaba wengine? 85

Je, itikadi za Ushia zilitokana na Uislamu? ..... 88
Ni akina nani Shia Ismaili? ..... 89
Kwa nini wanaitwa Ismaili (Ismaailiyya)? ..... 90
**SEHEMU YA NNE** ..... 91
Kadiyani (Ahmadiyya) ni akina nani? ..... 91
Ni nani Ghulam Ahmad Al-Kadiani? ..... 92
Kudai kwake Utume ..... 93
Madai yake kuwa yuko katika nafasi ya mwana wa Mungu, na katika nafasi ya Arshi ..... 94
Itifaki ya Umma wa Muhammadi kuwa Muhammadi ndiye mwisho wa Mitume, nakuwa hakuna Nabii baada yake, nakuwa mwenye kulipinga hilo ni kafiri ..... 95
Kudai kwake kuwa Malaika ni viungo vya Mwenyezi Mungu ..... 96
**SEHEMU YA TANO** ..... 96
Wabahai ni akina nani? ..... 96
Ulitengenezwa vipi ubahai? ..... 97
Ni zipi itikadi za Mashia (Raafidhwa)? ..... 99
Itikadi yao katika Qur’ani ..... 99
Madai yao kuwa Qur’ani si hoja ila kwa kunyooshwa ..... 101
Madai yao kuwa kauli ya imamu inaweza kufuta Qur’ani ..... 101
Madai yao kuwa Qur’ani yote ilishuka kwa ajili yao na maadui zao ..... 102
Itikadi yao ya kuteremshwa vitabu vya kiuungu kwa Maimamu wao .. 103
Itikadi yao katika hadithi za Mtume ..... 103
**Itikadi yao kuwa kauli ya Imamu ni sawa na kauli ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake** ..... 103
Kauli yao kuwa Mtume alificha baadhi ya yale aliyoteremshiwa ..... 104

Kuzikataa kwao riwaya za Maswahaba ........ 105
Itikadi yao kuhusu Imani na nguzo zake ........ 105
Shahada ya tatu: ........ 106
Maana ya Tauhidi kwao ........ 107
Kauli zao kuhusu kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada ........ 108
Kauli yao kuwa kuhiji katika makumbusho ni bora kuliko kuhiji katika nyumba ya Mwenyezi Mungu ........ 108
Madai yao kuwa Karbalaa ni bora kuliko Kaa'ba ........ 109
Kauli zao kuhusu kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika Uumbaji na uendeshaji ........ 109
Kauli yao kuwa: Dunia na Akhera ni miliki ya imamu anaziendesha atakavyo ........ 110
Sehemu ya Uungu iliyotua kwa Maimamu ........ 110
Kauli zao kuhusu Tauhidi ya Majina na sifa ........ 111
Kuwaamini Malaika ........ 112
Kuamini vitabu ........ 113
Kuwaamini Mitume ........ 113
Kauli yao kuwa maimamu wana miujiza kama miujiza ya Manabii ........ 114
Kuamini siku ya Mwisho ........ 115
Miongoni mwa itikadi zao ........ 116
Kurejea kwa wafu ........ 117
Kujitokeza kwa maimamu ........ 119
Itikadi ya Taqiyya (Kuficha unachoamini) ........ 119
Je kuficha imani (Taqiyya) kulikotajwa ndani ya Qur'ani ndiko huko wanakofanya Mashia? ........ 120
Itikadi ya kaudongo ........ 120

Siri ya kaudongo ........ 121
Mwanzo wa itikadi ya kaudongo........ 121
Ubatili wa itikadi ya kiudongo ........ 122
Imamu Mahdi na kutoweka kwake ........ 124
Mizizi ya itikadi ya Imamu Mahdi........ 125
Ndoa ya (mkataba) Mut'aa ........ 125
Usahihi kuhusu Mut'aa ........ 128
**SEHEMU YA SITA**........ 130
Aashuraa ni nini?........ 130
Mambo yanayofanyika siku ya Aashuraa........ 130
Kufuru inayofanyika katika siku ya Aashuraa........ 131
Majibu ya Kufuru zao ........ 132
Lipi jambo sahihi la kufanya siku ya Aashuraa ........ 137
Je, wanayofanya Mashia siku ya Aashuraa ndio waliyoamrishwa? ...... 138
**SEHEMU YA SABA** ........ 139
Maneno machafu ya Al-Khomeini kwa Maswahaba........ 139
**SEHEMU YA NANE** ........ 141
Machafu ya Mashia wasiyotaka watu wayajue ........ 141
Je itikadi kama hizi za Ushia ni rehema au ni laana? ........ 144
Kujionyesha kwao kwa kujinasibisha na Sunna ........ 145
**SEHEMU YA TISA**........ 146
Ni zipi itikadi za Mashia Ismailia kwa Ujumla?........ 146
**SEHEMU YA KUMI**........ 148
Je ni ipi hukumu ya Raafidhwa katika Uislamu? ........ 148
**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**........ 152

Je, inafaa kuswali nyuma ya Shia au katika misikiti yao? ...................... 152

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI** ........................................................ 154

Njia (Manhaji) ya Ahlus Sunna katika kuamiliana na makundi yanayokwenda kinyume ........................................................ 154

**SEHEMU YA KUMI NA TATU** ........................................................ 161

Njia fupi ya kukata mjadala katika Swala la haki ................................. 161

Sharti za kuapizana laana ........................................................ 163

**SEHEMU YA KUMI NA NNE** ........................................................ 163

Mwenye kufa katika itikadi za Ushia ................................................ 163

**Tamati** ........................................................ 167

بسم الله الرحمن الرحيم

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye Kurehemu**

## Utangulizi

kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa Walimwengu wote, na rehema na amani ziwe juu ya Mtume Muhammadi na Aali zake na Maswahaba wake, na wote watakaofuata njia yake mpaka siku ya mwisho.

## Sababu za kuandika kitabu hiki

Baada ya kuona ongezeko la kuenea kwa Ushia katika nchi zetu, hasa Tanzania, na udanganyifu wanaoufanya Mashia kupitia mitandao ya Kijamii wa kujionyesha kuwa wao ni wema, na ndio wenye uchungu zaidi na Uislamu, na ndio watetezi wa Waislamu duniani kote, na watu wengi kutoelewa hasa ni upi ukweli kuhusu ukafiri wa Ushia, nimeona niandike kitabu hiki, ikiwa lengo kuu ni kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuuweka wazi Umma kuhusu hili, huenda Mwenyezi Mungu akawaongoa watu wengi kupitia kile nitakachokinukuu ndani ya kitabu hiki, na wala lengo si kutafuta sifa wala umaarufu.

## Misingi ya kitabu hiki

Kitabu hiki kimejikita kueleza mambo kwa ushahidi kutoka katika Qur’ani na Sunna za Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na kauli za wema waliotangulia, pia nimenukuu maneno ya Masheikh, na waandishi wa kishia kutoka ndani ya vitabu vyao ili kuthibitisha ukweli wa yale niliyoyaandika ndani ya kitabu hiki, pamoja na kubainisha haki kwa kila mwenye kutafuta haki.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atuonyeshe haki na aturuzuku kuifuata na atuonyeshe batili na aturuzuku kuiacha.

# SEHEMU YA KWANZA

## Maana ya Ukafiri

Ukafiri ni: Kupinga jambo linalofahamika bila shaka katika dini, au kumpinga Mwenyezi Mungu au Mtume wake, au kuipuuza dini ya Uislamu, au kuwa na shaka nayo, au kua na unafiki wa kiitikadi. [1]

## Je, inafaa kumuita Muislamu Kafiri?

Watu wa Sunna hutofautisha kati ya kuhukumu kitendo na mtendaji maalum.

Kwa ujumla ni haramu kumuita Muislamu kuwa ni kafiri, bali mwenye kufanya hivyo anahofiwa yeye kuwa kafiri kwa kitendo hicho, kama ilivyokuja katika Hadithi:

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ :

" أَيُّمَا رَجُلٍ قَالَ لِأَخِيهِ : يَا كَافِرُ. فَقَدْ بَاءَ بِهَا أَحَدُهُمَا " (البخاري)

Kutoka kwa Abdillah bin Amri radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: **“Mtu yeyote atakayesema kumwambia ndugu yake: Ewe kafiri, basi atakuwa kapata kwa neno hilo moja katika mambo mawili”.**

---

[1 ] Rejea: Majmuu’ulfataawa ibin Taimiyya

[kaipokea Bukhari] Yaani: Ima iwe alilosema ni sawa, au lisiwe sawa na hapo ukafiri utamrejea yeye.

## Ni wakati gani ukafiri unathibiti kwa mtu?

Anasema Sheikhul Islam bin Taimiyya: **"Hakika kutoa hukumu ya ukafiri kwa ujumla, hakumaanishi ni kumkufurisha mtu maalum, ila kama zitapatikana sharti na vizuizi vikaondoka.** [2] Na anasema bin Taimiyya: **"Mimi ni katika watu ninaokataza vikali mtu kunasibishwa na ukafiri"** [3].

## Ni zipi Sharti za kumkufurisha mtu maalum?

1- Kufikiwa na hoja
2- Uwezo wa kuelewa
3- Utata umuondokee

## Vizuizi vya kumkufurisha mtu maalum

1- Ujinga.
2- Kulazimishwa.
3- Akiwa na tafsiri isiyo sahihi.
4- Kukosea.
5- Kusahau.

---

[2] Rejea: Qawaaidul Asmaa wal-ahkaam, bin Taimiyya: Uk.336
[3] Rejea: Majmuu'ul Fatawaa.

Na ufafanuzi wake utakuja baadaye, hivyo kwa yeyote yatakayetimia kwake masharti hayo, na vizuizi vikawa hakuna, basi huyu anakuwa kafiri kisheria.

## Je, inafaa kulikufurisha kundi lolote katika yale yanayojinasibisha na Uislamu?

Anasema Prof. Nassir bin Abdallah Alqifaari [4] katika kitabu chake **Maqaalaatul-Firaq**: "Ni lazima kutofautisha wakati wa kutoa hukumu juu ya makundi, kati ya kauli na msemaji, kwani kauli inaweza kuwa ni ukafiri, au uzushi, au uovu, na msemaji asiwe kafiri au mzushi au muovu, ila baada ya kutimia kwa sharti na kutokuwepo kwa vizuizi. (Kama tulivyoeleza hapo awali).

Ama kuhusu kauli; ziko ambazo ni ukafiri, na zingine ni uzushi tu wala si ukafiri, na ziko ambazo wanachuoni wanamitazamo tofauti….mpaka katika kauli yake: Na ama kuhusu kulihukumu kundi maalum; Ndiyo, yako makundi yaliyotoka katika Uislamu moja kwa moja kwa itifaki ya wanachuoni wote, hata kama yatajinasibisha katika Uislamu kwa muonekano wake; kama vile: Waliochupa mipaka katika Jahamiyya (wanaokanusha sifa za Mwenyezi Mungu) na Waliochupa mipaka katika Mashia (kama Shia Ithna-sharia, na Shia Ismaili, na Mabohora)…….na Makadiani, na mfano wao, amesema Imam Bin Qayyim: **"Na ama waliochupa mipaka katika Jahamiyya, na waliochupa mipaka katika Raafidhwa (Mashia) makundi haya hayana chochote**

[4] Ni Muhadhiri katika chuo kikuu cha Qasswim, nchini Saud Arabia.

**katika Uislamu"** Yaani: Si Waislamu.

Na anayejinasibisha miongoni mwao katika Uislamu kwa muonekano wake hukumu yake ni sawa na hukumu ya wanafiki, amesema Sheikhul Islami Bin Taimiyya: **"Na hawa (yaani: Mashia kundi la Qaraamitwa, na mfano wao) laa shaka hawa sio miongoni mwa yale makundi sabini na mbili, na wanapodhihirisha Uislamu lengo lao ni wawe wanafiki kama wale wanafiki waliokuwa katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake"**[5]

Anasema Sheikhul-Islami bin Taimiyya: **"Na ukweli wa mambo katika hilo nikuwa; kauli inaweza kuwa ni ukafiri, akaitwa kafiri mwenye kuisema, tukasema: Atakayesema kadhaa huyo ni kafiri, lakini mtu maalum aliyetamka kauli hiyo hahukumiwi kuwa ni kafiri, mpaka afikishiwe hoja na ukweli ambao anakufuru mwenye kuuacha"** [6]

[5] Rejea: Maqaalatul-Firaq Uk 49

[6] Rejea: Majmuu'ul-Fataawa (23/345)

# SEHEMU YA PILI

## Vitenguzi vya Uislamu

Tambua ndugu yangu Muislamu, Mwenyezi Mungu akurehemu, kuwa kama ambavyo ibada zinavitenguzi vyake ambavyo mtu akivifanya hata angefanya ibada nzuri na nyingi kiasi gani hizo ni sawa na mchezo, kama ambavyo mtu akitengukwa na Udhu hakuna swala yoyote itapokelewa kwake hata angeswali mara elfu moja, hali kadhalika Uislamu una mambo ambayo Muislamu akifanya moja kati ya hayo, basi atakuwa kauharibu Uislamu wake, hata kama atadai kuwa yeye ni Muislamu, na akafanya matendo mema na kuwa na muonekano wa kiislamu.

Amesema Sheikh bin Baazi Allah amrehemu katika Ufafanuzi wa vitenguzi vya Uislamu: "....Yanayouchafua Uislamu yako sehemu mbili:

1. Sehemu ya kwanza: Yanatengua itikadi hii na kuibatilisha, na mfanyaji wake anakuwa kafiri.
2. Sehemu ya pili: Yanaipunguza imani hii na kuidhoofisha.

Sehemu ya kwanza yanayoibatilisha imani hii na kuiharibu na mfanyaji wake anakuwa karitadi na kutoka katika Uislamu huitwa: Vitenguzi au vibatilishi, hivyo, vitenguzi

vya Uislamu: Ni kauli au kitendo kinachopelekea mtu kuritadi na kutoka ndani ya Uislamu.

Na kitenguzi kinaweza kuwa kauli, au kitendo, au itikadi, au inaweza kuwa shaka, hivyo mtu anaweza kuritadi kwa kauli anayoitamka, au kwa kitendo anachokifanya, au kwa itikadi anayoiitakidi, au kwa shaka inayojitokeza kwake, mambo yote haya manne ndiyo hutokea kwayo kitenguzi kinachochafua itikadi na kuibatilisha, na wameyataja wanachuoni katika vitabu vyao na mlango wakauita (Mlango wa hukumu ya mwenye kuritadi): Naye ni yule anaye kufuru baada ya kuwa Muislamu".

Kisha Sheikh akaendelea kusema: Na kukufurisha haku tamkwi ila kwa ubainifu; lazima ujue uhalisia wa mtu anayekufurishwa, na matendo yake na kauli zake, ili uweze kubainisha sababu za ukafiri wake, lazima akufurishwe kwa elimu…."

Na akasema: "Kuingia ndani ya Uislamu ni jambo jepesi, na kutoka pia ni jambo jepesi mno, na hutokea kwa wingi"

Na akasema: "Na makusudio yake nikuwa kupatikana kwa kitenguzi miongoni mwa vitenguzi vya Uislamu kunabatilisha yale aliyonayo miongoni mwa mambo ya Uislamu yote".[7]

---

[7] Rejea: Subulus salaami sharhu Nawaaqidhwul-Islaami (16-17)

## Kitenguzi cha Kwanza

Amesema Imamu Muhammadi bina Abdil Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: “Kitenguzi cha kwanza: **Ni kufanya shirki katika ibada ya Mwenyezi Mungu peke yake asiyekuwa na mshirika, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu**:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغۡفِرُ أَن يُشۡرَكَ بِهِۦ وَيَغۡفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُۚ وَمَن يُشۡرِكۡ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱفۡتَرَىٰٓ إِثۡمًا عَظِيمًا ٤٨﴾ [سورة النساء:٤٨].

**“Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa (na kitu kingine) na anasamehe yasiyokuwa hayo kwa amtakaye, na atakayemshirikisha Mwenyezi Mungu atakuwa amezua dhambi kubwa”** [An-Nisaa: 48, na 116].

Na amesema Mtukufu:

﴿إِنَّهُۥ مَن يُشۡرِكۡ بِٱللَّهِ فَقَدۡ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِ ٱلۡجَنَّةَ وَمَأۡوَىٰهُ ٱلنَّارُۖ وَمَا لِلظَّٰلِمِينَ مِنۡ أَنصَارٍ ٧٢﴾ [سورة المائدة:٧٢].

**“Bila shaka anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharamishia pepo, na mahala pake ni Motoni, na waliodhulumu hawatokuwa na wa kuwanusuru”** [Maaida: 72].

Na inaingia hapa kuchinja kwa lengo la asiyekuwa Mwenyezi Mungu, kama anayechinja kwa ajili ya Majini au kwa ajili ya kaburi”.

## Maana ya ibada

Amesema bin Baazi: “Ibada kwa Lugha ya Kiarabu: Ni kujidhalilisha na kujinyenyekeza na kujidhoofisha.....utiifu wetu kwa Mwenyezi Mungu umeitwa ibada kwa sababu tunautekeleza kwa udhalili na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na Kutukuka....”

Na akasema: “Ibada hazijulikani kwa rai za watu, bali ni kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na Kutukuka”.

Ametaja Sheikhul Islami bin Taimiyya Mwenyezi Mungu amrehemu kuwa: **“Ibada ni jina linalokusanya kila anacho kipenda Mwenyezi Mungu na kukiridhia, miongoni mwa kauli na matendo ya wazi na ya siri”** Na hii inaonyesha kuwa ibada inamaanisha: Utiifu kamili kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa amri na makatazo na kauli na matendo, na maisha ya mtu yasimame katika sheria ya Mwenyezi Mungu, ahalalishe alichokihalalisha Mwenyezi Mungu, na aharamishe alichokiharamisha Mwenyezi Mungu, na ajishushe katika mwenendo wake na matendo yake na harakati zake zote katika sheria za Mwenyezi Mungu, na ajivue na hadhi na majivuno na vishawishi vya matamanio ya nafsi yake, ili

wawe sawa katika hili watu wote, mtu binafsi na jamii nzima, mwanaume na mwanamke, hawezi kuwa mja wa Mwenyezi Mungu mtu yeyote aliyenyenyekea kwa Mola wake Mlezi katika baadhi ya sehemu ya maisha yake, na akamnyenyekea kiumbe katika sehemu nyingine, atakaye jishusha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na akamtii, na akahukumiwa kwa wahyi wake, basi huyu ndio mchamungu hasa, na atakayejishusha kwa asiyekuwa yeye, na aka hukumiana na watu kwa sheria isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, basi atakuwa kamuabudu Shetani na kamtii".

Na akasema: "...Kisha baada yakuwa akili haziwezi kupata ufafanuzi mzuri wa ibada, kama ambavyo haziwezi kujua hukumu, zikiwemo amri na makatazo kwa ufafanuzi mzuri, basi Mwenyezi Mungu Mtukufu akatuma Mitume na aka teremsha Vitabu ili kubainisha jambo ambalo ndio sababu ya Mwenyezi Mungu kuwaumba viumbe".

Na akasema: Wamesema baadhi ya wema waliotangulia: "Atakayemuabudu Mwenyezi Mungu kwa mapenzi, na katika madai yake nikuwa anampenda Mwenyezi Mungu tu! Basi huyu ni mnafiki zandiki, na kwa nini hamuogopi Mwenyezi Mungu wala hamtarajii? Kwanza yeye ni nani mpaka asimhofu Mwenyezi Mungu na wala asimtarajie? Hali yakuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema kuhusu Mitume rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao:

﴿إِنَّهُمۡ كَانُواْ يُسَٰرِعُونَ فِي ٱلۡخَيۡرَٰتِ وَيَدۡعُونَنَا رَغَبٗا وَرَهَبٗاۖ ۝٩٠﴾ [سورة الأنبياء: ٩٠].

**“Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema, na wakituomba kwa shauku na hofu”** [Al-Anbiyaa: 90] Hakusema wanatuomba kwa mapenzi pekee, amesema: “Na wakituomba kwa shauku na hofu” Kwa shauku ya kuipata Pepo, na hofu kuogopa Moto, Mitume na Manabii na Waumini waliogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu na wakataraji thawabu zake, na wakampenda mapenzi ya kweli, yaliyowapelekea kumtii na kuacha kumuasi, hayakuwapelekea katika kuchupa mipaka au kujiona na kiburi, yaliwasukuma kumtii Mwenyezi Mungu na kumhofu, na kutamani yaliyoko kwake, ibada inakuwa kwa mapenzi na kwa matarajio, na kwa hofu, na si kwa kiburi na jeuri na kujikweza kwa watu”.

Na akasema: “Na kinacholiweka wazi zaidi swala hili nikuwa: Atakayemtii Mwenyezi Mungu katika baadhi ya mambo hali yakuwa amejichanganya na ushirikina, huyu anastahiki zaidi kukataliwa ibada zake, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu washirikina: **“Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu”** [Kaafiruun: 3,5] Akaikanusha kwao ibada kwa sababu ya ushirikina wao, na inafahamika kuwa wao humuabudu Mwenyezi Mungu peke yake wakati wa shida, na kwa Hija na Umra, na kutoa

sadaka baadhi ya nyakati na mfano wa hayo, lakini kwakuwa ibada hizi zilikuwa zimechanganyikana na ushirikina wakati wa raha, na kutoamini Akhera, na mengine mengi miongoni mwa aina za ukafiri ikafaa kukataliwa ibada hizo kwa wenye nazo".

Na akasema: "Na mnatakiwa kufahamu kuwa ibada ina gawanyika sehemu mbili"

1. Kumuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni dhambi kubwa, ambalo ndio huleta ushirikina mkubwa.
2. Na ibada ndogo ambayo huleta ushirikina mdogo, na kutokea kwa maasi.

**Kumtii asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika maasi ni uhalifu, lakini hilo linagawanyika sehemu mbili:**

1. Atakapomtii asiyekuwa Mwenyezi Mungu kwa kuliona hilo kuwa ni halali, na kwa kudai kuwa inafaa kwake kumtii asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika maasi, huku kutakuwa ni kuritadi, na ni uovu, na ni shari kubwa, na ukafiri mkubwa.
2. Na akimtii asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika maasi, na huku akijua kuwa anafanya makosa, na anamuasi Mwenyezi Mungu, kitendo hiki kitakuwa ni maasi tu na si kuritadi wala kutoka katika Uislamu, ufafanuzi huu ni lazima ufahamike kama walivyobainisha wanachuoni".

## Maana ya Ushirikina

Amesema Bin Baazi: “Uhalisia wa Ushirikina: Ni kumshirikisha asiyekuwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu katika ibada, kama Mawalii (watu wema) au Manabii au Majini, au Malaika, au Mawe, au Masanamu, au Mti, au kinginecho, hii ndio shirki kubwa… na vile vile zinaunganishwa na haya aina zote za ukafiri, zote hizo hukumu yake ni hukumu ya ushirikina, kama atakaye mtukana Mwenyezi Mungu au akamtukana Mtume wake, au akaifanyia mzaha dini, au akamvunjia heshima Mtume rehema na amani ziwe juu yake, au akautia dosari utume wake, au akapinga baadhi ya yale aliyoyawajibisha Mwenyezi Mungu Mtukufu miongoni mwa mambo yanayofahamika uwajibu wake ndani ya dini pasina shaka,… yote haya huitwa ukafiri, na huitwa kumshirikisha Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na Kutukuka”.

Na akasema: “Ushirikina: Ni kuelekeza baadhi ya ibada kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, kuzifanya baadhi yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na baadhi yake kwa asiyekuwa yeye, miongoni mwa Majini au Binadamu, au Malaika, au Masanamu, au Miti, au Nyota, au Mawe, au kinginecho katika viumbe, akawataka msaada, na kuwawekea nadhiri, au kuwachinjia, au kuwataka uokozi, na mfano wa hayo, atakayefanya hivyo basi atakuwa amemshirikisha Mwenyezi Mungu na atakuwa kamuabudu pamoja naye kiumbe mwingine,

na atakuwa kabatilisha kwa hilo shahada yake ya "Laa ilaaha illa llaah Muhammadan Rasuulullaah" (Hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammadi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu)".

## Tofauti kati ya Mshirikina na Kafiri

Na aliulizwa Sheikh: Je kati ya Ushirikina na ukafiri kuna tofauti?

Akajibu: "Mara nyingi ukafiri hutumika katika kuipinga haki, na ushirikina katika kuielekeza ibada yoyote kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu..."

Na kwa hayo tuliyotaja inafahamika kuwa ushirikina uliofichikana hautoki katika aina hizi mbili: **Shirki kubwa, na Shirki ndogo,** na ikiitwa shiriki iliyofichikana ni sawa, kwani shirki huwa iliyofichikana na ya wazi.

**Ya wazi:** Kuwaomba wafu na kutaka msaada kwa wafu, na kuwawekea nadhiri na mfano wa hayo.

**Na iliyofichikana:** Ni kile kinachokuwa ndani ya nyoyo za wanafiki, wanaswali pamoja na watu, na wanafunga pamoja na watu, na hali ndani mwao ni makafiri, wanaitakidi kufaa kuabudiwa Masanamu, na wako katika dini ya washirikina, huu ndio ushirikina uliofichikana, kwa sababu uko ndani ya nyoyo" Mwisho.

Na akasema: “Na kwa Muhtasari: Lazima katika shahada mbili kuwe na ukweli, na yakini, na kuyafanyia kazi yanayotakiwa na shahada hizo, ama ilimradi tu mtu anatamka shahada mbili na huku anamuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu au anatukana dini, au anaharamisha aliyoyawajibisha Mwenyezi Mungu, hilo halimnufaishi chochote; kwani wanafiki huitamka shahada, na hali yakuwa watakuwa katika tabaka la chini kabisa la Moto, na waabudu Makaburi leo huitamka shahada, na hali yakuwa wao ndio Makafiri wakubwa kuliko watu wote, kama wanaomuabudu Al-Badawi [8], na wanaomuabudu Husein (kama Mashia), na wanaomuabudu Abdul-Qadiri Jailani [9], na waabudu Masanamu”.

Na akasema: “Hairuhusiwi kwa Muislamu yeyote kuziomba sifa za Mwenyezi Mungu, kwa mujibu wa wanachuoni wote, kama kusema: Ewe Uso wa Mwenyezi Mungu, au ewe Elimu ya Mwenyezi Mungu, au ewe Rehema za Mwenyezi Mungu, na mfano wa hayo” “Na sifa huombwa kwa lengo la kumfikia Mwenyezi Mungu (kutawasali) kama kauli ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake: “Ninajilinda kupitia radhi zako, dhidi ya ghadhabu zako, na

[8] Ni mtu anayedaiwa kuwa Walii, alizaliwa Morocco na akafia Misri, Mwaka: 675.H, sawa na 1276.G.

[9] Huyu ni katika wanachuoni wakubwa, na wachamungu katika zama zake, na alikuwa ni mtu wa Sunna, amefariki mwaka 561.H. sawa na mwaka 1139.G, huko Iraq.

kwa msamaha wako dhidi ya adhabu yako” lakini hapasemwi: Ewe radhi ya Mwenyezi Mungu niridhie mimi, ewe utukufu wa Mwenyezi Mungu ninusuru mimi”.

**Maswala Muhimu:** Na inaondolewa katika hayo kumuomba aliye hai aliyepo ulipo katika yale anayoyaweza, kwani hilo si katika ushirikina, kwa kauli yake Mtukufu katika kisa cha Nabii Mussa na Mkopti:

﴿فَٱسۡتَغَٰثَهُ ٱلَّذِي مِن شِيعَتِهِۦ عَلَى ٱلَّذِي مِنۡ عَدُوِّهِۦ ١٥﴾ [سورة القصص:١٥].

**“Akamtaka msaada yule ambaye ni katika jamaa zake, dhidi ya yule ambaye ni katika adui zake”** [Al-Qaswas: 15]

Kwa sababu kila mwanadamu huhitaji msaada wa ndugu zake, katika yale anayoyahitaji vitani na kwingineko, katika yale wanayoyaweza, hilo si katika shirki, bali hilo ni katika mambo ya halali, na msaada huo unaweza kuwa Sunna, na unaweza kuwa wajibu kulingana na ushahidi wa kisheria”.

## Kitenguzi cha pili

Amesema imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **"Cha pili: Atakayeweka kati yake na Mwenyezi Mungu wawakilishi, anaowaomba na kuwataka shifaa (ponyo), na kuwategemea, huyu atakuwa kakufuru kwa itifaki ya wanachuoni wote".**

Amesema bin Baazi: "Na katika itikadi chafu ni kuyategemea Masanamu, na Miti, na Mawe na Makaburi, na Nyota, na vinginevyo, na kuviomba kinyume na Mwenyezi Mungu na kuvitaka msaada, na kuviwekea nadhiri, na mfano wa hayo miongoni mwa yale yaliyotokea katika zama za ujinga, na ilikuwa itikadi yao ni kwamba; kuamini kwao kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Mola wao Mlezi inatosha, nakwamba haabudiwi isipokuwa kupitia wawakilishi, na wakisema kuwa: Wao wanamatendo mabaya, na sifa mbaya zinazowafanya wasistahiki kumuelekea Mwenyezi Mungu moja kwa moja, bali lazima kuwe na wawakilishi, kama wanavyowakilisha mawaziri na wakuu wa mikoa raia wa kawaida kwa Wafalme na Maraisi, basi wanamfananisha Mwenyezi Mungu na viumbe wake, kisha wanamshirikisha Aliyetakasika na Kutukuka, wakakusanya kati ya kumfananisha na viumbe na kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na viumbe, na yote hayo ni kwa sababu ya uchache wa elimu na ujinga totoro, na kuwaiga baba zao na babu zao".

Mpaka aliposema: "...Ni mara chache sana kukuta katika miji mingi ulimwenguni wenye utambuzi na elimu na msingi huu mkubwa, bali unaweza kukuta mtu anayeashiriwa kwa vidole, na watu wanasema kuwa ni mwanachuoni, pamoja na hilo ni miongoni mwa watu wanaoyatukuza Makaburi, jambo ambalo Mwenyezi Mungu hakulifanya kuwa sheria, na anawaomba waliomo, na anataka msaada kwao, na kutia nadhiri kwao, na mfano wa hayo".

"Na washirikina wanajua fika kabisa kuwa waabudiwa wao hawaumbi wala hawatoi riziki, na kwamba hata wao ni wahitaji, na kwamba wanamilikiwa, lakini Mwenyezi Mungu hakuwapa udhuru kwa hilo, na akawakufurisha kwa kutaka kwao uombezi kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu".

**"Ikiwa atasema msemaji katika hawa washirikina wa sasa:** Sisi hatukusudii kuwa hao wananufaisha wao kama wao, na kuponya wagonjwa wetu, au kutusaidia wao kama wao, au wanamdhuru adui wao kama wao, bali tunakusudia kutaka utetezi wao mbele ya Mwenyezi Mungu, katika hilo.

**Jawabu waambiwe kuwa:** Bila shaka hili mnalolifanya ndio lengo haswa la Makafiri wa mwanzo na dhumuni lao, na wala si lengo lao kwamba miungu yao inaumba au inatoa riziki au inanufaisha au inadhuru yenyewe; kwani

hilo linabatilishwa na kile alichokisema Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'ani kuhusu wao, bali walikusudia kupata utetezi wao, vyeo vyao, na kukurubishwa kwao kwa Mwenyezi Mungu ukaribu mkubwa, kama alivyosema Mtukufu katika Suratu Yunus amani iwe juu yake:

﴿وَيَعۡبُدُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمۡ وَلَا يَنفَعُهُمۡ وَيَقُولُونَ هَٰٓؤُلَآءِ شُفَعَٰٓؤُنَا عِندَ ٱللَّهِ﴾

**"Na wanaabudu kinyume na Mwenyezi Mungu yale yasiyowadhuru wala kuwanufaisha, na wanasema; hawa ndio waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu"** Mwenyezi Mungu akawajibu kwa kauli yake Mtukufu:

﴿قُلۡ أَتُنَبِّـُٔونَ ٱللَّهَ بِمَا لَا يَعۡلَمُ فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَلَا فِي ٱلۡأَرۡضِۚ سُبۡحَٰنَهُۥ وَتَعَٰلَىٰ عَمَّا يُشۡرِكُونَ ١٨﴾ [سورة يونس:١٨].

**"Sema: Je, mnampa habari Mwenyezi Mungu za yale asiyoyajua katika mbingu wala katika Ardhi, Subhaanahuu Wataala! Ametakasika na ametukuka na hao wanaomshirikisha naye"** [Yunus: 18] Akaweka wazi Mtukufu kuwa Yeye hamtambui katika mbingu wala katika Ardhi muombezi yeyote mbele yake, kwa namna ambayo wanaikusudia washirikina, na asichojua Mwenyezi Mungu

uwepo wake basi hicho hakipo, kwa sababu yeye Mtukufu hakifichiki chochote kwake”.

Na amesema Mtukufu:

﴿ذَٰلِكُمُ ٱللَّهُ رَبُّكُمۡ لَهُ ٱلۡمُلۡكُۚ وَٱلَّذِينَ تَدۡعُونَ مِن دُونِهِۦ مَا يَمۡلِكُونَ مِن قِطۡمِيرٍ ١٣ إِن تَدۡعُوهُمۡ لَا يَسۡمَعُواْ دُعَآءَكُمۡ وَلَوۡ سَمِعُواْ مَا ٱسۡتَجَابُواْ لَكُمۡۖ وَيَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ يَكۡفُرُونَ بِشِرۡكِكُمۡۚ وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثۡلُ خَبِيرٖ ١٤﴾ [سورة فاطر:١٣-١٤].

**“Huyo kwenu nyinyi ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi, Ufalme ni wake, na hao mnaowaomba badala yake hawamiliki hata ngozi ya kokwa la tende.** [13] **Hata mkiwaomba hawasikii maombi yenu, na hata wakisikia hawakujibuni, na Siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu, na hapana atakayekupa habari vilivyo kama Yeye Mjuzi wa habari”** [Faatir: 14-15] Akayaita Mwenyezi Mungu maombi yao kwao ni ushirikina, pamoja nakuwa wao hawakuwaomba ila tu wawe waombezi wao, hawakuwaomba ati kwa sababu wanamiliki madhara na manufaa, au wanaumba, au wanatoa riziki, bali alisema Mwenyezi Mungu kuhusu wao:

﴿مَا نَعۡبُدُهُمۡ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَآ إِلَى ٱللَّهِ زُلۡفَىٰٓ ٣﴾ [سورة الزمر:٣].

**“Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu”** [Zumar: 3] Na wakasema: **“Hawa ni waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu”** [Yunus: 18] Akawakufurisha kwa hilo, na wao hawakuitakidi isipokuwa ni waombezi wao waliokaribu na Mwenyezi Mungu, na hawakudai kuwa wao wanaumba au wanatoa riziki, au wananufaisha au wanadhuru”.

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُواْ مِن دُونِهِۦٓ أَوۡلِيَآءَ مَا نَعۡبُدُهُمۡ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَآ إِلَى ٱللَّهِ زُلۡفَىٰٓ إِنَّ ٱللَّهَ يَحۡكُمُ بَيۡنَهُمۡ فِي مَا هُمۡ فِيهِ يَخۡتَلِفُونَۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَهۡدِي مَنۡ هُوَ كَٰذِبٞ كَفَّارٞ ٣﴾ [سورة الزمر:٣].

**“Na wale wanaowafanya kinyume na Mwenyezi Mungu kuwa ni walinzi, wakisema: Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao katika yale wanayohitilafiana, hakika Mwenyezi Mungu hamuongoi aliye muongo Kafiri”** [Zumar: 3] Kawaita Waongo, Makafiri, hii inaonyesha kuwa kuwaabudu kwao wao kwa kutafuta ukaribu ni ukafiri na kuritadi, hata kama hawakusema kuwa hao wanaumba au wanatoa riziki, wanapowaomba na wanapowataka msaada na wakawawekea nadhiri na wakawachinjia kwa lengo la kujikurubisha kwamba wao wanawaweka karibu, huu ndio ukafiri

walioufanya washirikina, na ndio maana akawaita Waongo, Makafiri, walioongopa kuwa wao wanawaweka karibu na Mwenyezi Mungu, na wakakufuru kwa kitendo chao hiki”.

Na amesema Mtukufu:

﴿ وَمَن يَدۡعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ لَا بُرۡهَٰنَ لَهُۥ بِهِۦ فَإِنَّمَا حِسَابُهُۥ عِندَ رَبِّهِۦٓۚ إِنَّهُۥ لَا يُفۡلِحُ ٱلۡكَٰفِرُونَ ١١٧ ﴾ [سورة المؤمنون:١١٧].

**“Na anayemuomba pamoja na Mwenyezi Mungu mungu mwingine, hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hesabu yake iko kwa Mola wake Mlezi, kwa hakika Makafiri hawafanikiwi”** [Mu’minuun: 117] Kawaita kuwa ni Makafiri pamoja nakuwa hawakuwaabudu kwa sababu wananufaisha au wanadhuru, au wanasehemu ya kuleta manufaa, au kuzuia madhara, au wanaumba, bali waliwaabudu kwa madai yao nikuwa wao wanawaweka karibu zaidi na Mwenyezi Mungu, na wanawaombea.

**Na makusudio yake nikuwa:** Wanachuoni wote wamekubaliana kuwa yeyote atakayemuabudu kinyume na Mwenyezi Mungu: Sawa sawa liwe Sanamu, au Nabii, au mtu mwema au jini, au kinginecho, huyo ni kafiri moja kwa moja, hata kama anayeabudiwa atakuwa Nabii au mtu mwema, na haya ndio makubaliano ya wanachuoni wote, na ushihidi juu ya hilo kutoka katika kauli za Mwenyezi

Mungu Mtukufu na kauli za Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake uko wazi, na baadhi yake tayari umekwisha tangulia.

**Na ama kauli ya muulizaji:** Wale wa zamani walisema: "Hatuwaabudu ila wapate kutujongeza" Hawa walikiri kuwaabudu, lakini hawa wa sasa hawasemi kama wanawawa abudu, lakini wanasema kuwa wao wanataka baraka kutoka kwao?

**Jibu hapa nikuwa:** Kinachozingatiwa hapa ni uhalisia na maana, na si kutofautiana kwa matamshi, wakisema: Hatuwaabudu bali tunataka baraka kwao, hilo haliwasaidii, madamu wamefanya kitendo cha washirikina waliokuwa kabla yao, na hata wasipoliita hilo kuwa ni ibada, bali wakaliita kuwa ni kutawasali (kuwakilishwa) au kutaka baraka, kufungamana na asiyekuwa Mwenyezi Mungu na kuwaomba wafu na Manabii, na watu wema, na kuwachinjia, au kuwasujudia, au kuwataka msaada, yote hayo ni ibada, hata wakiyaita ni huduma, au wakayaita kinyume na hivyo, kwa sababu kinachozingatiwa ni uhalisia wa mambo na si majina, kama ilivyotangulia".

**Maswala Muhimu:** Ni ipi hukumu ya anayesema (Madadi Yaa fulani) Niokoe ewe fulani (kama wasemavyo Mashia: Madadi yaa Ali au Madadi yaa Husein, au Watu wa Kaadiria: Madadi yaa Jailani), je aliyetamka hivi anakufuru?

**Akajibu:** Ndiyo, hii ndio kazi ya Makuraishi wanasema: **"Hawa ni waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu"** Hawa hawakusema kuwa wanatunufaisha au wanatudhuru, au wao ni miungu wetu, walisema: **"Hawa ni waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu"** na wakasema: **"Hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu"** Hawakusema: Ili watunufaishe au watudhuru".

Na akasema: "Kuomba utetezi na uombezi kwa mtu aliyeko hai na upo naye, ni swala linalofaa Duniani na Akhera, kama mtu kusema: Ewe ndugu yangu niombee kwa Mwenyezi Mungu, hii inafaa kwa Mtume na asiyekuwa Mtume, haikemewi kwa makubaliano ya wanachuoni wote".

## Kitenguzi cha tatu

Amesema Imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **"Asiyewakufurisha washirikina, au akatia shaka katika ukafiri wao, au akaona kuwa madhehebu yao yako sawa, huyu atakuwa kakufuru kwa makubaliano ya wanachuoni wote".**

Amesema bin Baazi: "Tauhidi: Ni Kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada kwa imani, na kwa ukweli, na kwa matendo, si ilimradi maneno tu, ikiwa ni pamoja na kuitakidi kuwa ibada ya kuabudiwa asiyekuwa yeye ni

batili, na kwamba wanaoabudu asiyekuwa Yeye ni washirikina, na kujiepusha nao, kama alivyosema Aliyetakasika na Kutukuka:

﴿قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِيٓ إِبْرَٰهِيمَ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ إِذْ قَالُوا۟ لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَءَٰٓؤُا۟ مِنكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ
مِن دُونِ ٱللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ ٱلْعَدَٰوَةُ وَٱلْبَغْضَآءُ أَبَدًا حَتَّىٰ تُؤْمِنُوا۟ بِٱللَّهِ وَحْدَهُۥٓ إِلَّا قَوْلَ إِبْرَٰهِيمَ
لِأَبِيهِ لَأَسْتَغْفِرَنَّ لَكَ وَمَآ أَمْلِكُ لَكَ مِنَ ٱللَّهِ مِن شَىْءٍ ۖ رَّبَّنَا عَلَيْكَ تَوَكَّلْنَا وَإِلَيْكَ أَنَبْنَا وَإِلَيْكَ ٱلْمَصِيرُ ﴿٤﴾﴾

[سورة الممتحنة: ٤].

**"Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale walio kuwa pamoja naye, walipo waambia watu wao: Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayo yaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Tunakukataeni; na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu na nyinyi mpaka mtakapomuamini Mwenyezi Mungu peke yake. Isipokuwa kauli ya Ibrahim kumwambia baba yake: Hakika nitakuombea msamaha, wala similiki chochote kwa ajili yako mbele ya Mwenyezi Mungu. Mola wetu Mlezi! Juu yako tumetegemea, na kwako tumeelekea, na kwako ndio marejeo."** [Mumtahana: 3]

Na akasema Mtukufu:

﴿وَإِذْ قَالَ إِبْرَٰهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِۦٓ إِنَّنِى بَرَآءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ ﴿٢٦﴾ إِلَّا ٱلَّذِى فَطَرَنِى فَإِنَّهُۥ سَيَهْدِينِ ﴿٢٧﴾﴾ [سورة الزخرف:٢٦-٢٧].

**"Na pale Ibrahim alipomwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayo yaabudu.** [26] **Isipokuwa yule aliye niumba, kwani Yeye ataniongoa."** [Az-Zukhruf: 26-27]. Akajivua na kujitenga mbali na wale wanaoabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na yale wanayoyaabudu.

**Kinachokusudiwa nikuwa:** Lazima kumpwekesha Mwenyezi Mungu, kwa kumfanya kuwa pekee katika ibada, na kujitenga mbali na kumuabudu asiyekuwa Yeye, na wenye kumuabudu asiyekuwa Yeye, na ni lazima pia kuitakidi ubatili wa ushirikina".

**Maswala muhimu:** Mayahudi na Wakristo kwakuwa hawakumuamini Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, wamekuwa kwa hilo ni Makafiri wapotofu, na hata tukichukulia baadhi yao wapo wanaompwekesha Mwenyezi Mungu, ila wote ni wapotofu na ni Makafiri kwa itifaki ya Waislamu wote; kwa kutokumuamini kwao Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, ikiwa mtu atasema: Mimi ninamuabudu Mwenyezi Mungu pekee, na ninamsadikisha Muhammadi katika kila kitu, isipokuwa katika kuharamisha Zinaa, akaifanya kuwa ni halali, kwa hili moja tu, anakuwa

kafiri na damu na mali yake ni halali kwa itifaki ya Waislamu wote, na hivyo hivyo akisema Kuwa: Anamuamini Mwenyezi Mungu peke yake na anamuabudu pasina mwingine, na anawaamini Mitume wote, na hasa hasa Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, isipokuwa tu katika kuharamisha Ushoga, ambako ni kumuendea mwanaume kinyume na maumbile, kwa hili moja pekee atakuwa kafiri, na damu na mali yake ni halali kwa itifaki ya Waislamu wote".

Na akasema Sheikh: "Na mtu anamjua kafiri na batili aliyonayo kisha hamkufurishi, au akatia shaka juu ya ukafiri wake, hii inamaanisha huyu anapingana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wala haamini hukumu iliyotolewa na Mwenyezi Mungu juu yao ya Ukafiri, mfano kama Mayahudi na Wakristo, hawa ni Makafiri kwa ushahidi wa Qur'ani na Sunna, jambo la wajibu kwa watu wazima miongoni mwa Waislamu waitakidi ukafiri wao na upotovu wao, na asiyewakufurisha hao katika ukafiri wao anakuwa mfano wao; kwa sababu anakuwa kampinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na ana shaka na yale aliyoyaeleza Mwenyezi Mungu na Mtume wake...".

## Kitenguzi cha Nne

Amesema Imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **“Kitenguzi cha Nne: Atakayeitakidi kuwa usiokuwa muongozo wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake umekamilika kuliko muongozo wake, au kuwa hukumu isiyokuwa yake imekamilika kuliko hukumu yake, kama wale wanaoziona bora hukumu za wale wanaoabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu kuliko hukumu zake, basi huyu atakuwa kakufuru”.**

Tambua Ndugu msomaji kuwa hakuna awezaye kujua ni nini kinawafaa viumbe, na ni mahala gani na wakati gani kinawafaa, zaidi ya yule aliyewaumba, hivyo akateremsha sheria inayokwenda na nyakati zote na inayofaa kwa mataifa yote pasina ubaguzi wala kupitwa na wakati.

Amesema bin Qayyim Mwenyezi Mungu amrehemu: **“Bila shaka sheria imejengwa na imewekwa katika misingi ya hekima inayozingatia masilahi ya waja katika maisha, na marejeo yao, nayo ni uadilifu yote, na ni huruma yote, na ni masilahi yote, na ni hekima yote; na kila maswala yaliyotoka katika uadilifu na kwenda katika dhuluma, na kutoka katika rehema kwenda kinyume chake, na kutoka katika masilahi kwenda katika madhara, na katika hekima kwenda**

**katika mchezo; hiyo si sheria, hata kama itaingizwa katika sheria kwa tafsiri nyingi”.** [10]

Amesema Bin Baazi Mwenyezi Mungu amrehemu: “...Haifai kwa Waislamu kujifananisha na maadui wa Mwenyezi Mungu wanafiki kwa kuhukumiana kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu na kuzuia hukumu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kila hukumu inayopingana na sheria ya Mwenyezi Mungu hiyo ni katika hukumu za kijinga, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿أَفَحُكْمَ ٱلْجَٰهِلِيَّةِ يَبْغُونَ ۚ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ ٱللَّهِ حُكْمًا لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٥٠﴾﴾ [سورة المائدة: ٥٠].

**“Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?”** [Maaida: 50] Na akaeleza Mtukufu kuwa kuhukumu kwa sheria isiyokuwa ile aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu ni ukafiri na dhuluma na ni uovu.

Na Aya hizi na zilizokuja na maana yake zinawawajibisha Waislamu kutahadhari kuhukumu kwa yale asiyoyateremsha Mwenyezi Mungu na kujitenga nayo, na kufanya haraka kwenda katika sheria ya Mwenyezi Mungu na Mtume

---

[10] Rejea: Aalaamul-Muwaqqiin Juzuu ya 3 uk 11

wake, na kukunjua kifua kwa hukumu hiyo, na kujisalimisha kwayo.”

Kisha akasema Mh. Sheikh: “Na mwenye kwenda kinyume na hukumu ya Mwenyezi Mungu ana hali mbili: Akienda kinyume na hukumu ya Mwenyezi Mungu kwa kulihalalisha hilo huyu ni kafiri na ameritadi, na akienda kinyume kwa sababu ya tamaa au matamanio, na huku akijua kabisa kuwa amekosea na kwamba ameasi, lakini amekwenda kinyume kwa sababu ya rushwa au udugu wa karibu, au mfano wa hayo, kwa hilo atakuwa ni muasi aliyekufuru ukafiri mdogo, na hii ni kwa mujibu wa alivyosema bin Abbasi na Mujaahid Mwenyezi Mungu awarehemu.”

**Maswala Muhimu:** Kanuni za nchi ikiwa haziendi kinyume na sheria hakuna tatizo, na pia huitwa mfumo, kila kanuni inayowanufaisha Waislamu na wala haipingani na sheria ya Mwenyezi Mungu hiyo haina tatizo, mfano kama sheria za usalama barabarani, au katika kesi, au katika sekta za kiserikali, au mahali popote... bila shaka hizo sheria ya Mwenyezi Mungu inaziruhusu; kwani kila ambacho hakikupingana na kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume wala itifaki ya Waislamu basi hicho hakina tatizo...; kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu ameifanya sheria ni yenye kukipangilia kila kitu, na katika sheria ya Mwenyezi Mungu ni kupangilia mambo, na mambo yasipuuzwe, yapangiliwe na yatiliwe maanani

mpaka watu waishi katika jambo lililo wazi, linalowezekana wao kuchukuliwa hatua na kuadhibiwa na kuwalipa kwa yale wanayoyafanya kama shari au heri".

## Hukumu ya aliyedharurika kuhukumiana kwa kanuni

Na Sheikh akasema pia: "Nataka kukuelekeza kuhusu swali lako, huyu anayeuliza kuhusu mtu anayehukumiana kwa hakimu anayehukumu kwa kanuni za kuwekwa na watu, na wala hawezi kuifikia haki yake isipokuwa kwa kuhukumiwa na sheria hizo, je, anakuwa kafiri au la? Nakupa faida kwa hilo: Akilazimika kufanya hivyo hawi kafiri, lakini hatakiwi kuhukumiana kwao ila wakati wa dharura, pale inaposhindikana kwake kuipata haki yake ila kwa hilo, na hana haki ya kuchukua kinyume na yale yaliyohalalishwa na sheria (asichukue haramu), Mwenyezi Mungu awape taufiki watu wote" Mwisho. [11]

[11 ] Rejea: Subulus Salaam Sharhu Nawaaqidhul-Islami cha bin Baaz Uk 130

## Kitenguzi cha tano

Amesema Imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **"Kitenguzi cha Tano: Atakaye chukia chochote katika yale aliyokuja nayo Mtume rehema na amani ziwe juu yake hata kama atakifanyia kazi, atakuwa kakufuru kwa makubaliano ya wanachuoni wote, na ushahidi wa hilo ni kauli yake Mtukufu:**

﴿ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أَنزَلَ اللَّهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ ﴿٩﴾﴾ [سورة محمد:٩].

**"Hayo ni kwa sababu waliyachukia yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao."** [Muhammad: 9]

**Aliulizwa Sheikh bin Baazi:** Ikiwa mtu atachukia kitu lakini hakupinga, akachukia mfano kuharamishwa kunywa pombe.

**Akajibu:** "Atakayechukia sheria ya Mwenyezi Mungu yanaporomoka matendo yake: **"Hayo ni kwa sababu waliyachukia yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao."** [Muhammad: 9] atakaye chukia Swala hata akiswali, au akachukia Hija hata akihiji, au akachukia uharamu wa Zinaa au pombe anakufuru kwa hilo."

Na akasema katika Hadithi: “Tulimpa ahadi ya utiifu Mtume rehema na amani ziwe juu yake, juu ya usikivu na utiifu, katika furaha na machukizo”: Maana yake nikuwa: Wao watasikiliza na kutii hata kama jambo hili wanalichukia na linawawia vigumu kwa sababu ya ufakiri wao, au kwa sababu nyinginezo, wakati wowote atakapoamrisha Mtume watamtii, na hata kama ikiwa ni jambo litakaloweza kuwadhuru... na hilo ni upande wa kukarahika kwa tabia ya asili ya kimaumbile, kulingana na tabu za kawaida na si upande wa kulazimishwa, kulazimishwa nikuwa ana shurutishwa juu ya jambo hili au anatishiwa juu ya jambo alifanye, nalo si jambo la kisheria, hii ndio maana ya kulazimishwa.”

**Maswala Muhimu:** Na akasema: Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu Maswahaba:

﴿لِيَغِيظَ بِهِمُ ٱلۡكُفَّارَۗ﴾ [سورة الفتح:٢٩].

**“ili awakasirishe kwao Makafiri”** [Al-Fat-hi: 29] Kwa hivyo, atakayekasirishwa na Maswahaba, au akachukizwa na Maswahaba, huyu hakuna shaka juu ya ukafiri na upotovu wake, wale wanaowachukia Maswahaba kwa ujumla na wanawatukana Maswahaba kwa ujumla hawa hawawezi kuwa Waislamu abadani!, ama kuwatukana baadhi yao

ikipatikana sehemu ya chuki ya kuwachukia, huu ni uovu na ni upotovu, lakini hauwi ukafiri mkubwa.

**Maswala Muhimu:** Akasema: “Wale wanaopiga vita uke wenza (Ndoa ya zaidi ya mke mmoja) miongoni mwa wanawake na wanaume hawa wanakinzana na sheria, na inahofiwa kwao kujivua katika dini -Mwenyezi Mungu atuepushe- kwa kuchukia kwao sheria aliyoiweka Mwenyezi Mungu, na kwa kudai kwao kuwa hilo linaleta madhara katika jamii, au mengineyo katika madai yao, mimi ninahofia kwa hawa kuritadi na kutoka katika dini yao bila ya wao kujua; kwa sababu wanakwenda kinyume na sheria ya Mwenyezi Mungu, na wanakwenda kinyume na kitabu cha Mwenyezi Mungu, na wanakwenda kinyume na Mtume wa Mwenyezi Mungu, huu ni munkari (uovu) mkubwa”.

Na akasema pia: Atakayechukia kuoa zaidi ya mke mmoja, na akadai kuwa kutokuoa mke zaidi ya mmoja ndio bora, huyu ni kafiri na ameritadi katika Uislamu; kwa sababu -Mwenyezi Mungu atuepushe- huyu anapinga hukumu ya Mwenyezi Mungu na anachukia sheria ya Mwenyezi Mungu... na atakayechukia aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu yanaporomoka matendo yake, mtu anayechukia kuoa wake wanne, na akaona kuwa sheria imefanya dhuluma na inamapungufu, au hukumu ya Mwenyezi Mungu katika hili ina mapungufu, au si nzuri, au wanachokifanya katika miji ya Wakristo kubaki na mke

mmoja ndio bora na afadhali, maneno haya yote ni kuritadi na kutoka ndani ya Uislamu... kilichopo nikuwa: Mtu yeyote atakayechukia yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu na aliyoyafanya kuwa sheria huyo karitadi, na vile vile atakayeyapenda na kuyaridhia aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu, na akasema kuwa: Ni mambo mazuri na yanafaa, kama Zinaa na wizi, anakuwa kafiri pia” [12]

Na akasema: “Miziki na vinavyopumbaza huotesha unafiki, na huotesha ndani ya nyoyo kuichukia haki, na kuichukia Qur’ani, na kuchukia vikao vya kielimu na vya kutajwa Mwenyezi Mungu, na kuchukia ibada na swala, na kuridhia kila uovu na kila balaa, hii ni katika athari zake ndani ya nyoyo mpaka mioyo huota giza na kuwa mieusi”.

## Kitenguzi cha Sita

Amesema Imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **“Kitenguzi cha Sita: Atakayekifanyia mzaha kitu chochote katika dini ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake, au thawabu yake au adhabu yake atakuwa amekufuru, na ushahidi wa hilo ni kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:**

[12 ] Rejea: Subulus Salaam Sharhu Nawaaqidhul-Islami cha bin Baaz Uk 143

﴿ وَلَئِن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ ۚ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ ﴿٦٥﴾ ﴾ [سورة التوبة:٦٥].

**"Na ukiwauliza, bila shaka watasema: Hakika tulikuwa tukipiga porojo na kucheza tu. Sema: Kwani mlikuwa mkimfanyia masihara Mwenyezi Mungu, na ishara zake, na Mtume wake?"** [Tauba: 65]

Amesema bin Baazi: "Kimekwisha tamka kitabu kitukufu cha Mwenyezi Mungu kukufuru kwa atakayemfanyia mzaha Mtume rehema na amani ziwe juu yake, au chochote katika kitabu cha Mwenyezi Mungu kitukufu na sheria yake iliyojaa hekima, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ ﴿٦٥﴾ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ ۚ ﴿٦٦﴾ ﴾ [سورة التوبة:٦٥-٦٦].

**"Sema: Kwani mlikuwa mkimfanyia masihara Mwenyezi Mungu, na ishara zake, na Mtume wake?** [65] **Msitoe udhuru. Hakika mmekwishakufuru baada ya kuamini kwenu!"** [Tauba: 65-66] Aya hii tukufu ni ushahidi wa wazi na ni hoja ya nguvu juu ya ukafiri wa mwenye kumfanyia mzaha Mwenyezi Mungu au Mtume wake au Kitabu kitukufu".

**Nasema:** Wachukue tahadhari wale wanaotengeneza maudhui zenye uhusiano wa dini katika mitandao ya kijamii, kwa lengo kuwachekesha watu na kupata wafuasi (followers) wengi au kupendwa (Likes) za watu wengi, sawa sawa lengo lao liwe ni kukejeli dini au la! kwani dini haifanyiwi mzaha wala maigizo.

**Nasaha zangu:** Wafute maudhui walizozituma katika mitandao na wamuombe Mwenyezi Mungu msamaha, kwani wasipofanya hivyo zitabaki kuwa dhima kwao mbele ya Mwenyezi Mungu, na kwa Waislamu wote kuacha kuchekelea uovu huu na kuupenda (kuu Like) au kuutuma kwa watu wengine kwani nikuwasaidia watu katika maovu, na hili tumekatazwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kama alivyosema:

﴿وَتَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡبِرِّ وَٱلتَّقۡوَىٰۖ وَلَا تَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡإِثۡمِ وَٱلۡعُدۡوَٰنِۚ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَۖ إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلۡعِقَابِ ٢﴾ [سورة المائدة:٢].

**“Na saidianeni katika wema na ucha Mungu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika, Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.”** [Maaida: 2]

## Hukumu ya kukaa na watu wanaoifanyia mzaha dini

Amesema bin Baazi: "Atakapokaa nao na hakuwakemea na akanyamaza, hii inaonyesha amekubali, na vinginevyo ni wajibu kwa atakayekaa na mtu anayezungumza batili na kuipinga haki, na kuikejeli haki, asiendelee kukaa, bali asimame na aondoke ikiwa hawezi kukemea kwa ulimi, na vinginevyo anatakiwa kukemea na kubainisha kosa la aliyezungumza batili, ama atakapoendelea kukaa na akanyamaza, hii maana yake amekubali, Laa haulaa walaa Quwwata illa billaah (hakuna hila wala nguvu isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu): **"Hakika nyinyi mtakuwa mfano wao"** Qur'ani inaonyesha kutopewa udhuru, bali ni ima azungumze au anyanyuke, na atakapokemea na akabainisha batili, basi atakuwa katimiza wajibu wake...".

## Kitenguzi cha Saba

Amesema Imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **"Kitenguzi cha saba: Uchawi, na miongoni mwa uchawi ni kugeuza kitu au kukiunganisha, atakayeufanya, au akauridhia, basi amekufuru, na ushahidi wa hilo ni kauli yake Mtukufu:**

﴿وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ يَقُولَآ إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ ۖ ﴿١٠٢﴾﴾ [سورة البقرة:١٠٢].

**“Na hawamfundishi yeyote mpaka wamwambie, hakika sisi ni mtihani, basi usikufuru”** [Baqara: 102].

Amesema bin Baazi: Uchawi ni: Vifundo na makombe wanayoyafanya wachawi na wanapuliza katika vifundo vyao, na vitu vingine baadhi yake ni madawa wanayoyakusanya, na vingine wanavipokea kutoka kwa Majini na Mashetani ili wavitekeleze kwa yule wanayemtaka”.

“Nao ni ukafiri wa wazi kwa ushahidi wa Qur’ani kiasi kwamba alisema Mtukufu:

﴿وَٱتَّبَعُواْ مَا تَتۡلُواْ ٱلشَّيَٰطِينُ عَلَىٰ مُلۡكِ سُلَيۡمَٰنَۖ وَمَا كَفَرَ سُلَيۡمَٰنُ وَلَٰكِنَّ ٱلشَّيَٰطِينَ كَفَرُواْ يُعَلِّمُونَ ٱلنَّاسَ ٱلسِّحۡرَ ﴿١٠٢﴾﴾ [سورة البقرة:١٠٢].

**“Na wakafuata yale wanayoyasoma Mashetani katika Ufalme wa Suleiman, na wala hakukufuru Suleiman, lakini Mashetani ndio waliokufuru wakiwafundisha watu uchawi”** [Al-Baqara: 102] Akaeleza Mtukufu kuhusu ukafiri wao ni kwa kuwafundisha kwao watu uchawi”.

**Maswala Muhimu:** Amesema: “Na hukumu ya mchawi ambaye anafahamika kuwa anawafanyia watu kiini macho, au yanapatikana madhara kwa watu kwa sababu ya mambo yake ya uchawi wa kuroga macho, au kughushi, au kumpendezesha mwanaume kwa mke wake na mwanamke kwa mume wake, au kinyume chake miongoni mwa mambo

yanayowadhuru watu, wakati wowote litakapothibitika hilo kwa ushahidi wa wazi mbele ya mahakama za kisheria, basi ni wajibu kuuliwa kwa mchawi huyu, na toba yake haikubaliki hata akitubia."

**Na makusudio yake nikuwa:** Akija katika sura isiyokuwa na hila wala vitimbi, basi mfano wa huyu itakubaliwa toba yake; kwa sababu amekuja kwa lengo la kutubia na kujutia, ni kama wengineo katika makafiri miongoni mwa wale wanaokuwa na mwanzo mbaya, kisha Mwenyezi Mungu akawaneemesha kwa toba pasina kulazimishwa wala kushitakiwa na yeyote".

**Na aliulizwa:** Kuhusu hukumu ya kumswalia mchawi na kumzika katika makaburi ya Waislamu baada ya kuuliwa?

**Akajibu:** Atakapouliwa haswaliwi, wala hazikwi katika makaburi ya Waislamu, anazikwa katika makaburi ya makafiri, na wala haoshwi, na havikwi sanda".

**Maswala Muhimu:** Amesema bin Baazi: "Mchawi akijulikana atalazimishwa kuyaondoa aliyoyafanya, ataambiwa: Ima uyaondoe uliyoyafanya au tukuuwe, akikiondoa kitu kile basi kiongozi (hakimu) atamuuwa, kwa sababu mchawi anauawa bila kupewa nafasi ya kutubia kwa mujibu wa kauli sahihi zaidi, kama alivyofanya hivyo Omari radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na imepokelewa kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake yakwamba

alisema: “Adhabu ya mchawi ni kuuawa kwa upanga” (na hii haifanywi kiholela na kila mtu, bali ni mahakama ikiwa zinahukumu kwa sheria ya Mwenyezi Mungu), na alipobaini Hafswa mama wa waumini radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa kuna mjakazi kamfanyia uchawi alimuuwa.”

**Swali Muhimu:** Je, inafaa kumchoma moto mchawi?

**Jawabu:** Hachomwi moto binadamu yeyote; kwa sababu Mtume rehema na amani ziwe juu yake kakataza hilo, na akasema: **“Hakika haadhibu kwa Moto isipokuwa Mwenyezi Mungu pekee, bali atauliwa kwa upanga”.**

## Kitenguzi cha Nane

Amesema Imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **“Kitenguzi cha Nane: Kuwahami washirikina na kuwasaidia dhidi ya Waislamu, na ushahidi wa hilo ni kauli yake Mtukufu:**

﴿ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُۥ مِنْهُمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٥١﴾ ﴾ [سورة المائدة: ٥١].

**“Na mwenye kuwafanya marafiki wandani miongoni mwenu, basi huyo hakika ni miongoni mwao.”** [Maaida: 51]

Amesema bin Baazi: “La wajibu kwa kila Muislamu ni kujitenga mbali na washirikina, na kujiweka mbali na dini yao, na kuikufuru, na kuwaweka karibu watu wa tauhidi

na kuwapenda na kuipenda dini yao, na huu ndio msingi mkuu. Hivyo ni wajibu kuwapenda Waumini, na kuipenda dini yao, na kuwaweka karibu kwa hilo..., na ni wajibu kuwawekea uadui Makafiri, na kuwachukia, na ni wajibu kujiweka mbali na dini yao na kuitakidi ubatili wake, amesema Mfukufu:

﴿فَمَن يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِن بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ لَهَا ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٥٦﴾﴾ [سورة البقرة:٢٥٦].

**“Kwa hivyo, anayemkufuru Taaghuut (Kila anaye abudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu na akaridhia) na akamwamini Mwenyezi Mungu, basi bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisichovunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia mno, Mwenye kujua vyema.”** [Al-baqara: 256]. Ni lazima kukufuru Taaghuut, na kumuamini Mwenyezi Mungu, kwani katika vitenguzi vya Uislamu ni: Kuwahami washirikina na kuwasaidia dhidi ya Waislamu, hiki ni kitenguzi miongoni mwa vitenguzi vya Uislamu na ni kuritadi na kutoka katika Uislamu, na hivyo hivyo kuupenda ukafiri na kuuridhia ni ukafiri unaojitegemea hata kama Muislamu hatoufanya”.

**Nasema:** Kuamiliana na wasiokuwa Waislamu ni jambo ambalo halijakatazwa katika Sheria, kwa sababu hilo halimaanishi mapenzi wala kuwanusuru katika batili yao.

Anasema bin Baazi: “Ama jambo la tatu, nalo ni kusaidizana katika mambo ya kidunia wakati wa haja, kama alivyofanya Mtume rehema na amani ziwe juu yake pamoja na Mayahudi huko Khaibari, au kutaka msaada kwake dhidi ya kafiri anayehofiwa shari yake; ili azuie shari za kafiri mwingine kama alivyofanya Mtume rehema na amani ziwe juu yake kwa Mutwi’m bin Adiy na pamoja na wengine ili kuzuia shari za makafiri madhalimu, na kama alivyomtaka msaada Abuu Twalibi kumzuia dhidi ya makafiri, na kama alivyotaka msaada Abubakari Swiddiki kwa bin Daghana kafiri dhidi ya makafiri si kwa sababu ya kuipenda dini yake lakini ni kwa sababu ya kuwapiga vita makafiri wengine: Hili haliingii katika mlango huu, bali hili linafaa, na kama alivyotaka msaada Mtume rehema na amani ziwe juu yake kwa Abdallah bin Uraikiti wa kumuelekeza njia ya Madina.”

Na akasema pia: “Na ama makafiri wanaoupiga vita Uislamu haifai kuwasaidia kwa chochote, bali kuwasaidia dhidi ya Waislamu ni katika vitenguzi vya Uislamu kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُۥ مِنْهُمْ ﴾ [سورة المائدة: ٥١].

**“Na mwenye kuwafanya marafiki wandani miongoni mwenu, basi huyo hakika ni miongoni mwao.”** [Maaida: 51]

Kisha akasema: "...Na ama katika hali ya maelewano na utulivu na amani hakuna tatizo kuwasaidia na kuwatendea wema katika yale wanayoyahitaji, kama masikini wao au kiongozi wao, na mfano wake, na kuunga udugu na ukoo, kama alivyosema Mtukufu:

﴿لَّا يَنْهَىٰكُمُ ٱللَّهُ عَنِ ٱلَّذِينَ لَمْ يُقَٰتِلُوكُمْ فِى ٱلدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُم مِّن دِيَٰرِكُمْ أَن تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوٓا۟ إِلَيْهِمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُقْسِطِينَ ﴿٨﴾﴾ [سورة الممتحنة:٨].

**"Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu."** [Mumtahana: 8] kisha Sheikh akasema:

"Na wema na ihisani hii wakati wa utulivu na wakati wa maelewano unaweza kuwa njia ya kuongoka, na unaweza kuwa sababu ya kusilimu aliyepewa na aliyetendewa wema, na kuingia kwake ndani ya dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu…."

**Maswala Muhimu:** Na akasema kuhusu kafiri: "Na hakuna katazo lolote kisheria kumuuliza kuhusu wanawe, na kuhusu hali yake, hakuna ubaya katika hilo, na hakuna tatizo akila naye ikiwa kuna haja ya kufanya hivyo, na hakuna tatizo akiitika wito wake, kama alivyoitika Mtume

rehema na amani ziwe juu yake wito wa Mayahudi na akala chakula chao, ikiwa ataona kuna masilahi ya kisheria katika hilo".

## Je, kafiri apendwe endapo atawapenda Waislamu?

Amesema bin Baazi: "Na lau tukichukulia kuwa Wakristo wakiwapenda Waislamu na wakaonyesha mapenzi yao kwao, haitofaa kwa Waumini kuwapenda na kuwafanya wandani wao; kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu kawakataza hilo katika Aya zilizotangulia".

Na akasema: "Na haitoondoka chuki ya Makafiri juu ya Waislamu, ila pale watakapoacha dini yao na wakafuata mila ya maadui zao, na wakajiunga katika kundi lao, na huo ndio upotofu wa mbali na ukafiri wa wazi, na ndio sababu ya adhabu na mateso duniani na Akhera".

## Kitenguzi cha Tisa

Amesema Imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **"Kitenguzi cha Tisa: Atakaye itakidi kuwa kuna baadhi ya watu si wajibu kwao kumfuata Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na kwamba wana uhuru wa kutoka nje ya sheria ya Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, kama**

**alivyopata nafasi Khadhiri ya kutoka nje ya sheria ya Mussa amani iwe juu yake, basi huyo ni kafiri".**

Amesema bin Baazi: "Atakayeitakidi kuwa ana uhuru kwake wa kutoka katika sheria ya Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, kama ilivyomuwezekania Khadhiri kutoka katika sheria ya Mussa Msemeshwa wa Rahmaan -rehema na amani ziwe juu yake- basi huyo ni kafiri kwa makubaliano ya wanachuoni wote, atapewa nafasi ya kutubia na atabainishiwa ushahidi, na akikataa basi atauawa" (na hiyo ni kazi ya mahakama na si kikundi au mtu binafsi).

Na akasema: "Na atakayedai kuwa fulani katika watu amejitosheleza hahitaji kumfuata Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, na akadai kuwa inamjia elimu kutoka kwa Mwenyezi Mungu mubashara, na baadhi yao husema: Umenihadithia moyo wangu kutoka kwa Mola wangu, atakayedai hivi na akasema kuwa: Kuna uwezekano kwake wa kutoihitaji sheria ya Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, au kuwa na elimu yake maalum kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu isiyopitia njia ya Manabii, bali kwa njia ya fikira zake na yale yanayokuja ndani ya moyo wake katika fikira, na yale anayodai kuwa anayapokea moja kwa moja kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atakuwa katokomea mbali na kapotea njia iliyo sawa, na atakuwa katoka katika duara la Uislamu, na kaingia katika duara la ukafiri, -tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu na hilo-; kwa

sababu inawalazimu watu wote kufuata sheria ya Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake:

﴿ قُلْ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنِّى رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا ﴿١٥٨﴾ ﴾ [سورة الأعراف:١٥٨].

**"Sema; Enyi watu! Hakika mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwenu nyote"** [A'raaf: 158]

﴿ وَمَآ أَرْسَلْنَٰكَ إِلَّا كَآفَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا ﴿٢٨﴾ ﴾ [سورة سبأ:٢٨].

**"Na hatukukutuma ila kwa watu wote uwe mbashiri na muonyaji"** [Sabai: 28] Hivyo atakayedai kuwa inafaa kwake kutoka katika sheria ya Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, basi atakuwa kasema kauli kubwa na ameleta ukafiri wa wazi…"

## Kitenguzi cha Kumi

Amesema Imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **"Kitenguzi cha kumi: "Kuipuuza dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, hataki kuisoma wala kuifanyia kazi, na ushahidi ni kauli yake Mtukufu:**

﴿ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن ذُكِّرَ بِـَٔايَٰتِ رَبِّهِۦ ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَآ ۚ إِنَّا مِنَ ٱلْمُجْرِمِينَ مُنتَقِمُونَ ﴿٢٢﴾ ﴾ [سورة السجدة:٢٢].

**“Na ni nani dhalimu mkubwa zaidi kuliko yule aliyekumbushwa kwa aya za Mola wake Mlezi kisha akazipuuza, hakika sisi tutajilipiza kwa wakosefu”** [Sajd: 222].

Amesema bin Baazi: Mapungufu makubwa na mabaya zaidi leo hii ni katika utekelezaji, ama elimu ni nyepesi mno, mwanafunzi anaweza kurejea maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na maneno ya wanachuoni, na asiyejua kabisa kusoma pia anaweza kuuliza anapopenda kuijua heri… leo kimekuwa chepesi kila kitu…na anaweza kuwa na msomi katika mji wake na katika kijiji chake, anaweza kujifunza na kuuliza bila gharama yoyote, jambo la wajibu ni kutafuta elimu na kuwa na mwanga na kuifanyia kazi, anasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika Hadithi sahihi: **“Mwenye kumtakia Mwenyezi Mungu heri humpa ufahamu katika dini”** [Sahihi Bukhari na Muslim]. Huu ni ushahidi kuwa mwenye kumtakia Mwenyezi Mungu heri hupata ufahamu na hujifunza na hupata mwanga ili aifanyie kazi, na ambaye hatomtakia heri hupuuza na kughafilika, na hii ni hatari kubwa, kughafilika na kupuuza ni katika alama zinazoonyesha kuwa mja, Mwenyezi Mungu hajamtakia heri…”.

Na akasema: “…Na aliwasifia Mwenyezi Mungu makafiri kwa kupuuza lengo waliloumbiwa na yale waliyoonywa, ikiwa ni onyo kwetu kuwa la wajibu kwa Muislamu

aielekee dini ya Mwenyezi Mungu na awe na utambuzi katika dini ya Mwenyezi Mungu na aulize kwa yale yanayomtatiza, na awe na mwangaza, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَٱلَّذِينَ كَفَرُواْ عَمَّآ أُنذِرُواْ مُعۡرِضُونَ ٣﴾ [سورة الأحقاف:٣].

**“Na wale waliokufuru wanayapuuza yale waliyoonywa”** [Ahqaaf: 3]. Na amesema Mtukufu:

﴿وَمَنۡ أَظۡلَمُ مِمَّن ذُكِّرَ بِـَٔايَٰتِ رَبِّهِۦ فَأَعۡرَضَ عَنۡهَا وَنَسِيَ مَا قَدَّمَتۡ يَدَاهُۚ ٥٧﴾ [سورة الكهف:٥٧].

**“Na ni nani dhalimu mkubwa zaidi kuliko yule anayekumbushwa ishara za Mola wake Mlezi, naye akazipuuza na akasahau yale yaliyo tangulizwa na mikono yake...”** [Kahf: 57]. Katika mambo muhimu kwa muumini ni kutafuta elimu na kuwa na uelewa katika dini nakuwa na mwangaza, na kukipa kipaumbele kitabu cha Mwenyezi Mungu na kukielekea na kukizingatia na kufaidika nacho, na kuzipa kipaumbele Sunna za Mtume rehema na amani ziwe juu yake nakuwa na utambuzi nazo na kuzifanyia kazi...”

Na akasema Sheikh: “Ni lazima kwa wenye kuswali kutotoka anaposimama mtu kutoa mawaidha, na inahofiwa kwa mwenye kutoka na hakusikiliza mawaidha pasina dharura kuwa miongoni mwa wale aliosema Mtume rehema na amani ziwe juu yake juu yao: **“Mwenyezi Mungu akampuuza”**.

Na aliulizwa: Mwenye kushuhudia kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na akaitakidi hilo kwa moyo wake, je anakuwa bado Muislamu?

**Akajibu:** “Huyu habaki kuwa Muislamu, mpaka ampwekeshe Mwenyezi Mungu kwa matendo yake na ampwekeshe Mwenyezi Mungu kwa kumhofu na kumtarajia na kumpenda na kuswali, na aamini kuwa Mwenyezi Mungu amewajibisha kadhaa na ameharamisha kadhaa, na haiingii akilini mtu ni Muislamu anamwamini Mwenyezi Mungu kisha aache matendo yote, haya ni makadirio yasiyokuwa na msingi, haiwezekani kuingia akilini kwamba linaweza kutokea kwa mtu yeyote; kwa sababu imani ya kweli humchochea kufanya mambo ya heri”.

## Vizuizi vya kumkufurisha mtu Maalum

Amesema Imamu Muhammadi bin Abdil-Wahhab Mwenyezi Mungu amrehemu: **"Na hakuna tofauti katika vitenguzi vyote hivi kati ya anayefanya kejeli, na anayefanya kwa kudhamiria na mwenye kuogopa, isipokuwa aliye lazimishwa".**

Amesema Bin Baazi: "Mwenye kulazimishwa ni yule aliyelazimishwa kwa kupigwa au kwa kutishiwa kuuawa toka kwa mtu ambaye anadhani kuwa anauwezo wa kumuuwa, akatoa talaka kwa sababu ya kulazimishwa, kwa kuchelea kumfika yale aliyotishiwa na kuhofishwa, huyu talaka yake haithibiti, kwa sababu kalazimishwa kwa talaka hiyo, kama ambavyo mwenye kulazimishwa kukufuru hakufuru kwa kutamka kwake ukafiri kwa sababu ya kulazimishwa kwake, kama alivyosema Aliyetakasika na kutukuka:

﴿ مَن كَفَرَ بِٱللَّهِ مِنۢ بَعۡدِ إِيمَٰنِهِۦٓ إِلَّا مَنۡ أُكۡرِهَ وَقَلۡبُهُۥ مُطۡمَئِنُّۢ بِٱلۡإِيمَٰنِ ﴿١٠٦﴾ ﴾

[سورة النحل:١٠٦].

**"Anayemkufuru Mwenyezi Mungu baada ya kuamini kwake, isipokuwa aliyelazimishwa na hali yakuwa moyo wake umetua juu ya imani"** [An-Nahli: 106]

Na akasema: "...anayeambiwa: Sema hivi au tukuuwe, au akapigwa kwa mijeledi mpaka akasema, akitamka basi huyu kalazimishwa, moyo wake utakapokuwa umetulizana katika imani... lakini katamka kwa ulimi ili ajikinge na kipigo au kifo".

**Maswala Muhimu:** Amesema Bin Baazi: Mwenye kulazimishwa ana sharti mbili:

1- Kulazimishwa, nako nikuwa kwake hawezi kujinasua.
2- Na kutulizana katika imani.

Atakapolazimishwa na moyo wake umetulizana katika imani hakuna ubaya kwake, na madhambi yatakuwa juu ya aliyemlazimisha, na ama neno likitoka pasina kulazimishwa au likatoka kwa kulazimishwa, lakini hana shaka na katulizana kwalo, atabeba madhambi ya hilo".

Na akasema: "Hasira kwa wanachuoni ina daraja tatu:

**Daraja la kwanza:** Ni hasira zake kuwa kali mpaka akapoteza akili yake, mpaka akawa hakubakiwa na kujitambua kwa sababu ya hasira kali.

Huyu hukumu yake ni sawa na hukumu wendawazimu na mazezeta, na maneno yake hayatokuwa na hukumu yoyote, si talaka yake wala kutukana kwake, wala kinginecho,

anakuwa ni sawa na wendawazimu, wala hakuna hukumu yoyote kwake.

**Daraja la pili:** Iliyo chini ya hiyo, ni hasira yake kuwa kali, na ikamuelemea mpaka ikabadili fikira zake, na mpaka akashindwa kujidhibiti, na ikamtawala kikamilifu mpaka akawa kama aliyelazimishwa, na aliyesukumwa ambaye hawezi kujinasua na kile kilichomfika, lakini yuko chini ya huyo wa kwanza, hisia zake hazikuondoka zote, lakini bado yuko pamoja na hasira kali kwa sababu ya kutukanana na ugomvi na mvutano kati yake na baadhi ya watu, kama familia yake na mke wake, au wanawe au kiongozi wake, au wengineo.

Wako wanachuoni waliosema: Huyu anaunganishwa na yule wa kwanza aliyepoteza akili yake; kwakuwa yuko karibu naye, na ni kwa sababu mtu mfano wake anakuwa kasukumwa na kalazimishwa kutamka, na hawezi kujinasua na hilo; kwa sababu ya hasira kali, na kauli hii ndio kauli yenye uwazi zaidi, na kwamba hukumu yake ni sawa na hukumu ya aliyepoteza akili yake katika maana kama hii…

**Daraja la tatu:** Hasira ya kawaida ambayo akili yake haiondoki, na wala anakuwa hana ukali unaomkaba kiasi cha kupoteza udhibiti wa nafsi yake, bali yuko chini ya huyo, ni hasira tu ya kawaida, anavurugwa na anakasirika, lakini anabaki na akili timamu, na maamuzi yake ya sawa,

huyu kwa wanachuoni maamuzi yake yanachukuliwa, na kunakubalika kuuza kwake na kununua kwake na talaka yake na mengineyo, kwa sababu hasira yake ni hafifu haibadilishi maamuzi yake wala moyo wake. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi”.

## Je anapewa udhuru aliyefanya jambo la kufuru kwa sababu ya ajira?

**Maswala Muhimu:** Na akasema: Na iliyo sahihi zaidi ni kauli ya jopo la wanachuoni kuwa kulazimishwa kuna kuwa kwa kitendo na kuna kuwa kwa kauli… na atakapolazimishwa kwa kupigwa au kitu mfano wake miongoni mwa vile ambavyo vinaweza kumdhuru madhara ya wazi basi anatakiwa amche Mwenyezi Mungu katika hilo na apupie usalama wake na sababu zake kwa namna yoyote iwezekanayo, na ama tu kwa malengo ya dunia na tamaa na kuwa na mali nyingi, au kwa sababu ya cheo cha uongozi, au kwa sababu ya ajira, haya yote ni uovu na wala si udhuru, tunamuomba Mwenyezi Mungu atulinde na hayo”.

## Je ujinga ni udhuru kwa kila mtu?

Alijibu Sheikh: Katika mambo makubwa, bali hili ni kubwa zaidi, na asili katika hili nikuwa hapewi udhuru yeyote anayeishi na Waislamu, mwenye kufikiwa na Qur'ani na Sunna hapewi udhuru, amesema Mtukufu:

﴿ هَٰذَا بَلَٰغٌ لِّلنَّاسِ ﴿٥٢﴾ ﴾ [سورة إبراهيم:٥٢]. وقال تعالى: ﴿وَأُوحِيَ إِلَيَّ هَٰذَا ٱلْقُرْءَانُ لِأُنذِرَكُم بِهِۦ وَمَنۢ بَلَغَ ﴿١٩﴾ ﴾ [سورة الأنعام:١٩].

**"Hili ni tangazo liwafikie watu"** [Ibrahim: 52] Na akasema Mtukufu: **"Na nimefunuliwa kwangu Qur'ani hii ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayemfikia"** [An-Aam: 19] Itakayemfikia Qur'ani na Sunna huyo hana udhuru, bali amefikwa na ujinga kwa sababu ya kupuuza kwake na kutojali kwake"

**Na aliulizwa Sheikh:** Je, ni upi mtazamo wenu, kwa mtu asiyejua tauhidi, hapewi udhuru kwa ujinga?

**Akajibu:** Hapana, hapewi udhuru, atakapopewa elimu hapewi udhuru, au akawa anaishi na Waislamu, ama ikiwa anaishi mbali hukumu yake ni kama hukumu ya watu walioshi bila kufikiwa na ujumbe wowote (Ahlulfitra) tutaamiliana naye kama kafiri, lakini swala lake linabakia kwa Mwenyezi Mungu, akifa haswaliwi, na wala Waislamu

hawatomrithi, na swala lake litabakia kwa Mwenyezi Mungu”.

## Ni mambo yapi ambayo husimama hoja kwa mtu?

**Na miongoni mwa mambo ambayo hoja inasimama kwa mtu:** Ni kuisikia Tauhidi (ujumbe wa kumpwekesha Mwenyezi Mungu).

Amesema Bin Baazi: Mnasemaje kuhusu mama yake na Mtume rehema na amani ziwe juu yake, je alikuwa na maarifa ya dini?, je aliupata Uislamu au alizipata zama za utume? Aliishi zama za ujinga na hakupewa udhuru wa ujinga, kwa sababu aliishi katika mabaki ya mila ya Nabii Ibrahim, na hivyo watu wowote, kama waarabu walioishi katika mabaki ya dini ya Nabii Ibrahim wakaipoteza hawapewi udhuru, walihukumiwa kwa ukafiri na ujinga na upotovu, na hakupewa idhini Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kumuombea msamaha mama yake, na aliwahi kusema kumwambia mtu aliyemuuliza kuhusu baba yake: **“Bila shaka baba yangu na baba yako wako motoni”** na baba yake alikufa katika zama za ujinga, vipi kwa hawa walioishi katika Uislamu na katikati ya Waislamu!?”

**Na miongoni mwa mambo ambayo hoja inasimama kwa mtu:** Ni kuwepo kwa wasomi na vyuo vya dini.

**Na miongoni mwa mambo ambayo hoja inasimama kwa mtu:** Ni vyombo vya habari kama redio, na kanda, na simu ni katika vitu ambavyo inasimama hoja kwa mtu".

## Kizuizi cha kukosea

Amesema Bin Baazi: Anaweza kutamka Muislamu neno la kukufuru kwa kuzidiwa na furaha au hasira au mfano wake, hakufuru kwa hilo; kwa kutokukusudia, kama ilivyokuja katika kisa cha yule aliyesema: **"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ni Mola wako na Wewe ni mja wangu"** alikosea kwa sababu ya furaha kubwa". [13]

Ndugu msomaji, baada ya kupata faida na kuelewa kwa upana kabisa mambo yanayomtoa mtu katika Uislamu, sasa turejee kuutazama Uislamu wa Ushia kwa macho ya kielimu.

Na katika kitabu hiki tutajikita kuzungumzia Ushia hasa uliotapakaa katika nchi za Afrika Mashariki ili kufupisha maneno na msomaji ufaidike pasina kukuchosha.

[13] Rejea Ufafanuzi wa vitenguzi hivi katika kitabu: Subulus Salaami Sharhu Nawaaqidhil Islami cha Bin Baazi

Na Mwenyezi Mungu pekee ndiye ninayemuomba taufiki, ikhlas, na kukubaliwa katika kazi hii, kwani yeye ndiye msimamizi wa hayo na muweza juu yake.

# SEHEMU YA TATU

## Ushia ni nini?

Anasema Shahrustan [14]: Shia ni wale waliomtetea Ali radhi za Allah ziwe juu yake peke yake, na wakasema ustahiki wa uimamu wake na uhalifa wake kuwa ulithibiti kwa maandiko na wasia, ima wa wazi au wa siri, na wakaitakidi kuwa uimamu hautoki nje ya wanawe, na ukitoka basi ni kwa kudhulumiwa na mwingine, au ni kwa kuficha kwake uhalisia, na wakasema: Uimamu si swala la kimasilahi linaloweza kuegemezwa kwa watu wote wamsimike imamu, bali ni swala la msingi na ni nguzo ya dini, haitakiwi kwa Mitume kulisahau wala kulipuuza, wala kuliegemeza kwa watu na kuliacha".

Na akasema: Na Mashia wote wanakubaliana katika uwajibu wa kumteuwa imamu na kumtaja, na kuthibiti kwa kukingwa kwa lazima kwa Manabii na Maimamu dhidi ya madhambi makubwa na madogo, na uwajibu kuwapenda baadhi ya Maswahaba na kujitenga na baadhi

[14] Ni Muhammad Abdulkarim Shahrustani, ni katika wanachuoni wa elimu ya Falsafa, amefariki Mwaka: 548.H, sawa na 1153.G

yao, kwa kauli na vitendo na itikadi, isipokuwa katika hali ya unafiki wa kuficha unachoitakidi (Tuqya) ila badhi ya kundi la Zaidia wanapingana nao katika hilo” [15]

Anasema Prof. Abdallah Naasir Al-qifaari: “Ama Marafidhwa wa zama zetu hizi wanaoitwa Mashia, hawa wamekusanya kati ya daraja mbili ya kwanza na ya pili, kumfanya Ali radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kuwa Mungu, hata wakafikia kusema kuwa yeye ndiye wa mwanzo na wa mwisho, na wa dhahiri na wa ndani, na kuwa yeye pamoja na maimamu wengine wanayajua mambo yaliyopita na yajayo na hakuna chochote kinachofichikana kwao, pamoja na daraja la pili nalo ni kukataa (Rafdhwu), nako ni kumuita kafiri Abubakari na Omari, mpaka wakafikia kusema kuwa Maswahaba wote waliritadi isipokuwa watatu na kwamba atakayeitakidi Uislamu wa Abubakari na Omari si Muislamu, na kwamba kila tamko (Shetani) lililokuja ndani ya Qur’ani anakusudiwa hapo ni Omari bin Khattwab radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, (na huu ni ukafiri wa wazi) kama tutakavokuja kubainisha baadaye”. [16]

Kisha Prof. Naasir; akaendelea kusema baada ya kuleta maelezo ya wanachuoni: “Ama Raafidhwa wa zama zetu kama Ithna-asheria wanaoitwa Mashia leo hii, hawa

[15 ] Rejea: Almilal Wannihal 2/146
[16] Maqaalaatul-Firaq 104

wamechupa mipaka zaidi katika daraja zote...hawa hawamtangulizi Ali mbele ya Abubakari na Omari pekee, bali wanamtanguliza mbele ya Mitume na Manabii wote, na wao hawamtukani Abubakari na Omari pekee, bali wanawaita makafiri, na wanamuita kafiri mwenye kuwatakia rehema, na hawaamini itikadi ya kurejea tu, bali wanaamini kutoweka na mwanzo (ni itikadi tutazifafanua hapo baadaye), na wanaitakidi kupotoshwa kwa Qur'ani, na kushushwa kwa vitabu vya Mungu juu ya Maimamu wao, kama ambavyo huwafundisha ushirikina wafuasi wao na kuufanya kuwa ni dini, na wanahalalisha umwagaji wa damu kwa kila mpinzani wao, kama tutakavyoeleza hapo baadaye. Ama jina Shia likitajwa mahala popote leo hii moja kwa moja linamaanisha ni Ithna-asheria (ambao wamesambaa katika nchi za Afrika Mashariki -Tanzania, Kenya, na kwingineko) kama tutakavyoeleza. [17]

[17]Marejeo yaliyotangulia uk. 105

## Je, Ushia ulianza lini?

Mashia wa Ithna-asheria wana kauli mbili kuhusu hili:

**Kauli ya kwanza:** Nikuwa Ushia ulianza tangu zamani kabla ya utume wa Nabii Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake, bali ulianza pamoja na kuanza kwa binadamu, na walipewa jukumu la Ushia Mitume na Manabii wote, mpaka imekuja (katika kitabu cha Mashia cha) Alkaafi, yakuwa: "Uongozi wa Ali umeandikwa katika nyaraka zote za Manabii, na hatotuma Mwenyezi Mungu Nabii yeyote isipokuwa kwa Unabii wa Muhammadi rehema na amani ziwe juu yake na aali zake, na kwa wasia wa Ali amani iwe juu yake" Na wakasema katika tafsiri ya kauli yake Mtukufu:

﴿وَلَقَدْ عَهِدْنَآ إِلَىٰٓ ءَادَمَ مِن قَبْلُ فَنَسِىَ وَلَمْ نَجِدْ لَهُۥ عَزْمًا ﴿١١٥﴾﴾ [سورة طه: ١١٥].

**"Na hapo zamani tuliagana na Adam, lakini alisahau na wala hatukuona kwake azma kubwa"** [Twaha: 115]

Tuliagana naye kuhusu Muhammadi na maimamu walio baada yake, akaacha na wala hakuwa na azma kubwa, bali wameitwa Manabii wenye azma, kwa sababu walichukua agano kuhusu Muhammadi na wateule wake baada yake,

na (Imam Mahadi) na njia yake, na azma yao ikakusanyika katika hilo vile vile pamoja na kulikubali” [18]

Na imekuja katika kitabu chao kitegemewa: (Bihaar Al-Anwaar): Ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake (kama wanavyodai) alisema: “Ewe Ali hakutuma Mwenyezi Mungu Nabii isipokuwa alimuita kuja katika utawala wako, atake asitake” [19]

Na maneno haya kama alivyosema Sheikhul-Islam: “Yanafanana na maneno ya wendawazimu, kwa sababu; ni vipi itachukuliwa ahadi kwa wale waliokuwa kabla yetu Manabii na Umma zao ya kumtii Ali katika Uimamu wake!?, kwa sababu hao walikufa kabla ya Mwenyezi Mungu kumuumba Ali, sasa anawezaje kuwa kiongozi wao?!, linalowezekana ni yeye kuwa kiongozi kwa watu wa zama zake, ama uongozi kwa walioumbwa kabla yake, na watakaoumbwa baada yake, huu ni uongo wa mtu asiyejielewa anachozungumza, wala haoni haya kwa anayoyasema” [20]

**Kauli ya pili:** Nikuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake yeye ndiye aliyepandikiza mbegu za Ushia, na wakadai kuwa Ushia ulianza katika zama zake rehema na amani

[18] Rejea Usuulul Kaafi cha AlkulainiL 1/416
[19] Rejea: Al-Bihaar: 11/60
[20] Rejea: Al-Ma’alamuz Zulfaa uk. 303

ziwe juu yake, na kwamba kulikuwa na Maswahaba waliokuwa wakimfanyia Ushia (kumpendelea) Ali na wakimpenda zaidi katika zama zake rehema na amani ziwe juu yake.

Anasema Muhammadi bin Husein Al-kaashiful-Ghitwaa, mmoja kati ya marejeo yao: "Bila shaka mtu wa kwanza kupandikiza mbegu ya Ushia katika uga wa Uislamu ni yeye mwenyewe aliyekuja na sheria, yaani mbegu ya Ushia ilipandikizwa ndani ya mbegu ya Uislamu hatua kwa hatua, usawa kwa usawa, na aliendelea kudumu kuumwagilia mche wake na kuunywesha mpaka ukakua na ukachanua katika zama zake, kisha ukazaa matunda baada ya kifo chake" [21]

Na rai hii haina msingi wowote kutoka ndani ya Qur'ani wala Sunna, na haina mashiko yoyote ya kihistoria yaliyothibiti, bali ni rai inayokinzana na Uislamu na inapingana na uhalisia uliothibiti, kwani Uislamu ulikuja kuuweka pamoja Umma huu katika neno moja, na si kuufarakananisha nakuwa mapote na makundi makundi, na hapakuwa katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake na mwenye kujiita Sunni wala Shia, na Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na Kutukuka anasema:

---

[21] Rejea: Aslus-Shia: Uk.43

﴿ إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلۡإِسۡلَٰمُۗ ﴿١٩﴾ ﴾ [سورة آل عمران:١٩].

**"Hakika dini (ya Haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu"** [Al-Imran: 19] Si Ushia wala kinginecho, hata wao wanakiri kwa kauli yao iliyotangulia kuwa: "Mbegu ya Ushia ilipandikizwa ndani ya mbegu ya Uislamu hatua kwa hatua..." Yaani: Ushia sio Uislamu (bali ulipandikizwa ndani ya Uislamu) na Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ وَمَن يَبۡتَغِ غَيۡرَ ٱلۡإِسۡلَٰمِ دِينٗا فَلَن يُقۡبَلَ مِنۡهُ ﴿٨٥﴾ ﴾ [سورة آل عمران:٨٥].

**"Na anayetafuta Dini isiyokuwa Uislamu haitakubaliwa kwake"** [Al-Imran: 85].

**Na ama kauli ya Wasiokuwa Mashia, na ndio kauli iliyochaguliwa zaidi:** Ni ile aliyoisema Imam Bin Hazmi na wengineo, kuwa Ushia (kuegemea kwa) Ali kulianza kwa kuuawa Othman radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake (mwaka 35.H), anasema Bin Hazmi: "Kisha akatawala Othman radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na akakaa katika utawala miaka kumi na mbili (12), na kwa kifo chake zikatokea hitilafu, na likaanza swala la Maraafidhwa (Mashia)" [22] Na hii ndio kauli iliyo karibu zaidi na usahihi kuliko kauli zote kuhusu kuanza kwa Ushia.

[22] Rejea: Alfaslu: 2/7

## Je, neno Shia lililokuja ndani ya Qur'ani linamaanisha Ushia?

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ وَإِنَّ مِن شِيعَتِهِۦ لَإِبۡرَٰهِيمَ ٨٣ ﴾ [سورة الصافات:٨٣].

**"Na hakika Ibrahim alikuwa katika kundi lake"** [Swaafaat: 83].

Ili kuwapotosha watu, Mashia huitumia Aya hii kuthibitisha kuwa Ushia umetajwa ndani ya Qur'ani!.

Huu ni upotoshaji wa wazi kwani hakuna Swahaba yeyote aliwahi kusema maana kama hiyo, na ili kupata tafsiri sahihi ya Aya hii kwanza rejea Aya iliyo kabla yake kujua ni nani aliyekusudiwa, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ سَلَٰمٌ عَلَىٰ نُوحٖ فِي ٱلۡعَٰلَمِينَ ٧٩ ﴾ [سورة الصافات:٧٩].

**"Iwe salama kwa Nuhu ulimwenguni kote"** [Swaafaat: 79] Aya hii inamaanisha kuwa Ibrahim alikuwa katika kundi la Nuhu (Dini ya Nuhu).

Amesema Ali bin Abii Twalha, kutoka kwa bin Abbasi anasema kuhusu Aya hii, yaani: **"Ni katika watu wa dini**

**yake”** Na amesema Mujaahidi: “Alikuwa katika mfumo wake na njia yake”.[23]

**Je Dini ya Nuhu ni ipi?**

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿لَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِۦ فَقَالَ يَٰقَوْمِ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُۥٓ ﴿٥٩﴾﴾ [سورة الأعراف: ٥٩].

**“Tulimpeleka Nuhu kwa Kaumu yake, naye akasema: Enyi Kaumu yangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi Hamna Mungu ila Yeye...”** [Aaraaf: 59]. Aya hii inamaanisha kuwa Nabii Nuhu aliwaamrisha watu wake kumuelekezea Ibada zao na dua zao Mwenyezi Mungu peke yake, kwani wao hawana Mungu mwingine zaidi yake, na huu ndio Uislamu halisi.

Ama Mashia dua zao wakati wa matatizo humuelekezea Ali na si Mwenyezi Mungu Mtukufu, jambo linaloonyesha wazi kuwa dini yao si dini waliyokuwa nayo Manabii, kama ilivyokuja katika kauli yao Mashuhuri:

«نادِ عليًّا مُظهرَ العجائب * تجده عونًا لك في النوائب. كلُّ همٍّ وغمٍّ سينجلي * بولايتك يا علي يا علي يا علي»

[23] Rejea: Tafsiri Bin Kathiir 7/23

“Muombe Ali mwenye kudhihirisha maajabu * Basi utamkuta ni msaada kwako katika matatizo. Kila msongo na matatizo yataondoka * kwa utawala wako ewe Ali, ewe Ali, ewe Ali” [24] Na kwa maelezo haya unabainika ubatili wa uzushi wao wa kuihusisha Aya hii tukufu na Ushia.

## Je, Ushia ni dhehebu au ni Dini?

Katika mahali Mashia wanatumia kuwahadaa watu ni kipengele hiki.

Tunaposema Dini tunamaanisha: Mfumo kamili wa kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu, sawa sawa uwe sahihi au si sahihi.

Na tunaposema dhehebu kwa maana ya kisheria: Ni mtazamo anaoshikamana nao mmoja kati ya wanachuoni wakubwa katika jambo fulani, ambao huenda ukaenda kinyume na mtazamo wa mwanachuoni mwingine, katika mambo ambayo hayamtoi mtu katika Uislamu, kama je, swala ya Ijumaa ina Adhana moja au Adhana mbili? Na Je, swala ya Tarawehe ina rakaa kumi na moja au ishirini na moja? N.k

[24] Rejea: Kitabu chao: Al-Kaf’amii, Asswabaah: Mlango wa Al-Adiyatul Mujarraba.

Na hii ndio maana wanayoitumia kuwapotosha watu, ama wanachuoni wakisema dhehebu la Ushia; wanamaanisha kundi linalojinasibisha na Uislamu na si kwa maana ya dhehebu kama ilivyotangulia.

**Jawabu:** Ushia ni Dini inayojitegemea iliyo mbali na Uislamu (hata kama wao wanajinasibisha na Uislamu), miongoni mwa ushahidi wa hilo nikuwa mfumo wa ibada za Ushia si mfumo wa ibada alizozifundisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake, kwa sababu:

Uislamu ni kutamka shahada mbili (Ash-hadu An-laa ilaaha illa llaah, wa anna Muhammadan rasuulullah).

Lakini Ushia ni shahada tatu kwa kuongeza: Ash-hadu Anna Aliyya Waliyyullaah.

Uislamu sahihi ni kuthibitisha bila shaka yoyote kuwa Qur'ani hii haikubadilishwa wala kupotoshwa tangu zama za Mtume mpaka leo hii, bali Mwenyezi Mungu aliihifadhi kama alivyosema Mtukufu:

﴿ إِنَّا نَحۡنُ نَزَّلۡنَا ٱلذِّكۡرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ ٩ ﴾ [سورة الحجر:٩].

**"Hakika sisi ndio tulioteremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutakao ulinda"** [Hijri: 9].

Lakini Mashia hawakubaliani na Qur'ani hii, bali wanasema si sahihi, na ilipotoshwa, kama walivyolithibitisha hilo wanachuoni wao, na wakaandika vitabu kwa hilo, mfano kama kitabu:

فَصْلُ الخِطَابِ فِي إِثْبَاتِ تحرِيفِ كِتَابِ رَبِّ الأَرْبَابِ ((للطبرسي))

"Kukata utata katika kuthibitisha kupotoshwa kitabu cha Mola Mlezi wa Walimwengu" (Cha Attabarsiy).

Haya na mengine mengi kama tutakavyokuja kuona mbele ya kitabu hiki -In shaa Allah- ni miongoni mwa itikadi zinazoonyesha kuwa Ushia si dhehebu bali ni Dini kamili inayojitegemea.

## Je, Ushia ulipandikizwa na nani ndani ya Uislamu?

Anasema Prof. Naasir: Wamethibitisha wahakiki miongoni mwa wanachuoni yakuwa: Aliyepandikiza mbegu ya Ushia ni Myahudi akiitwa: Abdallah bin sabai, na habari za kutajwa kwake zimekuja kwa mtiririko mkubwa katika vitabu vya Sunna na vya Mashia kwa kiwango sawa, na yeye ndiye kiongozi mkuu wa kundi la Sabaiya, na alikuwa akiitakidi na kusema kuwa Ali ni Mungu -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-, kama ambavyo alikuwa akisema kuwa Ali atarudi kuwa hai, na akiwatukana Maswahaba,

na alikuwa akijionyesha kuwa ni Muislamu, na alisafiri kwa ajili ya kueneza fitina zake katika miji ya Hijazi (Saudia) Basera na Kuufa (Iraq) na akaingia Damascus (Syria) katika zama za Othman bin Affan radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, wenyeji wakamfukuza, akaondoka kuelekea Misri na huko ndiko aliko tangaza uzushi wake, na akaenda Kuufa (Iraq) hakuondoka mpaka akahakikisha amepandikiza mbegu za watu wanaolingania katika madhehebu yake, amesema Bin Hajari[25]: "Abdallah bin Sabai ni katika mazandiki (wanafiki) wabaya zaidi waliochupa mipaka, ni mpotofu aliyepoteza watu,..." [26] Na zimekuja kwa wingi habari za fitina yake na kujitenga kwake na harakati zake za makusudi, yeye na kundi lake, katika vitabu vinavyoelezea makundi na historia na vinginevyo, miongoni mwa vyanzo vya Kisunna na Kishia kwa pamoja.

## Ni kauli zipi hasa zilikuwa ndio msingi wa mwanzo wa Ushia?

Alizua mnafiki Yahudi bin Sabai kauli tatu, ndio zilizogeuka baadaye kuwa ndio msingi wa Ithna-asheria, na zikazaliwa kutoka katika kauli hizo itikadi nyingine nyingi, nazo ni:

---

[25] Ahmad bin Ali Al-Asqalaaniy, ni katika wanachuoni wakubwa wa Hadithi, na ndio mwandishi wa kitabu Fat-hul-Baariy, amefariki Cairo Misri, mwaka: 852.H=1449.G.

[26] Rejea: Maqaalaatul Firaq: Uk. 109.

1. Usia wa Uimamu kwa Ali radhi za Allah ziwe juu yake, na wao wanauelezea kuwa ulithibiti kwa kuali ya wazi, na ndio msingi wa Ushia kama wanavyoona hivyo Masheikh wa Kishia, na vimeeleza vitabu vya kauli za makundi yanayojinasibisha na Uislamu kuwa bin Sabai ndiye mtu wa kwanza kuwajibisha uimamu wa Ali radhi za Allah ziwe juu yake.

2. Kumtukana Abubakari, na Omari, na Othmani, na Maswahaba wengine wengi radhi za Allah ziwe juu yao.

3. Kauli ya kurejea kwa Ali kuwa hai, radhi za Allah ziwe juu yake, na kurejea kumekuwa ni msingi miongoni mwa misingi ya Shia Ithna-asheria. [[27]]

## Ni wapi Mashia wanapatikana hasa Afrika Mashariki?

1. **Shia Ithna-asheria, (Twelvers)** na huitwa pia Raafidhwa, wengi wao wana asili ya Asia ya kusini (Khoja) walioingia Afrika Mashariki tangu karne ya 19 kwa ajili ya biashara.

**Taasisi zao:** Wanajulikana kupitia Jumuiya zao (Jamaat) na Taasisi zao ni kama: **Bilal Muslim Mission.**

[[27]] Rejea: Al-Maqaalaatu wal-firaq, cha Sheikh wa Kishia Alqummi (uk.20)

**Vyombo vyao habari:** Al-Itrah (IBN TV), Mwangaza tv, ipo katika Ving'amuzi vya Startimes na Azam, ShiaLive TV, Al-Kawthar Tv, Al-Manar TV, Imam Husein TV, Thaqalayn TV, Sauti ya Qur'ani, inapatikana Dar es Salaam na maeneo jirani.

**Pia:** Taasisi ya machapisho ya Africa Federation, yenye Makao Makuu yake Dar es Salaam.

**Magazeti:** Kama; Sauti ya Bilal

**Tovuti:** Kama: Al-Islam.org

## Tahadhari dhidi ya kuwasikiliza Mashia

Watu wengi hawaoni kama kuna tatizo kuwafuata (Kuwafollow) na kuwasikiliza Mashia katika TV, au mitandao ya kijamii, au kwingineko, hii ni hatari sana kwani wanachuoni wakubwa wa zamani na wasasa wametahadharisha kuwasikiliza watu wapotofu, isipokuwa kwa mwenye upeo mkubwa wa elimu, anayewajua vizuri wao na upotofu wao, akasikiliza kwa lengo la kujibu upotofu wao.

Anasema Imamu Maliki Allah amrehemu: **"Usimpe nafasi mpotofu wa moyo, ya kumtegea sikio, kwani hujui ni kwa lipi atakunasa katika upotofu huo"** [28]

[28] Rejea: Al-Muntaqaa Sharhul-Muwattwa'a, cha Imam Baajiy

## Ni akina nani Raafidhwa?

Neno Raafidhwa: Maana yake ni kukataa.

Amesema Abul-Hasan Al-Ash'ariy: "Na bila shaka wameitwa kuwa ni Raafidhwa, kwa kuukataa kwao uongozi (Uimammu) wa Abubakari na Omari". [29] Na wamesema baadhi ya wanachuoni: "Wamepewa jina la Raafidhwa; kwa kuikataa kwao dini ya Uislamu" [30]

Anasema prof. Naasir A-Qifaariy: Jina hili linawakusanya Ithna-asheria na Ismailia kwa kiwango sawa, kabla hawaja gawanyika mwaka 148H, baada ya kifo cha Ja'fari Swadiq, na wamekubaliana kundi la wanachuoni kuwaita jina la Raafidhwa hawa Ithna-asheria, kama mwanachuoni Al-Ash'ariy katika kitabu chake cha Maqaalaati, na Bin Hazmi katika kitabu chake cha Al-Fasli. [31]

2. **Shia Ismaili:** Hawa wamegawanyika katika makundi mawili.

(a). **Nizari Ismaili (Agha Khan):** Hawa wanamtabua Aga Khan kama imamu wao aliye hai.

[29] Rejea: Maqaalaatul-Islaamiyyiin 1/89
[30] Rejea: Ar-Raddu alas-shi'a, cha Al-Iskuubiy (23)
[31] Rejea: Maqaalaatul-Firaq Uk.115

(b). **Musta'li Ismaili (Bohora):** Na wanajulikana zaidi kama Dawoodi Bohra, asili yao ni India na wana jishughulisha sana na biashara.

Na miongoni mwa makundi ya Ismaili:

(a). **Kadiyani (Ahmadiyya)**: Hawa wanajulikana kama Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya (Ahmadiyya Muslim Community), na waliingia Tanganyika mno mwaka 1930. Na kituo chao kikuu kipo mtaa wa Libibi, Magomeni, Jijini Dar es Salaam.

Na vyombo vyao vya habari ni kama, chaneli za TV (MTA-Muslim Television Ahmadiyya)

(b). **Wabahai:** Hawa waliingia Tanganyika mno miaka ya 1950, na mpaka sasa wana mabaraza ya Kiroho (Local Spiritual Assemblies) katika mikoa mbalimbali, kama Dar es Salaam, Mwanza, Iringa, Arusha, na Dodoma. Na miongoni mwa miradi yao, ni shule ya Sekondari ya Ruaha, iliyopo Iringa.

Na Mashia hawa wanapatikana hasa katika miji ya: Zanzibar, Dar es Salaam, Arusha, Moshi, Mwanza, Singida, Kigoma, na kwingineko nchini Tanzania.

Na Nairobi na Mombasa nchini Kenya, na Kampala nchini Uganda, na kwingineko.

## Shia Ithna-asheria ni akina nani?

Neno Ithna-ashara humaanisha kumi na mbili (12)

Anasema prof. Naasir Al-Qifaariy: Wameitwa Ithna-asheria; kwa madai yao kuwa uimamu hautoki nje ya Maimamu kumi na mbili, na hairuhusiwi kwa yeyote asiyekuwa wao kuwaongoza Waislamu, na maimamu hao ni: 1. Ali bin Abii Twalib wanayemuita wao Murtadhwaa (Amefariki mwaka 40.H), 2. Al-Hasan bin Ali, wanayemuita Zaki (Amefariki mwaka 50.H) 3. Na Al-Husein bin Ali, wanayemuita Shahidi (Amefariki mwaka 61.H) 4. Ali binil-Husein, wanayemuita Zeinul-Aabidiin (Amefariki mwaka 95.H) 5. Muhammadi bin Ali, wanayemuita Al-Baaqir (Amefariki mwaka 114.H) 6. Na Ja'fari bin Muhammadi, wanayemuita As Swaadiq (Amefariki mwaka 148.H) 7. Na Musa bin Ja'fari, wanayemuita Al-Kaadhwim, (Amefariki mwaka 183.H) 8. Na Ali bin Musa, wanayemuita Ar-Ridhwaa (Amefariki mwaka 203.H) 9. Na Muhammadi bin Ali, wanayemuita Al-Jawwaad (Amefariki mwaka 220.H) 10. Na Ali bin Muhammadi, wanayemuita Al-Haadi (Amefariki mwaka 254.H) 11. Na Al-Hasan bin Ali Al-Askari (Amefariki mwaka 260.H) 12. Na Muhammadi bin Hasan Al-Askari, wanayemuita Mahdi, na huyu kiuhalisia hakuwahi kuwepo,

wala hakuna uwepo wake isipokuwa ni simulizi zao za uongo. [32]

## Je, ni kweli Maimamu hawa walikuwa Mashia?

Ameeleza Mwandishi wa kitabu: Diraasatun-anil-firaq: Hawa wote (Yaani maimamu 12) ni katika Ahlus sunna wal-jamaa'a (ni watu wanaofuata Qur'ani na mafundisho ya Mtume pasina kupinga chochote), na wa mwanzo wao ni Imamu Ali bin Abii Twalib radhi za Allah ziwe juu yake, Halifa muongofu, na wa nne katika Mahalifa waliobashiriwa kuingia Peponi, na Ali ajitenga mbali na fikira za Kishia na Kiraafidhwa walizomnasibishia kuhusu uimamu, kwani aliwahi kutangaza wazi kuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake hakumuachia Wasia wowote katika hilo, wala katika kumfanya kuwa yeye ni bora kuliko Abubakari na Omari, kwani alisimama siku moja akawahutubia watu na akasema kuwa: Mtu yeye atakayemfanya kuwa bora kuliko Abubakari na Omri basi atampa adhabu (Haddi) ya mzushi, na mengine mengi miongoni mwa yale yaliyothibiti kuhusu cheo chake na fadhila zake.

Na ama Hasan radhi za Allah ziwe juu yake, uhalifa wake ni miongoni mwa uhalifa wa mahalifa wanne waongofu, na aliwahi kumsifia Mtume rehema na amani ziwe juu yake

[32] Rejea: Maqaalaatul-Firaq: 119

kuwa ni bosi wa vijana wa Peponi, na kwamba Mwenyezi Mungu atasuluhisha kupitia yeye baina ya makundi mawili makubwa katika makundi ya Waislamu -lakini Mashia suluhu hiyo iliwachukiza- wakasema kumwambia: Wewe ndiye uliyezitia giza nyuso za Waumini, kama lilivyoelezwa hilo katika kitabu cha Al-Bidaaya cha bin Kathiir.

Ama waliobakia miongoni mwa wale waliowafanya kuwa maimamu wao mpaka kufikia wa kumi na mbili aliyejificha ndani ya pango la chini ya Ardhi (Sirdaab) ambaye wala Mwenyezi Mungu hakumuumba, hakuna aliyewahi kuwa kiongozi wa Waislamu miongoni mwao, lakini hao wote ni watu wa nyumba ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake na ni lazima kuwapenda.

Na wamewatumia vibaya Mashia watu wa nyumba ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake (Ahlul-Baiti) kwa madai ya kuwapenda na kuwatetea, kwa sababu wameyafanya madai haya kuwa ni pazia la kubomoa misingi ya dini hii. [33]

---

[33] Rejea: Maktabatu Shaamila, kitabu: Ardh wa Naqd diraasatun naqdiyya wa taujiihiyya likitaabi diraasatun ani-l-firaq (Uk. 492-493)

## Kwa nini Ushia na Iran?, na kwa nini Ali tu na si Maswahaba wengine?

Anasema Prof. Naasir Al-Qifaari: Wamesema wanachuoni wengine kuwa: Ushia unarudi asili yake katika misingi ya Uajemi (Iran) na hilo ni kwa ushahidi mwingi sana, miongoni mwake nikuwa:

**Ushahidi wa kwanza:** Wairan walikuwa na ufalme mpana, na walikuwa na nguvu kubwa kwa mataifa yote, na walikuwa wakijiona wao kuwa ni watukufu, kiasi kwamba walikuwa wakijiita kuwa wao ni watu huru na ni mabwana (mabosi), na walikuwa wakiwachukulia watu wengine kuwa ni watumwa wao, walipopewa mtihani wa kudondoka kwa dola yao kupitia mikono ya Waarabu, na Waarabu kwa wakati huo walikuwa hawana hatari yoyote kwa wairani, hilo liliwapa wakati mgumu sana, na tatizo likawa kubwa sana kwao, hivyo wakakusudia kuufanyia vitimbi Uislamu kwa kuupiga vita, kwa nyakati tofauti tofauti, na kwa nyakati zote hizo Mwenyezi Mungu aliidhihirisha haki. Basi wakaona kuupiga vita kwa hila na mbinu ndilo jambo linaloweza kufanikiwa, basi wakajionyesha watu miongoni mwao kuwa ni Waislamu, na wakajisogeza karibu zaidi kwa kujifanya watetezi, kwa kudhihirisha mapenzi kwa watu wa nyumba ya Mtume, na wakaonyesha kuwa Ali kadhulumiwa dhuluma mbaya -kwa madai yao- kisha

wakawapitisha watu katika mfumo huo mpaka wakawatoa katika njia ya uongofu. [34]

**Ushahidi wa pili:** Nikuwa Wairani wengi waliingia ndani ya Uislamu na hawakujivua na itikadi zao zote za zamani walizozirithi vizazi baada ya vizazi, kadiri nyakati zilivozidi kwenda basi walizichanganya rai zao za zamani na mchanganyiko wa Uislamu, anasema Sheikh Muhammadi Abuu Zuhra: “Hakika sisi tunaitakidi kuwa Mashia waliathirika na fikira za kiirani kuhusu ufalme na urithi, na hata mfanano kati ya madhehebu yao na mfumo wa ufalme wa Irani uko wazi, na kinacholithibitisha zaidi hilo nikuwa raia wengi wa Irani ni Mashia, na kwamba Mashia wa mwanzo kabisa walikuwa ni kutoka Irani” [35]

**Ushahidi wa tatu:** Kipindi Waislamu walipoifungua miji ya Uajemi (Iran) alipewa zawadi Husein bin Ali radhi za Allah ziwe juu yake, ya binti wa Yazdajirudu (Yazdegerd) mmoja kati ya wafalme wa Irani kwa wakati huo, baada ya kuja pamoja na mateka, basi akamzalia Ali bin Husein, na Wairani walishuhudia miongoni mwa watoto wa binti huyu (Muirani) aliyezaa na Husein wakiwarithi Wafalme wao wa zamani, na wakaona kuwa damu inayotembea kutoka katika kizazi cha Ali bin Husein na katika kizazi

[34] Rejea: Al-Faslu 2/273

[35] Rejea: Taariikhul-Madhaahibil Islaamiyya, cha Muhammad Abuu Zuhra (1/38)

chake kuwa ni damu ya Kiirani kutoka kwa mama yake binti wa Yazdajiridu ambaye ni katika ukoo wa Wafalme wa Wasasanidi, waliokuwa wakitukuzwa kwao.[36]

**Ushahidi wa nne:** Kuwepo kwa riwaya nyingi kutoka kwa Mashia wa Ithna-asheria zinazotilia mkazo athari za Kiirani, miongoni mwazo ni kauli yao kuwa: “Hakika Salman (Swahaba mwenye asili ya Irani) ni mlango wa Mwenyezi Mungu katika Ardhi, atakayemtambua basi atakuwa muumini, na atakayemkataa, atakuwa ni kafiri”[37] Kama ambavyo yalisema baadhi ya makundi yao kuhusu Uungu wa Salman Al-Faarisiy (Muirani), na yalipatikana makundi haya katika zama za Abul-Hasan Al-Ash’ariy aliyefariki mwaka (330.H), na akaliashiria hilo katika Makala yake kwa kusema: “Na wametamka wazi baadhi ya wasemaji katika zama zetu kuwa Salamn Al-Faarisiy ni Mungu”[38]

**Ushahidi wa tano:** Kumtukuza kwao Abuu Lu’lua Muirani mmajusi (Kafiri muabudu moto) aliyemuuwa halifa mkubwa Omari bin Khattwab radhi za Allah ziwe juu yake, mpaka wakamuita jina la (Mlango wa Mashujaa wa dini), na wakaizingatia siku ya kumuuwa kwake Omari radhi za Allah ziwe juu yake, ni sikukuu miongoni mwa sikukuu zao, na alitaja sheikh wao mualjeria riwaya zao katika hilo,

[36] Rejea: Taariikhul-Ya’quubiy (2/247), na Swahiihul-Kaafiy (1/53)
[37] Rejea: Rijaalul-Kushiy (Uk. 15-19)
[38] Rejea: Maqaalaatul-Islaamiyyiin (1/80)

[39] na wamemjengea aliyemuuwa Omari Kuba (kijumba) huko Irani, wanakitukuza na kukizunguka (kutufu) pembezoni mwake.

**Ushahidi wa sita:** Wanazitukuza sikukuu za Wairani Wamajusi (makafiri waabudu moto) wanaitukuza siku ya Nairuuzi, kama wanavyofanya Majusi, na zimethibitisha hilo taarifa zao, kuwa siku ya Nairuuzi ni katika sikukuu za Wairani. [40]

## Je, itikadi za Ushia zilitokana na Uislamu?

Anasema prof. Naasir Al-qifaariy: Nikuwa Ushia umepandikizwa kutoka katika itikadi mbali mbali, za Kiyahudi, Kikristo, Kipagani, na Kimajusi (Waabudu moto), bila shaka alipanda katika msafara wa Ushia kila aliyetaka kuufanyia vitimbi Uislamu na Waislamu, na kila aliyefanya hila ya kuishi chini ya itikadi zake za zamani kwa jina la Uislamu, kama Yahudi, Mkristo, Majusi, na wengineo, zikaingia katika Ushia fikira nyingi miongoni mwa fikira za nje na za ndani, na kwa sababu hii alisema Sheikhul-Islam bin Taimiya kuwa; wanaojinasibisha na Ushia wamechukua kutoka katika madhehebu ya Irani, Roma, Wayunani (Wagiriki), Wakristo, na Wayahudi, na wengineo, mambo mengi

[39] Rejea: Al-Anwaar Annu'maaniyya (1/108)

[40] Rejea: Kitabu chao, Bihaarul-Anwaar (48/108)

waliyoyachanganya na Ushia, na anasema: Na hii ni kusadikisha yale aliyoyaeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na akaeleza baadhi ya hadithi, kuwa Umma huu utapita katika mfumo wa wale waliokuwa kabla yao". [[41]]

Anasema Mwandishi wa kitabu Mukhtaswarut Tuhfa, Yakuwa: "Madhehebu ya Ushia yanafanana kikamilifu na makundi ya Kiyahudi, na Kikristo, Kishirikina, na Kimajusi"[[42]]

## Ni akina nani Shia Ismaili?

Asili yao ni watu wanaomini kuwa maandiko yana maana ya siri na ya wazi (Baatwiniyya).

Mwenyezi Mungu alipoudhihirisha Uislamu na akakunjua mbawa zake katika Ardhi ya Irani, lilishauriana kundi la Majusi (makafiri waabudu moto) na Wamazdaki (makafiri walioshikilia itikadi za Kiajemi), na kundi katika Thanawiyya (wanomini kuwa kuna miungu wawili) na kundi katika wapagani wa wanafalsafa, na baadhi ya Mayahudi, kuwa ni mbinu gani wataitumia kuumaliza Uislamu na watakayoitumia kuisambaratisha nguvu ya Waislamu, wakakubaliana katika mkutano huo kuwa watengeneze madhehebu yatakayochukua misingi yake kutoka kwa Wana Falsafa, na misingi kutoka

[[41]] Rejea: Minhaajus-Sunna (4/148)
[[42]] Rejea: Mukhtaswarut Tuhfa (Uk.298)

katika makundi yote tuliyoyataja hapo juu, na wakaona kuwa njia itakayofanikiwa kutimiza malengo yao ni wao kujipendekeza kwa kujinasibisha katika kuwatetea Ahlul-bayt (watu wa nyumba ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake), na wamchague mtu mmoja atakayedai kuwa yeye ni katika watu wa nyumba ya Mtume (Ahlul-bayt), na kwamba ni wajibu kwa viumbe wote kumuunga mkono, na ni lazima kumtii kwani yeye ni Halifa wa Mtume, na kuwa yeye amekingwa na kukosea.

## Kwa nini wanaitwa Ismaili (Ismaailiyya)?

Ni kwa sababu wanadai kuwa wao wanajinasibisha kwa Ismail bin Ja'fari Asswadiq, na wamekubaliana wasomi wa maswala ya nasaba kuwa huyu Ismail alifariki katika kipindi cha uhai wa baba yake mwaka 145.Hijiria, na kuwa hakuacha mtoto, isipokuwa hawa Ismaili wanadai kuwa Ismail hakufa, na kwamba baba yake aliacha Wasia wa Uimamu wake.

Na wanaitwa pia kwa jina la: Assabaiyya (wasabaia) kwa sababu wanaamini kuwa mzunguko wa Uimamu unaishia kwa watu saba, na kwamba mwisho ni kwa huyo wa saba, na ndio makusudio ya Kiyama, na kwamba zama za mzunguko huo pia hazina mwisho.

Na madhehebu haya yamechukuliwa kutoka kwa wapagani makuhani waagua nyota. [43]

## SEHEMU YA NNE

### Kadiyani (Ahmadiyya) ni akina nani?

Hili ni kundi jipya lililoanzishwa katika nchi ya India, katika kipindi ambacho Waislamu walikusanyika kuwafukuza wakoloni wa kizungu, waliokuwa na hasira nao, na hapo ndipo walipoona wakoloni njia rahisi ya kuwasambaratisha Waislamu, na kuzima hasira zao ni kuzungumza na bwana mmoja aliyeitwa Ghulam Ahmad Al-Kadiani aliyekuwa akijinasibisha asili yake na familia ya Kiislamu, ili atangaze dini mpya inayokwenda kinyume na dini wanayoiamini Waislamu wote, na itakayotengua misingi ya Uislamu, na itakayopinga mambo yanayofahamika ndani ya dini kuwa hayana utata.

Akaanza kwa kudai kuwa Wahyi (Ufunuo) haujakatika, na kwamba yeye ni Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ametumwa kuja kutengua Jihadi na uwajibu wa kuwakubali Wakoloni wakizungu, na kwamba wao ni rehema iliyotoka

[43] Rejea: Al-Adiyaani wal-firaq, cha Abdul-qaadir Shaibatul-Hamdi (Uk.83-84)

kwa Mwenyezi Mungu aliyoituma katika Ardhi ya India. [44]

## Ni nani Ghulam Ahmad Al-Kadiani?

Anajitambulisha mwenyewe katika Uk.72 katika kitabu chake (Al-Istifaa) kilichochapishwa na Annusra huko Rabwa nchini Pakistani mwaka 1378.H, anasema: “Mimi naitwa: Ghulam Ahmad Mirza Ghulam Murtadhwa...” kisha anasema katika uk. Huo huo: “Na mimi nilimsikia baba yangu akisema kuwa baba zangu wanatokana na Jurthuma wamaghuli (Waturuki). Lakini Mwenyezi Mungu aliniteremshia Wahyi akanieleza kuwa wao walitokana na Waajeni (Wairani) na si hawa waturuki” na amezaliwa Ghulam Ahmad katika kijiji cha Kadiani moja kati ya vijiji vya Punjab huko India kati ya mwaka 1835.G, au 1839, au 1840 (kulingana na historia), na aliuanza ujana wake kwa kusoma Kifursi na akaingia kusoma kiarabu na kanuni zake (Nahwu, na Sarfu). Kama ambavyo alisoma kidogo elimu ya udaktari, isipokuwa alipata maradhi aliyodumu nayo tangu utotoni, ikiwemo aina ya wendawazimu, -kama zinavyoeleza duru za habari za Makadiyani- hivyo hakuweza kuendelea na masomo yake. [45]

---

[44] Marejeo hayo hayo (Uk.97)
[45] Marejeo yaliyopita (Uk.97)

## Kudai kwake Utume

Ghulam Ahmad alimteuwa mmoja kati ya wafuasi wake wapotofu kuwa imamu katika Msikiti wake huko Kadiani, akiitwa: Abdul-Karim, na Abdul-Karim huyu alikuwa ni moja kati ya mbawa zake, na mbawa yake ya pili alikuwa ni bwana mmoja akiitwa Hakim Nurudini, kama alivyolisema wazi hilo Ghulam mwenyewe. Na mwaka 1900.G, alitoa Hotuba siku ya Ijumaa Abdul-Karim na akatamka ndani ya Hotuba hiyo -na Ghulam akiwepo- kuwa Mirza Ghulam Ahmad ni Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni wajibu kumwamini. Na kwamba mwenye kuwaamini Manabii na asimwamini, basi huyo atakuwa anatofautisha kati ya Manabii, na atakuwa kaenda kinyume na kauli ya Mwenyezi Mungu kuhusu sifa ya Waumini:

﴿لَا نُفَرِّقُ بَيۡنَ أَحَدٖ مِّن رُّسُلِهِۦۚ ﴿٢٨٥﴾﴾ [سورة البقرة:٢٨٥].

**"Hatumtofautishi yeyote katika Mitume"** [Baqara: 285] Na hotuba hii ilizua mjadala na malumbano makubwa kati ya wafuasi wa Ghulam, waliokuwa wakiitakidi kuwa yeye kaja kuifufua dini, nakuwa yeye ndiye Mahdi aliyeahidiwa na ndiye Kristo aliyekuwa akisubiriwa. Walipompinga, alitoa hotuba ya pili siku ya Ijumaa na akamgeukia Ghulam na akasema: Hakika mimi ninaamini kuwa wewe ni Nabii na ni Mtume, ikiwa nakosea nirekebishe katika hilo, na

walipomaliza swala na Ghulam akataka kuondoka, Abdul-Karim alimshika Ghulam, basi Ghulam akasema: “Hilo ndio ninaloliamini na ndio ninalowaita watu kwalo” kisha akaondoka kuelekea nyumbani kwake, basi ukazuka mzozo mkubwa kati ya Abdul-Karim na baadhi ya watu, na zikanyanyuka sauti zao, basi Ghulam akatoka nyumbani kwake, akasema:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَرۡفَعُوٓاْ أَصۡوَٰتَكُمۡ فَوۡقَ صَوۡتِ ٱلنَّبِيِّ ﴿٢﴾ ﴾ [سورة الحجرات:٢].

**“Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu juu ya sauti ya Nabii”** [Hujraati: 2] [46]

## Madai yake kuwa yuko katika nafasi ya mwana wa Mungu, na katika nafasi ya Arshi

Anasema mwenyewe katika kitabu chake (Al-Istiftaa Uk.82): “Wewe kwangu ni sawa na mpweke wangu na mwana wa pekee, sasa umewadia wakati upate msaada, na utambulike kwa watu kuwa wewe kwangu uko katika nafasi ya Arshi, wewe kwangu ni sawa na mwanangu. Wewe kwangu uko katika nafasi ambayo viumbe hawaijui” [47]

[46] Marejeo yaliyotangulia (Uk.100-101)
[47] Marejeo yaliyotangulia (Uk.106)

## Itifaki ya Umma wa Muhammadi kuwa Muhammadi ndiye mwisho wa Mitume, nakuwa hakuna Nabii baada yake, nakuwa mwenye kulipinga hilo ni kafiri

Ghulam Ahmad anadai utume tena bila kujali Qur'ani na Sunna na itifaki ya Umma. Hivyo, katika misingi hii mitatu kuna hoja za wazi kuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake ndiye wa mwisho katika Manabii na Mitume.

Ama Qur'ani ni kauli yake Mtukufu:

﴿مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَآ أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ ٱللَّهِ وَخَاتَمَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ ۗ ﴿٤٠﴾﴾ [سورة الأحزاب: ٤٠].

**"Muhammadi si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Manabii"** [Ahzaab: 40]

Na katika Sunna:

عن أبي هريرة رضي الله عنه عن النبي ﷺ أنه قال: **((كَانَتْ بَنُو إِسْرَائِيلَ تَسُوسُهُمُ الأَنْبِيَاءُ، كُلَّمَا هَلَكَ نَبِيٌّ خَلَفَهُ نَبِيٌّ، وَأَنَّهُ لَا نَبِيَّ بَعْدِيْ))** [صحيح البخاري]

Imekuja kutoka kwa Abuu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake, kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake yakwamba amesema: **"Walikuwa wana wa Israeli**

**wakiongozwa na Manabii, kila anapokufa Nabii, anakuja baadala yake Nabii mwingine, na hakika hakuna Nabii baada yangu”** [Sahihi Bukhari].

Na kwa hilo yamefungamana makubaliano ya Waislamu wote, na yakawa katika nafasi ya jambo linalojulikana pasina mtu kuhitaji kusoma. [48]

## Kudai kwake kuwa Malaika ni viungo vya Mwenyezi Mungu

Anasema mwenyewe katika kitabu (Himaayatul-bashari Uk.98): “Na watazameni Malaika ni namna gani Mwenyezi Mungu aliwafanya kama mbawa zake”.[49] Maneno haya yanatosha kuonyesha kuwa huu ni ukafiri na si Uislamu.

# SEHEMU YA TANO

## Wabahai ni akina nani?

Ubahai: Ni njama za kukanusha uwepo wa Mungu, zinazokinzana na asili ya dini na misingi yake, na unakwenda kinyume na mila zote zilizotoka mbinguni, ulipangwa na Freemason, na Mayahudi wanaotaka kuitawala dunia, na

[48] Marejeo yaliyotangulia (Uk. 107)
[49] Marejeo yaliyotangulia (Uk. 110)

ulipandikizwa na ujasusi wa Urusi, kwa lengo la kuutumia katika malengo yake maalum ya kujitanua: Wakiwa na lengo la kuubadili Uislamu na kufuta itikadi zake, na kubatilisha sheria zake, na mfumo wake...ili wapate fursa ya kuanzisha nchi ya ujamaa kwa ajili ya Mayahudi katika Ardhi ya Palestina...[50]

## Ulitengenezwa vipi ubahai?

Mnamo mwaka (1810.G) huko Karbalaa nchini Iraq, alijitokeza mtu mmoja asiyefahamika asili yake wala kazaliwa na kukulia wapi, wanaeleza baadhi ya watu kuwa alikuwa ni Kasisi (wa kanisa). Na akadai kuwa jina lake ni (Kaadhim Rushtaa), na -Rushta ni kijiji miongoni mwa vijiji vya Irani- pamoja nakuwa watu wa Rushta hawajui chochote kuhusu habari yake.

Mtu huyu alisoma itikadi za Shia Ithna-asheria, na akadai kuwa yeye ni katika wanachuoni wake, na akatumia kutoka katika Ushia fikira ya Imamu Mahdi anayesubiriwa, na kupitia fikira hii ya Mahdi alitafuta mtu atakayempa jina hilo, ili kupitia mlango huu afanikishe malengo yake anayoyakusudia.

Hivyo alipata wanafunzi, na katika wanafunzi hao kinara wao alikuwa ni mtu mmoja aliyefahamika kwa jina la

[50] Marejeo yaliyotangulia (Uk. 129)

Husein Al-Bashruui, kutokea Bashruwiaa, moja kati ya vijiji vya Irani, na alifahamika Husein huyu kwa matendo machafu na njama, na ujanja, na kuwa kigeugeu, na ndio maana alikumbatiwa na njama hizi ovu…na ndiye aliyeteuliwa kutekeleza mipango hiyo na njama hizo ovu…” [51]

Na ulipandikizwa mti huu uliolaaniwa katika Ardhi ya Umma wa Kiislamu, na ulifanikiwa kwa hatari kubwa kukusanya kundi kubwa la watu katika kundi hili, kwani walimleta mtu mmoja akiitwa: “Husein Ali Al-Mazandarani mzaliwa wa Tehran mwaka 1817.G”, Na Jasusi huyu ndiye aliyekuja kudai uungu wake, baada ya hapo, na kujiita Wabahai, na akamtumia kwa kila alichokitaka.

Bali mwisho wa uhai wake Husein Ali Mazandarani alijiita Mungu, kama alivyoandika Ujumbe kwa mwanaye akisema: “Kutoka kwa Mungu mwenye nguvu na hekima, kwenda kwa Mungu mpole mwenye habari” [52]

[51] Marejeo yaliyotangulia (Uk. 130)
[52] Marejeo yaliyotangulia (Uk. 53)

## Ni zipi itikadi za Mashia (Raafidhwa)?

Kwanza kabla ya kufahamu itikadi za Mashia, ni vyema ufahamu kuwa tabia ya Mashia ni uongo, na kubwa zaidi ni kudhihirisha vitendo au kauli kinyume na wanavyoitakidi, lau utamuuliza Shia unasemaje kuhusu Swahaba Abubakari na Omari? Atawasifia na kukuonyesha kuwa hana itikadi mbaya dhidi yao, ilhali uhalisia ndani ya nafsi yake anaitakidi kuwa ni makafiri, na hii ndiyo Itikadi ya (Taqiyya).

## Itikadi yao katika Qur'ani

**Kauli yao kuwa: Qur'ani ilipotoshwa:** Walizua kauli hii watangulizi wa Mashia katika karne ya pili, na ilipofika karne ya kumi na tatu (Hijiria) alianza kukusanya mmoja kati ya Masheikh wakubwa wa Mashia, akiitwa Nuri Attwabarsiy uzushi huu katika kitabu alichokiita:

((فَصْلُ الخِطَابِ فِي إِثْبَاتِ تحرِيفِ كِتَابِ رَبِّ الأَرْبَابِ))

"Kukata utata katika kuthibitisha kupotoshwa kitabu cha Mola Mlezi wa Walimwengu"[53]

Na wanadai kuwa Qur'ani sahihi, iliyosalimika na kupotoshwa ipo kwa Ali radhi za Allah ziwe juu yake.

[53] Rejea: Maqaalaatul firaq cha Prof. Naasir A-qifaariy (Uk. 135)

Na itoshe kuonyesha uongo na ubatili wa hilo -kama alivyosema bin Hazmi kuwa: “Ali bin Abii Twalib radhi za Allah ziwe juu yake, ambaye kwa wengi wao ndio Mungu muumbaji, na kwa baadhi yao ni Nabii anayeendelea kuzungumza hadi leo hii, na kwa wengine ni imamu aliyekingwa na kukosea, aliyeshika utawala na akaumiliki, aliyekaa katika utawala miaka mitano na miazi tisa akiwa kiongozi anayesikilizwa, na wakati huo Qur’ani ilikuwa ikisomwa kila Msikiti na kila mahali, na hata yeye aliwasalisha watu kwa Qur’ani hii hii, na misahafu ikiwa pamoja naye na mingine ikiwa mkononi mwake, lau kama angeona kubadilishwa kokote kama wanavyosema Mashia je, angeweza kukubali hilo?! Kisha akaja mwanaye Hasan, ambaye kwao ni sawa na baba yake, naye akaishi na Qur’ani hii hii.

Hivi wanawezaje hawa wapumbavu kusema kuwa: Ndani ya msahafu kuna herufi iliyozidi au iliyopungua, au ilibadilishwa pamoja na haya yote?! Na kumpiga vita mtu aliyepotosha Qur’ani au kubadili Uislamu ndiyo lilikuwa ni jambo la lazima zaidi kuliko kuwapiga kwake vita wale waliompinga katika rai ndogo katika watu wa Sham, ambayo wao waliona hivyo na yeye akaona kinyume na wao tu, kufaulu kwa uongo wa Mashia kunahitaji ushahidi na hoja za wazi, Alhamdulillah”[54]

[54] Rejea: Al-Faslu, cha bin Hazmi (2/216-217)

## Madai yao kuwa Qur'ani si hoja ila kwa kunyooshwa

Walisema kauli yao hii kupitia ulimi wa Imamu wao katika upotofu wanayemuita jina la (muaminifu wa Uislamu) anayeitwa Al-Kulaini, na hayo ni katika kitabu chake (Usuulul-Kaafi) ambacho wanakichukulia kuwa ndio marejeo yasiyo na shaka, alisema kuwa: "...Qur'ani haiwezi kuwa hoja, isipokuwa kupitia mnyooshaji, nakwamba Ali ndiye aliyekuwa akiinyoosha Qur'ani". [55]

## Madai yao kuwa kauli ya imamu inaweza kufuta Qur'ani

Wanadai Mashia kuwa Maimamu wao wana haki ya kuifanya aya ya watu wote kuwa mahususi, na mahususi kuwa ya watu wote, na kufuta aya iliyo wazi.

Ameeleza Abuu Ja'fari An-nah-aas: "Na wanasema wengineo (katika Mashia): Mlango wa aya inayofuta na inayofutwa huu ni wa Imamu, anafuta akitakacho"[56] Na akalichukulia hilo ni ukafiri mkubwa, kisha akabainisha ubatili wake kwa kauli yake kuwa: "Kufuta hakukuwa kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake isipokuwa kwa Wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ima kwa

[55] Rejea: Usuulu-Kaafiy (1/188)
[56] Rejea: Wasaa ilush-Shia (18/149)

Qur'ani mfano wake, kulingana na kauli za baadhi ya wanachuoni, na ima kwa Wahyi usiokuwa Qur'ani, lilipoondoka hilo kwa kifo cha Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na kufuta kukaondoka" [57]

## Madai yao kuwa Qur'ani yote ilishuka kwa ajili yao na maadui zao

Wanaitakidi Mashia kuwa: "Qur'ani yote iliteremka kwao (kwa ajili ya Maimamu wao 12), na kwa mawalii wao, na maadui zao" Mpaka anadai mmoja kati ya Masheikh wao, Al-Bahriy kuwa Ali peke yake ametajwa ndani ya Qur'ani mara (1,154) [58]

Na kinachojulikana nikuwa Ali radhi za Allah ziwe juu yake, hakutajwa ndani ya Qur'ani kwa jina lake moja kwa moja, bali madai haya yamesimama katika tafsiri ya ndani kabisa ya kipagani. [59]

[57] Rejea: An-Naasikh Wal-Mansuukh (Uk.8-9)
[58] Rejea: Tafsirus Swafi (1/24)
[59] Rejea: Maqaalaatul-firaq (Uk.137)

## Itikadi yao ya kuteremshwa vitabu vya kiuungu kwa Maimamu wao

Walisema kuhusu kushuka kwa kitabu mfano wa Qur'ani, walichokiita (Msahafu wa Fatma), na kitabu kingine walichokiita (Lauhu Fatma) Yaani: Ubao wa Fatma, kisha wakadai kuteremka Nyaraka kumi na mbili kutoka mbinguni kuja kwa Maimamu wao, na mengineyo.[60]

## Itikadi yao katika hadithi za Mtume

### Itikadi yao kuwa kauli ya Imamu ni sawa na kauli ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake

Sunna kwao ni: Kila kinachotoka kwa aliyekingwa na kukosea, miongoni mwa kauli, au kitendo, au kukiri" kwa sababu Imamu kwao ni sawa na Nabii, anashushiwa Wahyi, na anafanya miujiza, na Uimamu ni muendelezo wa Unabii, bali ni daraja la juu kuliko Unabii, na kauli ya Imamu -kwa madai yao- ni kama kauli ya Mtume sawa sawa, bali ni kama kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, mpaka walisema: Inafaa kwa mwenye kusikia hadithi kutoka kwa Ja'fari Muhammadi Swadiq aseme: Amesema Mwenyezi Mungu

[60] Marejeo hayo hayo (Uk.139)

Mtukufu, wakaruhusu kumsemea uongo Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake. [61]

Na Maimamu kwa madai yao: "Kauli yao ni kauli ya Mwenyezi Mungu na amri yao ni amri ya Mwenyezi Mungu, na kuwatii ni kumtii Mwenyezi Mungu, na kuwaasi ni kumuasi Mwenyezi Mungu, na kwamba hawatamki ila nikutoka kwa Mwenyezi Mungu na kwa Wahyi wake"[62]

## Kauli yao kuwa Mtume alificha baadhi ya yale aliyoteremshiwa

Anasema marejeo wao wa sasa Muhammad Husein Al-Kaashiful-Ghitwaa: "Hakika hekima ya kushuka sheria kidodo kidogo ilipelekea kubainishwa idadi kadhaa ya hukumu na kufichwa zingine kadhaa, lakini yeye salamu za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake aliziweka kwa wausiwa wake,….."[63]

Na itikadi hii mbovu inamaanisha kumkashifu Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na kuwa alificha sehemu ya sheria na akapingana na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

[61] Marejeo yaliyotangulia Uk. Huo huo
[62] Rejea: Al-I'tiqaadaat (Uk.106)
[63] Rejea: Aslu Shia wa Usuuliha (Uk.77)

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلرَّسُولُ بَلِّغۡ مَآ أُنزِلَ إِلَيۡكَ مِن رَّبِّكَۖ وَإِن لَّمۡ تَفۡعَلۡ فَمَا بَلَّغۡتَ رِسَالَتَهُۥۚ ﴿٦٧﴾ ﴾ [سورة المائدة:٦٧].

**"Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake"** [Maaida: 67] Na kwamba dini haikukamilika, na kuwa Wahyi haujakatika.

## Kuzikataa kwao riwaya za Maswahaba

Anasema Sheikh wao Al-Kaashiful-Ghitwaa: "Hakika Shia hawaizingatii Sunna (anamaanisha Hadithi za Mtume) isipokuwa zile zilizothibiti kutoka kwa Ahli baiti…ama anazozipokea mfano kama Abuu Huraira na Samura na Jundub..na Amru bin Aaswi, na wengineo, basi habari hizo mbele ya Mashia hazina thamani hata ya mbu" [64]

## Itikadi yao kuhusu Imani na nguzo zake

Maana ya imani kwao: Ni kuwaamini maimamu kumi na mbili, na yeyote ambaye hatowaamini maimamu wao huyo si muumini kwao, na mafikio yake ni motoni, anasema Sheikh wao Muhammad Jawadi Al-Aamiliy: "Imani kwetu inatimia kwa kukiri uimamu wa maimamu kumi na mbili

[64] Marejeo yaliyotangulia (Uk.79

amani iwe juu yao"[65] na anasema Sheikh wao bin Mutwahar Al-Hulai: "Hakika swala la uimamu kwetu (maimamu 12) ni moja kati ya nguzo za imani ambazo mtu anastahiki kwayo kuishi Peponi milele, na kuepukana na ghadhabu za Rahmani (mwingi wa rehema)"[66]

Imani hii inathibitisha wazi kabisa kuwa Ushia ni dini inayojitegemea nje na Uislamu aliotuachia Mtume rehema na amani ziwe juu yake.

Na mtu wa mwanzo kuasisi itikadi hii potofu ni imamu wao Al-Kulaini, ambaye wanachukua kutoka kwake dini yao, na wanamuita kuwa ni Thiqatul-Islami (muaminifu wa Uislamu) [67]

## Shahada ya tatu:

Sote tunajua kuwa Uislamu sahihi una shahada mbili: Kushuhudia kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, nakuwa Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ila wao walizua shahada ya tatu, na ndio nembo ya imani hii mpya, nayo ni kauli yao: "Ninashuhudia kuwa Ali ni walii (kipenzi) cha Mwenyezi Mungu" huikariri kauli hii katika masikio yao na baada ya

[65] Marejeo yaliyotangulia (Uk. 79)
[66] Rejea Mifataahul-Karaama (2/80)
[67] Rejea: Maqaalaatul-Firaq (Uk. 141)

swala zao, na huwatamkisha maiti wao, imepokelewa kutoka kwa Abuu Baswiri kutoka kwa Abuu Ja'fari amesema: "Watamkisheni wanaokaribia kufa miongoni mwenu wakati wa kufa, shada yakuwa hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na uwalii (ukaribu wa Ali kwa Mwenyzi Mungu) na anatamkishwa shahada hii wakati wa kuingizwa kaburini, na wakati watu wanapo tawanyika na kumuacha...[68]

## Maana ya Tauhidi kwao

Tauhidi kwao ni kuwapwekesha maimamu kumi na mbili kwa uimamu, na ushirikina kwao ni mtu kujifanyia imamu au kiongozi asiyekuwa wao, na ndio maana aya zote za Qur'ani zilizokuja kuamrisha kumuabudu Mwenyezi Mungu peke yake, walibadilisha maana yake nakuwa ni kuamini uimamu wa Ali na maimamu wengine, na aya zilizokuja kukataza ushirikina walifanya makusudio yake kuwa ni katazo la kuwashirikisha wengine katika uimamu wa Ali. [69]

[68] Rejea: Maqaalaatul-Firaq (Uk. 141)
[69] Marejeo hayo hayo (Uk. 144)

## Kauli zao kuhusu kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada

Wanasema Ithna-asheria: Hakika maimamu kumi na mbili ndio wawakilishi baina ya Mwenyezi Mungu na waja wake. Amesema Al-majlisiy kuhusu maimamu wake: "Hao ni ngao ya Mola Mlezi, na ni wawakilishi baina yake na viumbe wake" na akaandika mlango kwa anwani: "Mlango wakuwa watu hawaongoki ila kupitia wao, na wao ndio wawakilishi baina ya viumbe na Mwenyezi Mungu, na kwamba hatoingia Peponi isipokuwa atakayewajua" Na huu ni ushirikina wa kuwashirikisha viumbe katika ibada ya Mwenyezi Mungu.

## Kauli yao kuwa kuhiji katika makumbusho ni bora kuliko kuhiji katika nyumba ya Mwenyezi Mungu

Imekuja katika kitabu Al-Kaafiy na vinginevyo katika vyanzo vyao kuwa: Hakika kulitembelea kaburi la Husein kunalingana na Hija ishirini, bali ni bora kuliko Umra ishirini na Hija zake" [70]

[70] Rejea: Furuu'ul-Kaafiy (1/324)

## Madai yao kuwa Karbalaa ni bora kuliko Kaa'ba

Wanasema: Bila shaka Karbalaa (Mahali alipouliwa Husein huko nchini Iraq) ni bora kuliko Al-Kaaba, na hakika Al-kaaba si kitu isipokuwa ni kimkia dhalili na kisicho na thamani kwa Ardhi ya Karbalaa. [71]

## Kauli zao kuhusu kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika Uumbaji na uendeshaji

Kauli yao kuwa: Hakika Mola Mlezi ni Imamu.

Na katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿قَالَ أَمَّا مَن ظَلَمَ فَسَوْفَ نُعَذِّبُهُۥ ثُمَّ يُرَدُّ إِلَىٰ رَبِّهِۦ فَيُعَذِّبُهُۥ عَذَابًا نُّكْرًا ﴿٨٧﴾﴾ [سورة الكهف:٨٧].

**"Akasema: Ama aliyedhulumu basi tutamuadhibu, na kisha atarudishwa kwa Mola wake Mlezi amuadhibu adhabu isiyojulikana"** [Al-Kahf: 87] Wakasema: Atarudishwa kwa kiongozi wa waumini (Ali) basi atamuadhibu adhabu isiyojulikana.

[71] Rejea: Maqaalaatul-Firaq (Uk. 146)

## Kauli yao kuwa: Dunia na Akhera ni miliki ya imamu anaziendesha atakavyo

Ameandika Mtunzi wa kitabu Al-Kaafiy mlango kauita: “Mlango wa: Ardhi yote ni miliki ya Imamu”[72] Na huu ni Ushirikina wa wazi katika uumbaji na uendeshaji, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

﴿أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ ٱللَّهَ لَهُۥ مُلْكُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۗ ﴿١٠٧﴾﴾ [سورة البقرة:١٠٧]. ﴿وَلِلَّهِ مُلْكُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۖ وَإِلَيْهِ ٱلْمَصِيرُ ﴿١٨﴾﴾ [سورة المائدة:١٨].

**“Hujui kwamba Mwenyezi Mungu ana ufalme wa Mbingu na Ardhi?”** [Baqara: 107] Na anasema: **“Na ni wa Mwenyezi Mungu tu, ufalme wa Mbingu na Ardhi, na marejeo ni kwake Yeye”** [Maida: 18]

## Sehemu ya Uungu iliyotua kwa Maimamu

Anasema Abuu Abdillah: “Kisha akatufuta kwa mkono wake wa kulia, basi nuru yake ikatuvaa”[73] Na akasema: “Lakini Mwenyezi Mungu alichanganyika nasi yeye mwenyewe”. Na sehemu hii ya uungu -kama wanavyodai- walipewa uwezo usiokuwa na mipaka, na ndio maana mwenye kusoma hiyo wanayoiita miujiza ya maimamu, atabaini kuwa maimamu

[72] Rejea: Mir-aatul-Anwari (Uk.59)
[73] Rejea: Usuulul-Kaafiy (1/440)

wamekuwa ni sawa na Mola Mlezi wa Walimwengu - Ametukuka na ametakasika mbali Mwenyezi Mungu na hayo wanayoyasema- katika kuhuisha, kufisha na kuumba.

Huyu Ali radhi za Allah ziwe juu yake, kwa madai yao, atawafufua wafu wote katika makaburi ya Jabana (huko Iraq), na aliwahi kulipiga jiwe wakatoka Ngamia mia moja. [[74]]

Ikiwa binadamu wamempa uwezo mkubwa wa kuhuisha na kufufua wafu, na kugawa riziki, wanatofauti gani na Wakristo wanaosema Yesu ni Mungu???! Na wanapopata neema wakasema Asante Yesu??!! Imani hii ni sawa na imani ya Wakristo wanaosema Yesu ni Mungu pamoja nasi-Tunamuomba Allah atuonyeshe haki na aturuzuku kuifuata-.

## Kauli zao kuhusu Tauhidi ya Majina na sifa

Na katika mifano aliyomzulia Al-Kulaini Abuu Abdillah Ja'fari Swaadiq nikuwa lisema: "Hakika mimi ninayajua yaliyoko mbinguni na Ardhini, na ninajua yaliyoko peponi, na ninayajua yaliyoko motoni, na ninayajua yaliyopita na yajayo" [[75]] Bali walisema: Hakika majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yaliyotajwa ndani ya Qur'ani, hayo ni

[[74]] Rejea: Bihaarul-Anwaar: (41/194)
[[75]] Usuulul-Kaafiy (1/261)

majina ya maimamu, wakasema: "Sisi Wallahi ndio majina mazuri, ambayo Mwenyezi Mungu hakubali kutoka kwa waja amali yoyote isipokuwa kwa kutujua sisi"[76] Na ameeleza Shahrustani kuwa itikadi hii ni itikadi ya waliyochupa mipaka waliyoipokea kutoka kwa Mayahudi na Wakristo. [77]

## Kuwaamini Malaika

Na miongoni mwa kauli zao nikuwa: Malaika waliumbwa kwa Nuru ya Ali radhi za Allah ziwe juu yake, na kwamba Uhai wa Malaika unategemea kumpenda Ali radhi za Allah ziwe juu yake na kuwaombea msamaha watetezi wake, kwa sababu hilo ni kama sehemu ya chakula chao na kinywaji chao, wakasem: "Hawana chakula wala kinywaji isipokuwa kwa kumtakia rehema Ali radhi za Allah ziwe juu yake na vipenzi vyake, na kuwaombea msamaha watetezi wake wakosefu"[78] Na walidai kuwa wako miongoni mwa Malaika wa Rahmani ambao hawana kazi haswa zaidi ya kulia juu ya kaburi la Huseini, wakasema: "Mwenyezi Mungu kawaweka mawakala katika kaburi la Husein Malaika elfu nne, wenye nywele timtimu, na waliojaa vumbi, wakimlilia

[76] Marejeo hayo hayo (1/143-144)
[77] Rejea: Almilal wan Nihal (1/173)
[78] Bihaarul-Anwaar (26/354)

mpaka siku ya Kiyama"[79] Maneno haya pamoja nakuwa ni uongo wa wazi ila ni ajabu sana kupata mtu mwenye akili timamu akiyaamini!.

## Kuamini vitabu

Wanadai Ithna-asheria kuwa kuna vitabu vitakatifu vilivyoteremka kutoka mbinguni na wahyi kutoka kwa Mola Mlezi mwenye nguvu Mtukufu kuja kwa maimamu.[80]

## Kuwaamini Mitume

Mitume ndio binadamu bora na ndio wenye haki zaidi ya utume kuliko wengineo; kiasi kwamba Mwenyezi Mungu aliwaandaa kwa ukamilifu wa ibada na kufikisha na kulingania na Jihadi:

﴿ٱللَّهُ أَعۡلَمُ حَيۡثُ يَجۡعَلُ رِسَالَتَهُۥۗ ١٢٤﴾ [سورة الأنعام:١٢٤].

**"Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi kuliko wote kujua wapi anaweka ujumbe wake"** [An-Aam:124]

Wamesifika kwa nafasi ya utume kuliko watu wote, na hakuna binadamu yeyote anaweza kuwa bora kuliko wao,

[79] Rejea: Wasaailu-Shia (10/318)
[80] Rejea: Maqaalaatul-Firaq (150)

na katika upotofu wa kundi hili la kipagani katika nguzo hii ni:

**Kuwafanya bora maimamu kuliko Manabii:** Aliandika mlango Sheikh wao Al-Majlisiy katika kitabu (Bihaarul-Anwaar) kwa anwani: "Mlango wa kuwafanya bora maimamu (Alaihimus-salaam) kuliko Manabii, na juu ya viumbe wote…"[81] Na kama alivyolithibitisha hilo mkubwa wao katika kitabu chake (Al-hukuumatul-Islaamiyya) aliposema: "Hakika miongoni mwa mambo muhimu katika madhehebu yetu nikuwa maimamu wetu wana nafasi kubwa ambayo hawezi kuifikia Malaika aliye karibu na Mwenyezi Mungu, wala Nabii aliyetumwa, na imekuja kutoka kwao pia kuwa: Hakika sisi pamoja na Mwenyezi Munug tuna hali ambayo haisikii Malaika aliye karibu na Mwenyezi Mungu wala Nabii aliyetumwa"[82]

## Kauli yao kuwa maimamu wana miujiza kama miujiza ya Manabii

Wanadai kuwa Mwenyezi Mungu aliwatia nguvu maimamu wao kwa miujiza, anasema Al-Bahrani katika kitabu chake alichokitunga kuhusu miujiza ya maimamu: "Hakika Mwenyezi Mungu alidhihirisha kupitia mikono yao miujiza na dalili,

[81] Rejea: Bihaarul-Anwaar (26/267)
[82] Rejea: Al-Hukuumatul-Islamiyya (Uk. 59)

kwa sababu wao ndio hoja yake kwa waja wake"[83] Na hii ni imani ya makafiri kama walokole na wengineo, kuamini kuwa wachungaji wao wanatenda miujiza!.

Na itikadi hii ni batili kwa itifaki ya wanachuoni wote, kwa sababu miujiza hakuna awezaye kuileta isipokuwa Nabii, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ameifanya hoja kwa waja wake ni kuwatuma Mitume na si maimamu, amesema Mtukufu:

﴿ رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى ٱللَّهِ حُجَّةٌۢ بَعۡدَ ٱلرُّسُلِۚ ﴿١٦٥﴾ ﴾ [سورة النساء: ١٦٥].

**"Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletwa Mitume"** [An-Nisaai: 165] Na hakuwataja maimamu!.

## Kuamini siku ya Mwisho

Kuamini siku ya Mwisho ni moja kati ya nguzo kubwa za Imani, na ni katika mambo waliyokubaliana Manabii wote -amani iwe juu yao- lakini Ithna-asheria wana sehemu ya upotofu katika mlango huu, na miongoni mwa upotofu wao ni kauli yao kuwa amri ya siku ya Mwisho ni ya Imamu, anasema mtunzi wa kitabu cha Al-Kaafiy: "Akhera ni ya

[83] Rejea: Yanabiiul-Ma'aajizi-Hashim Al-Bahraani (Uk. 2)

Imamu anaiweka mahala popote atakapo, na anamuepushia amtakaye, ameruhusiwa hilo kutoka kwa Mwenyezi Mungu"[84]

Na wanasema: "Lau kama si maimamu isingeumbwa pepo na moto"[85] Na: "Hakika Mwenyezi Mungu aliiumba Pepo kutokana na nuru ya Husein"[86]

Na mara nyingine wanasema Pepo ni sehemu ya mahari ya Fatma alipoolewa na Ali!! Imekuja katika vyanzo vyao kuwa: "Hakika Mwenyezi Mungu alimpa mahari Fatma ya robo ya Dunia, hivyo robo ya Dunia ni yake, na akampa mahari ya Pepo na moto, anawaingiza maadui zake motoni, na anawaingiza vipenzi vyake peponi"[87]

Hebu tafakari upuuzi huu, inawezekanaje pepo kuwa mahari ya Fatma, hali yakuwa pepo hiyo hiyo imeumbwa kutokana na nuru ya mwanaye Husein!!

## Miongoni mwa itikadi zao

**Kukingwa na makosa:** Swala la Imamu kukingwa na kukosea lina umuhimu mkubwa kwa Raafidhwa Ithna-asheria, nalo ni katika misingi muhimu katika itikadi yao.

[84] Usuulul-Kaafiy (1/409)
[85] Rejea: Al-I'tiqaadaat (Uk. 106-107)
[86] Rejea: Al-Maalimuz-Zulfaa (Uk. 149)
[87] Marejeo hayo hayo (350)

Na kukingwa maana yake: "Kukingwa kwa maimamu kutokana na madhambi makubwa na madogo, halitokei dhambi lolote kamwe kwao, si makusudi wala kwa kusahau wala kukosea kwa sababu ya kutoelewa jambo vizuri, kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu"[88]

Na sura hii ya kukingwa wanayowasifu nayo maimamu wao haikupatikana hata kwa Manabii na Mitume wa Mwenyezi Mungu, bali kukanusha kughafilika na kusahau moja kwa moja kwa maimamu, ni kuwafananisha na asiyepatwa na usingizi wala kulala (Allah).[89]

Na itikadi hii haipishani mbali na itikadi ya Wakristo wanaoamini kuwa Papa, na mapadri wao ni watakatifu!.

## Kurejea kwa wafu

Wanamaanisha: "Kurejea kwa wafu wengi Duniani kabla ya siku ya Kiyama baada yakuwa wamekufa" wanarejea "kuwa hai baada ya kifo" kabla ya siku hiyo iliyoahidiwa wanarudi "katika sura zao walizokuwa nazo".[90]

Na mtu wa kwanza kusema itikadi hii ni Yahudi bin Sabai aliyekuwa akidai kuwa Muhammad rehema na amani ziwe juu yake atarudi kuwa hai baada ya kufa

[88] Rejea: Bihaarul-Anwaar (25/211)
[89] Rejea: Maqaalaatul-Firaq (Uk159)
[90] Rejea: Awaailul-Maqaalaati (Uk. 95)

kwake, kisha akabadili kauli na kusema kuwa Ali radhi za Allah ziwe juu yake atarejea tena kuwa hai, na alisema zilipomfikia habari za kifo cha Ali, akasema kumwambia aliyemletea taarifa: "Umesema uongo, lau ungetuletea ubongo wake katika bakuli sabini, na ukamuua mbele yetu mara sabini, basi sisi tungejua kuwa hajafa, na wala hujamuuwa, na wala hatokufa mpaka aimiliki Ardhi"[91]

Na mzizi wa itikadi hii inatokana na athari ya itikadi za Kiyahudi na Kikristo, kama wanavyoona baadhi ya watafiti.[92]

Na itikadi hii inakwenda kinyume wazi kabisa na Qur'ani, kwani kurejea kumebatilishwa katika Aya nyingi za Qur'ani ikiwemo kauli yake Mtukufu:

﴿قَالَ رَبِّ ارْجِعُونِ ﴿٩٩﴾ لَعَلِّي أَعْمَلُ صَالِحًا فِيمَا تَرَكْتُ كَلَّا إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَائِلُهَا وَمِن وَرَائِهِم بَرْزَخٌ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٠٠﴾﴾ [سورة المؤمنون:٩٩-١٠٠].

**"Husema: Mola wangu Mlezi nirudishe!** [99] **Ili nitende mema sasa badala ya yale niliyoyaacha. Wapi! Hii ni kauli aisemayo yeye tu. Na nyuma yao kipo kizuizi (barazahi) mpaka siku watakapo fufuliwa"** [Mu'minuun: 99-100] Na kauli yake Mtukufu: **"Na nyuma yao kipo**

[91] Rejea: Al-Maqaalatu-wal-firaq: (Uk.21)
[92] Rejea: Maqaalaatul-Firaq (Uk.161)

**kizuizi (barazahi) mpaka siku watakapo fufuliwa”** Inakanusha wazi moja kwa moja kurejea duniani.

## Kujitokeza kwa maimamu

Yaani: Kujitokeza kwa maimamu baada ya kufa kwao kwa baadhi ya watu, kisha wanarudi makaburini mwao (vichekesho!), na ameandika mlango Al-Majlisiy: “Mlango wa kuwa wao hujitokeza baada ya kufa kwao, na yakaonekana maajabu yao”[93] Na hii ni tofauti na itikadi ya kurejea.

## Itikadi ya Taqiyya (Kuficha unachoamini)

Wanamaanisha: “Ni mtu kusema au kufanya kinyume na unavyoamini, ili kuzuia madhara kwako au kwa mali yako, au kulinda heshima yako”[94] Na maana hii haiendani na uhalisia wa Taqiyya ya Mashia, kwa sababu Taqiyya yao haihusiani tu na kuzuia madhara pekee, bali ni wajibu uliothibiti na ni hali endelevu, hawaachi kuifanyia kazi mpaka atakapotoka Mahadi wao wa uongo.

[93] Rejea: Bihaarul-Anwaar (27/303-304)
[94] Rejea: Ash-shia fil-Miizaan (Uk. 48)

## Je kuficha imani (Taqiyya) kulikotajwa ndani ya Qur'ani ndiko huko wanakofanya Mashia?

Kuficha imani katika Uislamu ni ruhusa katika hali ya dharura, na mara nyingi kunakuwa mtu anapokuwa pamoja na makafiri (na akahofia madhara juu ya nafsi yake), amesema Mtukufu:

﴿إِلَّآ أَن تَتَّقُواْ مِنۡهُمۡ تُقَىٰةٗۗ ٢٨﴾ [سورة آل عمران:٢٨].

**"ila ikiwa ni kwa ajili ya kujilinda na shari zao"** [Al-Imran: 28] Amesema bin Jariri Twabari: "Kuficha imani alikokutaja Mwenyezi Mungu katika Aya hii, si vinginevyo isipokuwa ni mtu kuficha imani anapokuwa na makafiri, na si kwa wengineo"[95]

Ama kwa Mashia ithna-asheria ni nguzo katika nguzo za dini yao, bali kuficha imani ndio dini yote, na hana dini asiyeficha imani.[96]

## Itikadi ya kaudongo

Maana yake: Ni itikadi yao kuwa wao waliumbwa kutokana na udongo safi, na watu wengine waliumbwa kutokana na udongo mchafu.[97]

[95] Rejea: Tafsiir Twabari (6/316)
[96] Rejea: Maqaalaatul-Firaq (Uk. 163)

## Siri ya kaudongo

Itikadi ya kiudongo ni miongoni mwa itikadi za siri ambazo hupeana usia kuzificha hata kwa waumini wa kawaida; kwa sababu wao husema: Lau angeona muumini wa kawaida wa kishia itikadi hii "Basi angefanya makusudi kufanya madhambi makubwa (kama Zinaa, Ulevi, na mengineyo) ili kupata ladha za dunia, na angefanya hivyo kwa kujua kwake kuwa adhabu ya madhambi hayo Akhera atapewa mtu mwingine"[98]

## Mwanzo wa itikadi ya kaudongo

Aliyesimamia kupandikiza itikadi hii mbovu ni Sheikh wao Al-Kulaini aliyefariki mwaka (329. Hijiria), aliyeandika mlango kwa anwani ya: "Mlango wa udongo wa muumini na udongo wa kafiri"[99]

Na huenda ufafanuzi mpana wa itikadi hii ni yale yaliyokuja katika mapokezi ya Sheikh wao Bin Baabawaihi, na muhtasari wake: Nikuwa Shia (kwa madai yao) ameumbwa kutokana na udongo maalum, na wanauita (Udongo msafi, au udongo wa Ahlul-Baiti) na Msuni (anayefuata muongozo wa Mtume) ameumbwa kutokana na udongo mwingine,

[97] Rejea: marejeo hayo hyao (uk. 169)
[98] Rejea: Al-Anwaarun-Nu'maaniyya (1/195)
[99] Usuulul-Kaafiy (1/2-6)

wanauita (udongo uliolaaniwa, au udongo wa usaa wa watu wa motoni) na ukafanyika uchanganyaji baina ya dongo mbili kwa namna maalum, hivyo yanayojitokeza kwa Shia miongoni mwa maasi na uhalifu, ni kwa sababu ya kuathirika kwake na udongo mchafu, na uzuri na uaminifu ulioko kwa Msuni ni kwa sababu ya kuathirika kwake na Mshia, basi itakapofika siku ya Kiyama madhambi na adhabu za Mshia zitawekwa kwa watu wa Sunna, na mema ya watu wa Sunna watapewa Mashia.[100]

## Ubatili wa itikadi ya kiudongo

Itikadi hii ubatili wake uko wazi, na itoshe kuvuta picha ya uove wake ili kujua ubatili wake, na ni katika fedheha ya madhehebu ya Ithna-asheria na aibu yao, na Shia haoni haya hadi leo kuonyesha wazi itikadi hii na kuitangaza..

Bila shaka riwaya hizi kuhusu udongo alioumbwa nao Mshia zinapingana na uhalisia wao, Mashia kama unavyoona wamezama sana katika uhalifu, na uvamizi, na maasi na madhambi makubwa, na miamala mibaya, tabia chafu na dini mbovu, hivi inawezekana vipi mwenye hali kama hii awe ni udongo msafi, na awe kiumbe msafi kuliko wengine?!

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaumba watu katika umbile salama la Uislamu, amesema Mtukufu:

[100] Rejea: Maqaalaatul-Firaq (169)

﴿ فَأَقِمۡ وَجۡهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفٗاۚ فِطۡرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِي فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيۡهَاۚ لَا تَبۡدِيلَ لِخَلۡقِ ٱللَّهِۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلۡقَيِّمُ ٣٠ ﴾ [سورة الروم: ٣٠].

**“Basi uelekeze uso wako sawa sawa kwenye Dini. Ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumba watu, hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu, hiyo ndio Dini iliyonyooka sawa”** [Ar-Rum:30]

Na ama yaliyothibitishwa na habari zao kuwa madhambi makubwa ya Mshia na mizigo yake ataibeba mtu wa Sunna, na mema ya watu wote watapewa Mashia, maneno haya yanapingana na uadilifu wa Mola Mlezi, na hayaendani na akili timamu wala maumbile salama, achilia mbali maandiko ya Sheria na msingi ya Uislamu, amesema Mtukufu:

﴿ وَلَا تَكۡسِبُ كُلُّ نَفۡسٍ إِلَّا عَلَيۡهَاۚ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٞ وِزۡرَ أُخۡرَىٰۚ ١٦٤ ﴾ [سورة الأنعام: ١٦٤].

**“Na kila nafsi haichumi isipokuwa juu yake yenyewe. Na habebi mwenye kubeba mzigo wa mwenzie”** [An’aam: 164] Na akasema Mtukufu:

﴿ كُلُّ ٱمۡرِيِٕۭ بِمَا كَسَبَ رَهِينٞ ٢١ ﴾ [سورة الطور: ٢١].

**“Kila mtu lazima atapata alichokichuma”** [Tuur: 21] Na akasema Mtukufu:

﴿فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُۥ ﴿٧﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُۥ ﴿٨﴾﴾ [سورة الزلزلة:٧-٨].

**“Basi anayetenda chembe ya wema, atauona * Na anayetenda chembe ya ovu atauona!”** [Az-zalzala: 7-8] Na kauli yake Mtukufu:

﴿ٱلْيَوْمَ تُجْزَىٰ كُلُّ نَفْسٍۭ بِمَا كَسَبَتْ ۚ لَا ظُلْمَ ٱلْيَوْمَ ﴿١٧﴾﴾ [سورة غافر:١٧].

**“Leo kila nafsi italipwa kwa iliyo chuma. Hapana dhuluma leo”** [Ghafir: 17]. Na Aya nyinginezo nyingi.

## Imamu Mahdi na kutoweka kwake

Kutoweka kwa Imamu Mahdi ni madai yao kuwa Hasan Al-Askari aliyefariki mwaka 260.H, akiwa mtoto mchanga, alitoweka baada tu ya kuzaliwa kwake kwa kuhofia kuuawa, na bado yuko hai mpaka hivi sasa, na kwamba yeye ndiye Mahdi anayesubiriwa ambaye atarudi kwa ajili kuijaza Ardhi uadilifu, na ndiye Imamu wa Waislamu wa kisheria tangu mwaka 260 Hijiria.[101]

[101] Rejea: Maqaalaatul-Firaq (Uk. 171)

## Mizizi ya itikadi ya Imamu Mahdi

Itikadi ya Raafidhwa ithna-asheria kuhusu Mahdi na kutoweka, inarudi katika misingi ya Majusi (Makafiri waabudu moto), Mashia wengi wao wanatokea Iran, na Iran miongoni mwa dini zao ni Umajusi, na Majusi wanadai kuwa wana kiongozi wao wanayemsubiri, yuko na ataendelea kubakia, aliyeongozwa, katika watoto wa (Bashtasaf bin Bahrasaf), anaitwa: Abshauthan, na kwamba yuko katika ngome kubwa kati ya Iran na China, na itikadi hii inakwenda sambamba na kiini cha madhehebu ya Ithna-asheria.[102]

Na Imamu Mahdi anayedaiwa hapa ni maneno ya uongo na ya kutunga, na wala hakuna uhalisia wala uthibitisho wowote, kama tulivyotangulia kusema.

## Ndoa ya Mut'aa (mkataba)

**Mut'aa ni nini?:** Anasema Muhammad bin Husein Attusiy: "Mut'aa ni kuingia makubaliano ya kustarehe na mwanamke kwa muda maalum na kwa malipo maalum"[103]

Anasema Sayid Husein Al-Musa (Shia aliyetubia): Hakika imetumika Mut'aa kama fursa mbaya zaidi, na akadhalilishwa mwanamke kwa udhalili mbaya, na watu wengi wakawa

---

[102] Mrejeo yaliyopita (Uk. 174)
[103] Rejea: An-Nihaayaa (Uk. 489)

wanashibisha matamanio ya hisia zao za (ngono) chini ya pazia la Mut'aa na kwa jina la dini, kwa madai ya kuifanyia kazi kauli yake Mtukufu:

﴿فَمَا ٱسۡتَمۡتَعۡتُم بِهِۦ مِنۡهُنَّ فَـَٔاتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ فَرِيضَةً ٢٤﴾ [سورة النساء:٢٤].

**"kama mnavyostarehe nao, basi wapeni mahari yao kwa kuwa ni wajibu"** [An-Nisaai:24]

Na wameandika riwaya nyingi za kuhamasisha Mut'aa, na wakaainisha malipo na thawabu zake, na adhabu kwa mwenye kuiacha, bali wakamzingatia yeyote ambaye hajaifanyia kazi si Muislamu.

**Hebu tusome pamoja ushahidi (wao) huu (wa uongo):**

1. Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: **"Atakayestarehe na mwanamke muumini, atakuwa kama kazuru Al-Kaaba mara sabini"** Hivi mwenye kustarehe anakuwa sawa na aliyezuru Al-Kaaba mara sabini? Na nani? Na mwanamke muumini?!

2. Amepokea Swaduq kutoka kwa Swadiq alaihis salaam, amesema: **"Hakika Mut'aa ni dini yangu, na ni dini ya baba zangu, atakayeifanya basi atakuwa ameifanyia kazi dini yetu, na atakayeipinga basi ameipinga dini yetu, na atakuwa kaitakidi kinyume na dini yetu"** Maneno haya yako katika kitabu:

Manlaa Yahdhuruhul-Faqiih (3/366). Na huku ni kumtia katika ukafiri mtu yeyote asiyekubaliana na Mut'aa.

3. Amepokea Sayid fat-hallah Al-Kaashaani katika tafsiri ya Manhajus Swaadiqiin, kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, amesema: **"Atakayestarehe na mwanamke atakuwa na daraja kama ya Husein alaihis salaam, na atakayestarehe mara mbili daraja yake itakuwa sawa na Hasan alaihis salaam, na atakayestarehe mara tatu atakuwa sawa na daraja ya Ali bin Abii twalib alaihis salaam, na atakaye starehe mara nne basi daraja yake itakuwa sawa na daraja yangu"** [104]

Hebu tuchukulie, lau kama mtu mshenzi atastarehe mara moja hivi daraja yake itakuwa sawa na daraja ya Husein radhi za Allah ziwe juu yake, na akistarehe mara mbili au tatu au nne, hivi daraja yake itakuwa sawa na daraja ya Hasan na Ali na Mtume rehema na amani ziwe juu yake?!

Hivi daraja ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na daraja ya maimamu ndio imekuwa ya kudhalilishwa kiasi hiki?! Na hata kama mwenye kustarehe atakuwa kafikia daraja ya juu kiasi gani ya imani, ndio atakuwa na

[104] Rejea: Kitabu: Lillaahi thumma littaariikh (Uk. 34-35)

daraja sawa na Husein, au kaka yake, au baba yake, au babu yake?!

Hakika nafasi ya Husein ni tukufu na ya juu zaidi kuliko kufikiwa na yeyote, vyovyote vile atakavyokuwa na imani ya nguvu kiasi gani, na daraja ya Hasan na Ali na Mtume rehema na amani ziwe juu yake, hakuna awezaye kuifikia, vyovyote itakavyopea na kuwa juu imani yake.

## Usahihi kuhusu Mut'aa

Na ukweli kuhusu swala hili nikuwa Mut'aa iliharamishwa siku ya Khaibar.

Amesema kiongozi wa waumini Ali radhi za Allah ziwe juu yake: "Aliharamisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake siku ya Khaibar nyama ya punda wa nyumbani na ndoa ya Mut'aa"[105]

Na kutoka kwa Sabra bin Ma'bad Al-Juhani: Ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliharamisha Mut'aa siku ya Ufunguzi wa Makka (Fat-hu Makkah)" Kaipokea Muslim.

Na zimekuja hadithi nyingi kuelezea uharamu wa Mut'aa na nafasi haitoshi kuzielezea zote.

[105] Tazama: Attahdhiib: 2/142

Na aliulizwa Abuu Abdillah (Ja'far As Swadiq): "Je Waislamu katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake walikuwa wakioa bila mashahidi? Akasema: Hapana"[106]

Na hapana shaka kuwa ushahidi huu ni hoja ya kukata mzozo katika kufutwa kwa hukumu ya Mut'aa na kuibatilisha.[107]

Na ama hadithi zinazoelezea ubora wa kufanya Mut'aa na malipo yake, ni hadithi za Mashia za kutunga, na ni uongo wanaounasibisha kwa Mtume, na Mtume yuko mbali nao, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.

Kwa muhtasari nikuwa: Mut'aa ni uchafu ambao hakuna mwenye imani na akili timamu anayeuridhia kwa binti yake au bint wa ndugu yake wa damu, na ukitaka kulithibitisha hilo, mfuate Sheikh yeyote wa Kishia mwenye mabinti, mwambie kuwa ninahitaji binti yako nistarehe naye kwa muda kisha nimlipe niachane naye! Kamwe hatokubali!. Kisha uchafu huu wanaufanya na kuwafundisha watu wengine!.

[106] Marejeo hayo hayo (Uk. 189

[107] Rejea: Lillaahi thumma littaariikh (Uk. 39)

# SEHEMU YA SITA

## Aashuraa ni nini?

Aashuraa: Ni siku ya tarehe 10 ya mwezi wa kwanza (Muharram) katika kalenda ya Kiislamu, na katika historia ni siku ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuokoa Nabii Mussa amani iwe juu yake, kutokana na mateso ya Firauni.

Hivyo kwa Mashia: Ni siku ya maombolezo na mikutano, na ibada zinazofanyika katika siku ya kumi ya mwezi Muharram kwa kuhuisha kumbukumbu ya kuuawa kwa Husein bin Ali katika vita vya Karbalaa (Iraq).

## Mambo yanayofanyika siku ya Aashuraa

1- **Vikao vya maombolezo:** Hukusanyika katika vikao hivyo ili kusikiliza hotuba, na wakisimuliana matukio ya Karbalaa, na wakikumbushana kuuawa kwa Husein na watu wa familia yake.

2- **Kujipiga:** Hujipiga kifua na uso, kama ishara ya kuelezea huzuni yao.

3- Kujikata: Kwa baadhi yao hujipiga kichwa kwa panga, na vitu vyenye ncha kali mpaka wanatiririka damu.

4- **Matembezi na misafara:** Hukusanyika na kufanya matembezi mitaani, wakiwa wamebeba bendera nyeusi na wakiimba nyimbo za huzuni.

5- **Kulisha watu chakula na kutia nadhiri:** Hufanya wengi wao zoezi la kugawa vyakula na vinywaji, ikiwa kama sadaka na nadhiri kwa jina la Husein.

## Kufuru inayofanyika katika siku ya Aashuraa

1- Kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kutaka msaada kwa wafu, mfano kauli yao: "Yaa Husein Aghthinii" Ewe Husein nisaidie" au "Yaa Ali adirikni" Ewe Ali niokoe.

Na yamesikika maneno kutoka kwa kiongozi wao hapa nchini Tanzania (Sheikh Jalala) kwenye matembezi yao siku ya Aashuraa ya Mwaka 2022 Jijini Dar es salaam, ndani ya dua yake kwa Raisi, baada ya kumuomba Allah pia akamuomba (mfu) Abuu Abdillaah Al-Husein awe pamoja naye katika utendaji wake.[108]

Na kuthibitisha haya skani QR kodi hii ili kusikia maneno hayo katika mtandao wa Facebook.

[108] Tazama clip hii katika mtandao wa Facebook: https://www.facebook.com/share/v/17gnDXLiUU/

Au ingiza kiunganishi (Link) iliyoko hapo juu.

2- Na miongoni mwa mambo ya shirki ni kutufu (kuzunguka) makaburi na kuweka kwao nadhiri kwa jina la Husein, au Ali, katika vichinjwa vyao, na kuwaomba wawatimizie haja zao.

3- Kuwatukana baadhi ya Maswahaba, na kuwakashifu, hasa hasa katika misimu ya maombolezo.

Na mengine mengi wanayoyafanya katika siku hiyo.

## Majibu ya Kufuru zao

1- Kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu, au kumshirikisha pamoja na Mwenyezi Mungu, na kutaka msaada kwa wafu:

Wafu ni watu ambao hawamiliki manufaa wala madhara kwa nafsi zao, achilia mbali kumnufaisha au kumdhuru mtu mwingine, bali hawasikii maombi yao wala hawajui hata kinachoendelea katika mambo yao, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُواْ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَن لَّا يَسْتَجِيبُ لَهُۥٓ إِلَىٰ يَوْمِ ٱلْقِيَٰمَةِ وَهُمْ عَن دُعَآئِهِمْ غَٰفِلُونَ ٥ ﴾ [سورة الأحقاف:٥].

**“Na ni nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawata waitikia mpaka siku ya Kiyama, na wala hawatambui maombi yao”** [Al-Ahqaaf: 5]

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu akakataza kumuomba asiyekuwa yeye, akasema:

﴿ وَلَا تَدۡعُ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَا لَا يَنفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَۖ ﴾ [سورة يونس:١٠٦].

**“Na wala usiwaombe wasiokuwa Mwenyezi Mungu ambao hawakufai kitu wala hawakudhuru”** [Yunus: 106]

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu akaeleza kuwa kumuomba mwingine pamoja na yeye, huo ni ukafiri. Akasema Mtukufu:

﴿ وَمَن يَدۡعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ لَا بُرۡهَٰنَ لَهُۥ بِهِۦ فَإِنَّمَا حِسَابُهُۥ عِندَ رَبِّهِۦٓۚ إِنَّهُۥ لَا يُفۡلِحُ ٱلۡكَٰفِرُونَ ﴾ [سورة المؤمنون:١١٧].

**“Na anayemuomba -pamoja na Mwenyezi Mungu- mungu mwinginewe, hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hesabu yake iko kwa Mola wake Mlezi. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi”** [Al-Mu’minuun: 117].

2- Kutufu katika makaburi na nadhiri wanazo ziweka: Kutufu na nadhiri ni ibada zinazopaswa kuelekezwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake,

na kuzielekeza kwa asiyekuwa yeye ni kumshirikisha kiumbe katika ibada za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na hili ni katika madhambi makubwa, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَلۡيَطَّوَّفُواْ بِٱلۡبَيۡتِ ٱلۡعَتِيقِ ٢٩﴾ [سورة الحج:٢٩].

**“Na waizunguke nyumba ya kale”** [Haji: 29]

Na kauli yake Mtume rehema na amani ziwe juu yake:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، أَنّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ: «قَاتَلَ اللَّهُ الْيَهُودَ، اتَّخَذُوا قُبُورَ أَنْبِيَائِهِمْ مَسَاجِدَ» [البخاري]

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira, yakwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: **“Mwenyezi Mungu amewalaani Mayahudi, waliyafanya makaburi ya Manabii wao kuwa mahali pa ibada”** [Bukhari]

Hatukuamrishwa kutufu isipokuwa katika nyumba kongwe (Al-Ka’aba) pekee, ama kufanya hivyo mahala pengine hakuna Aya wala mafundisho sahihi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake, yaliyotulekeza kufanya hivyo.

Na ama kuhusu nadhiri akasema Mtukufu:

﴿وَمَآ أَنفَقْتُم مِّن نَّفَقَةٍ أَوْ نَذَرْتُم مِّن نَّذْرٍ فَإِنَّ ٱللَّهَ يَعْلَمُهُۥ﴾ [سورة البقرة: ٢٧٠].

**"Na chochote mnachotoa, au nadhiri mnazoweka basi hakika Mwenyezi Mungu anajua"** [Al-Baqara: 270]

وفي الصحيح عن عائشة رضي الله عنها: أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال:

((من نذر أن يطيع الله فليطعه ; ومن نذر أن يعصي الله فلا يعصه))

Na imekuja katika Sahihi Bukhari kutoka kwa Aisha radhi za Allah ziwe juu yake: Ya kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: **"Atakayeweka nadhiri ya kumtii Mwenyezi Mungu basi na amtii, na atakaye weka nadhiri ya kumuasi Mwenyezi Mungu, basi na asimuasi".**

3- Wamekubaliana wanachuoni wote Allah awarehemu kuwa, atakayemtukana Aisha radhi za Allah ziwe juu yake, na akamtuhumu kwa yale ambayo Mwenyezi Mungu aliyakanusha basi huyo ni kafiri, kwa sababu amei kadhibisha Qur'ani, na makubaliano haya ameyaeleza mwanachuoni zaidi ya mmoja, kama vile Sheikhul-Islami bin Taimiya na Imamu binil-Qayyim, na Al-Hafidh bin Kathiri.[109]

[109] Rejea: Diraasaatun Fii ilmil-Aqiidah, cha Dr. Naasir Al-qifaari (4/403-405)

Na akaeleza Sheikhul-Islami bin Taimiya kuwa hata kumtukana Swahaba mwingine hukumu yake ni sawa na kumtukana Aisha.

Na bila shaka historia inaonyesha kuwa Husein radhi za Allah ziwe juu yake si Swahaba wa mwisho kufa, bali walibakia Maswahaba wengi baada yake.

Swali la msingi la kujiuliza: Je, ni nani katika Maswahaba waliobakia hai baada ya kifo cha Husein mwaka 61.Hijiria, alifanya mfano wa hayo mnayoyafanya Mashia?!

Na ikiwa hakuna, hivi nyinyi mnajua sana dini, na mna imani na uchungu sana kuliko Maswahaba?! Na baadhi yao walikuwa ni katika ndugu zake wa damu, kama mwanaye Ali bin Husein! (Zeinul-Aabidiin, aliyefariki mwaka 95.Hijiria)!

Na je, maombolezo ya namna hiyo ndivyo tulivyo fundishwa katika Qur'ani na Sunna za Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-?

## Lipi jambo sahihi la kufanya siku ya Aashuraa

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم: «صَوْمُ يَوْمِ عَاشُورَاءَ، يَوْمٌ كَانَتْ تَصُومُهُ الْأَنْبِيَاءُ فَصُومُوهُ أَنْتُمْ» [مصنف ابن أبي شيبة]

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake amesema: Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: **"Swaumu ya siku ya Aashuraa, ni siku ambayo walikuwa wakiifunga Manabii, basi ifungeni"** [Muswannaf bin Abii Shaiba].

قَالُوا: يَا رَسُولَ اللهِ، فَمَا تَقُولُ فِي صَوْمِ يَوْمِ عَاشُورَاءَ؟ قَالَ: ((إِنِّي لَأَحْتَسِبُ عَلَى اللهِ أَنْ يُكَفِّرَ السَّنَةَ)) [مسند أبي داود]

Maswahaba walimuuliza Mtume rehema na amani ziwe juu yake, wakasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu unasemaje kuhusu swaumu ya siku ya Aashuraa? Akasema: **"Hakika mimi ninataraji kwa Mwenyezi Mungu kuwa itafuta makosa ya mwaka mzima"** [Musnad Abii Daud].

## Je, wanayofanya Mashia siku ya Aashuraa ndio waliyoamrishwa?

Imekuja katika kitabu chao cha Maqtalul-Husein, cha mwandishi: Assayyid Abdul-Razaq Al-Musawiy, baada ya kutaja kisa cha kuingia Abdallah bin Sinani kwa Abii Abdillah Asswaadiq, anasema: "Kisha Abuu Abdillah Asswadiq akamuamrisha Abdallah awe katika muonekano wa wafiwa wa ndani wa marehemu, awe akifungua kikoi chake na kufunua miundi yake, na awe na masikitiko, na wala asifunge swaumu siku nzima, na afungue kinywa baada ya Laasiri kwa lisaa limoja kwa kunywa maji…"[110]

Na maombolezo haya wameyawekea thawabu na malipo tofauti na yale aliyoyaeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika swaumu ya Aashuraa, jambo linaloonyesha wazi kuwa Ushia si Uislamu, bali ni Dini iliyoegemezwa katika Uislamu, kwa mfamo:

Anasema Ali bin Musa Twausi katika kitabu chake, Al-Malhuuf alaa qatlat tufuuf: Imepokelewa kutoka kwa Maulana Al-Baaqir alaihis salaam yakwamba yeye amesema: "Alikuwa Zainul-Aabidiin alaihis salaam, akisema: Muumini yeyote yatakaye bubujika macho yake machozi kwa ajili ya kuuawa kwa Husein aliahis salaam, mpaka yakatiririka katika shavu lake, basi Mwenyezi Mungu atamuandalia kwa machozi hayo, vyumba peponi, ataishi humo miongo na miongo…"[111] Na malipo mengine mengi waliyoyatunga na

---

[110] Rejea: Maqtalul-Husein- Assayyid Abdurrazaaq Al-Muqrim (Uk. 224-225)


[111] Rejea: Al-Malhuuf Alaa qatlat twufuuf, cha Ali bin Musa Twausi (Uk. 86)

kuyanasibisha kwa Maimamu, na Maimamu wako mbali na hayo.

## SEHEMU YA SABA

## Maneno machafu ya Al-Khomeini kwa Maswahaba

Anasema Imamu wao Mkuu na Alama ya Mwenyezi Mungu (kama wanavyomtukuza kwa jina hilo) katika kitabu chake Attwahaara:



النوع العاشر : الكافر ................................................ ٥٧؛

ثمّ إنّ المتيقّن من الإجماع هو كفر النواصب والخوارج؛ أي الطائفتين المعروفتين، وهم الذين نصبوا للأئمّة عليهم السلام أو لأحدهم بعنوان التديّن به؛ وأنّ ذلك وظيفة دينية لهم، أو خرجوا على أحدهم كذلك، كالخوارج المعروفة. والظاهر أنّ «الناصب» الوارد في الروايات ـكموثّقة ابن أبي يعفور المتقدّمةـ أيضاً يراد به ذلك؛ فإنّ النواصب كانوا طائفة معهودة في تلك الأعصار، كما يظهر من الموثّقة أيضاً، حيث نهي فيها عن الاغتسال في غسالة الحمّام التي يغتسل فيها الطوائف الثلاث والناصب، وليس المراد منه المعنى الاشتقاقي الصادق على كلّ من نصب بأيّ عنوان كان، بل المراد هو الطائفة المعروفة، وهم النصّاب الذين كانوا يتديّنون بالنصب، ولعلّهم من شعب الخوارج.

**طهارة الناصب والخارج لغرض دنيوي ونحوه**

وأمّا سائر الطوائف من النصّاب بل الخوارج، فلا دليل على نجاستهم وإن كانوا أشدّ عذاباً من الكفّار، فلو خرج سلطان على أمير المؤمنين عليه السلام لا بعنوان التديّن، بل للمعارضة في الملك، أو غرض آخر، كعائشة والزبير وطلحة ومعاوية وأشباههم، أو نصب أحد عداوة له أو لأحد من الأئمّة عليهم السلام لا بعنوان التديّن، بل لعداوة قريش، أو بني هاشم، أو العرب، أو لأجل كونه قاتل ولده أو أبيه، أو غير ذلك، لا يوجب ـ ظاهراً ـ شيء منها نجاسة ظاهرية وإن كانوا أخبث من الكلاب والخنازير؛ لعدم دليل من إجماع أو أخبار عليه.

"Na ama makundi mengine kama Nasswaab bali na Makhawaariji, hakuna dalili ya unajisi wao, hata kama wao watakua na adhabu kali kuliko makafiri, lau kama atatoka mtawala yeyote chini ya uongozi wa kiongozi wa waumini (Ali bin Abii twalib) alaihis salaam, si kwa sababu za kidini, bali ni kwa sababu za kugombea madaraka, au kwa lengo jingine, kama alivyofanya Aisha (mke wa Mtume) na Zubairi na Twalha na Muawia, na mfano wao, au akatengeneza yeyote uadui kwake au kwa yeyote miongoni mwa maimamu alaihimus salaam, si kwa lengo la kidini, bali ni kwa ajili ya uadui kwa Makuraishi au Banii Hashim, au Waarabu, au pengine tu ni kwa sababu walimpiga vita mwanaye au baba yake, au mengineyo, hayo hayapelekei moja kwa moja katika unajisi wa wazi, **pamoja nakuwa ni wachafu kuliko Mbwa na Nguruwe…".** [112]

Maneno haya ya kiongozi mkuu wa Mashia Duniani, na mtegemewa wao, na marejeo yao, anasema wazi kuwa Mama wa Waumini na mke wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, Aisha radhi za Allah ziwe juu yake, na baadhi ya Maswahaba aliowataja hawasemi moja kwa moja kuwa ni najisi, lakini ni wachafu kuliko hata Mbwa na Nguruwe!.

---

[112] Rejea: Kitabut Twahara, cha Al-Khomeini (3/457) chapa ya Mu-assasatu tandhwiim.

Kauli yao pia ya kumkashifu Mama wa waumini Aisha radhi za Allah ziwe juu yake kuwa ni mzinifu, na malaya, kwa tukio ambalo Mwenyezi Mungu Mtukufu alilikanusha na akamtakasa Mama wa waumini radhi za Allah ziwe juu yake, katika Suratun Nuru kuanzia Aya ya kumi na moja na kuendelea.

Ndugu msomaji: Tumeandika baadhi tu ya itikadi na kauli zao, ili kitabu kisimchoshe msomaji, na lengo ni msomaji apate picha ya uhalisia wa Mashia, lakini kuna mengine machafu na makubwa zaidi dhidi ya mama waumini na kwa Maswahaba wengineo.

# SEHEMU YA NANE

## Machafu ya Mashia wasiyotaka watu wayajue

Ameeleza mwandishi wa kitabu: Kashful-Asraar, Sayyid Husein Al-Musa, aliyezaliwa Karbalaa nchini Iraq, na akasoma Ushia, kisha akatubia, siri nyingi za Mashia na hapa tutaandika baadhi tu ya siri hizo (na tutakitafsiri kwa kiswahili kitabu hicho In shaa Allah katika siku zijazo).

### 1- Kustarehe na mtoto mchanga anayenyonya:

Na alikuwa imamu Khomeini anaona kuwa inafaa kustarehe hata na mtoto anayenyonya akasema: **"Hakuna tatizo kustarehe na mtoto anayenyonya**

**kwa kumkumbatia na kupenyeza katikati ya mapaja -Yaani: Anaweka uume wake katikati ya mapaja yake- na kumbusu”** [113]

2- **Kuazimana tupu:** Anasema mwandishi wa kitabu hicho kuwa: “Hakika kuenea kwa vitendo vya Mut’aa kumepelekea kuazimana tupu, na kuazimana tupu maana yake: Ni mtu kumpa mwanaume mwingine mke wake au mjakazi wake na kumhalalishia kustarehe naye au kumfanya anachotaka, anapotaka mwanaume huyo kusafiri basi anamuwekesha mke wake kwa jirani yake au rafiki yake, au mtu yeyote atakaye mchagua, hivyo, anamhalalishia kumfanya anachotaka kwa muda wote wa safari yake. Na sababu kubwa ya hilo ni ili mumewe awe na amani na utulivu juu ya mke wake kuwa hatozini kwa wakati wote wa kutokuwepo kwake!!.[114]

3- **Kuhalalisha Ulawiti kwa wanawake:** Anasema mwandishi wa kitabu hicho kuwa: Na mambo hayakuishia hapo, bali wamehalalisha kumlawiti mwanamke, na wakasimulia pia riwaya za uongo walizozinasibisha kwa maimamu radhi za Allah ziwe juu yao, kwa mfano; amepokea Attuusiy kutoka kwa Abdillah bin Abil-Ya’furi amesema: Nilimuuliza Abuu Abdillah (Ja’fari bin Muhammadi Asswadiq)

[113] Rejea: Tahriirul Wasiila (2/241) Mas’ala ya 12

[114] Rejea: Kashful-Asraar watabriatil- A immatil At-haar (uk. 46-47)

alaihis salaam kuhusu mwanaume anayemuendea mke wake katika utupu wake wa nyuma, akasema: Hakuna tatizo ikiwa ataridhia, nikasema unaiweka wapi kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Basi waendeeni alivyokuamrisheni Mwenyezi Mungu"** Akasema: Hii ni katika kutafuta mtoto, yaani: Tafuteni mtoto alivyokuamrisheni Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu anasema: **"Wake zenu ni kama konde (mashamba) yenu, basi yaendeeni mashamba yenu mpendavyo"**[115]

kisha mwandishi akasema: Hakika kuwaendea wanawake kinyume na maumbile, hakuna aliyesema maneno haya (katika Uislamu) isipokuwa Mashia, na hasa Shia Ithna-asheria.

**Na ama kuwalawiti wanaume (Ushoga) Mwandishi akasema**: Na hawakutosheka na kuwalawiti wanawake pekee, bali wengi wao wamehalalisha hata kuwalawiti wanaume, na hasa hasa watoto wadogo wa kiume ambao bado hawajaota ndevu.[116]

Alitaja riwaya Sheikh wao Sayyid Sharafuddiin baada ya kuulizwa swali kuhusu mtu anayeishi ugenini na akakosa namna ya kuoa, akasema: **"Ikiwa safari yako itachukua muda mrefu, basi oa mwanaume"**[117]

[115] Rejea: Al-Istibswaar (3/243)
[116] Rejea: Kashful-Asraar (Uk. 52)
[117] Marejeo hayo hayo (Uk. 54)

Innaa lillaahi wa Innaa ilaihi raajiuun!

Huu ndio Uislamu wa Mashia ambao kuna watu wanautetea kwa ujinga na kuona kuwa wako sawa, kwa kusikiliza maneno yao ya ulaghai.

## Je itikadi kama hizi za Ushia ni rehema au ni laana?

Ndugu Muislamu, tukirejea maneno machafu ya Kiongozi wao mkuu dhidi Mama wa waumini Aisha radhi za Allah ziwe juu yake, na Maswahaba wengine Allah waridhie, je, lau kama Mtume rehema na amani ziwe juu yake angeliyasikia yangemfurahisha au yangemuudhi?. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يَرْمُونَ ٱلْمُحْصَنَٰتِ ٱلْغَٰفِلَٰتِ ٱلْمُؤْمِنَٰتِ لُعِنُوا۟ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٢٣﴾﴾ [سورة النور:٢٣].

**"Hakika wanaowasingizia wanawake, wanao jiheshimu, walioghafilika, Waumini, wamelaaniwa duniani na Akhera, nao watapata adhabu kubwa"** [An-Nur: 23] Na anasema nini Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu kumuudhi Yeye na Mtume wake:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يُؤْذُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ لَعَنَهُمُ ٱللَّهُ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ وَأَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا مُّهِينًا ﴿٥٧﴾﴾

[سورة الأحزاب:٥٧].

**"Hakika wanaomuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Mwenyezi Mungu amewalaani duniani na Akhera, na amewaandalia adhabu ya kufedhehesha"** [Al-Ahzaab: 57]

Kwa mujibu wa maneno hayo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, je, itikadi za Ushia ni rehema au ni laana??.

## Kujionyesha kwao kwa kujinasibisha na Sunna

Ameashiria bin Taimiya tabia hii, kwa kauli yake: "Wanaweza kupatikana baadhi ya wanaojinasibisha katika madhehebu ya maimamu wanne, ambao undani wao ni Maraafidhwa (Mashia), kama ambavyo wanapatikana katika wale wenye kujionyesha kuwa ni Waislamu ambao undani wao ni wanafiki, kwa sababu Mashia baada yakuwa ni jamii ya wanafiki wanaoficha itikadi zao, basi wakawa na haja kubwa ya kujionyesha kinyume na walivyo, kama walivyohitaji wanafiki kujionyesha kinyume na ukafiri"[118]

Baada ya kuona itikadi za Mashia hasa Ithna-asheria, tuhitimishe kwa kutazama itikadi za Mashia Ismailia.

[118] Rejea: Minhaajus Sunnati Annabawiyya (4/133)

# SEHEMU YA TISA

## Ni zipi itikadi za Mashia Ismailia kwa Ujumla?

Anasema Sheikh Abdul-Qadir Shaibatul Hamdi yakuwa: Yanazunguka makundi haya katika duara la kubumba lisilo na mpaka, na yote kiuhalisia yanarudi katika upagani, (kupinga uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu) na kukanusha majina yake matukufu na sifa zake za Juu, na kuzipotosha sheria za Manabii na Mitume, kwa kujificha chini ya kivuli cha kuwatetea watu wa nyumba ya Mtume nyakati zingine, na kuanzisha mambo mapya wakati mwingine, na wakashikamana na hadithi walizozitunga, au kwa aya sahihi wanazozipotosha, au kuzifasiri kinyume na makusudio yake, na tafsiri zao nyingi zimejengeka katika misingi ya Wamajusi (Makafiri waabudu moto), na baadhi ya nadharia za wanafalsafa kama Arosto.

Na wengi miongoni mwao wanatangaza kuwa muumba wa Mbingu na Ardhi ni Ali bin Abii Twalib, na wakadai kuwa hakika Ali alijitokeza katika sura ya binadamu ili awaliwaze viumbe wake na waja wake, na ili wamjue na wamuabudu.

Na wanasema baadhi yao: Hakika Ibilisi wa Maibilisi ni Omari bin Khattwab aliyewaelemea Wairani na Majusi, radhi za Allah ziwe juu yake, na anayemfuatia katika

daraja la Uibilisi ni Abubakari radhi za Allah ziwe juu yake, kisha Othman radhi za Allah ziwe juu yake, na hawana kikomo katika madai yao ya kipagani na unafiki, na kuyapotosha maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake, kwa kuyatoa katika makusudio yake.

Na wanasema baadhi yao kuwa: Maana ya swala tano nikujua siri zao, au ni kujua majina yao matano, ambayo ni Ali na Hasan na Husein, na Muhsin, na Fatma, na swaumu iliyofaradhishwa ni kuficha siri zao, au ni wanaume thelathini na wanawake thelathini, wanawataja kwa majina yao ndani ya vitabu vyao, na kuhiji nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu ni kuwatembelea Masheikh wao, na baadhi yao wanaifasiri kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: **"Imeangamia mikono ya Abii Lahabi naye ameangamia"**, kuwa mikono ya Abii Lahabi ni Abubakari na Omari.

Na wote kwa ujumla wamehalalisha zinaa, na pombe, na kufanya machafu, kama walivyodai baadhi yao kuwa Manabii ni watafuta madaraka, wako walioyatafuta kwa wema, na wako walioyatafuta kwa ubaya mpaka wakauawa..."[[119]]

[[119]] Rejea: Al-Adyaanu wal Firaq, wal Madhaahibul-Muaaswira, cha Shaibatul Hamdi (Uk. 157-158)

# SEHEMU YA KUMI

## Je ni ipi hukumu ya Raafidhwa katika Uislamu?

Ameeleza prof. Naasir Al-qifaari, katika kitabu chake Maqaalaatul-Firaq kuwa: Hukumu ya Shia (Raafidhwa) iko katika sehemu tatu:

**Sehemu ya kwanza:** Atakayedhihirisha miongoni mwao itikadi hizi, na akazitangaza wazi, kama madai ya kupotoshwa kwa Qur'ani, kukufuru kwa Maswahaba, na kuwafanya waungu maimamu, na kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na yeyote, hakuna shaka kabisa kuwa huu ni katika ukafiri wa wazi, na yamekuja kwa wingi maneno ya wanachuoni kulithibitisha hilo.

Amesema imamu Maliki: **"Anayewatukana Maswahaba wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, watu hawa hawana jina -au alisema- hawana fungu lolote katika Uislamu"**.

Amesema Imamu Sam'aani: "Na umekubaliana Umma mzima juu ya ukafiri wa Imamia (Ithna-asheria), kwa sababu wao wanaitakidi kupotea kwa Maswahaba, na wanapinga makubaliano yao".

Na anasema bin Taimiya: "Na atakayedai kuwa Maswahaba waliritadi (kutoka katika Uislamu) baada ya Mtume rehema

na amani ziwe juu yake, isipokuwa kikundi kidogo kisichofika takriban watu kumi, au kuwa wengi wao waligeuka na kuwa waovu, huyu pia hakuna shaka juu ya ukafiri wake; kwa sababu anapinga kile kilichoelezwa na Qur'ani katika sehemu zaidi ya moja, kama kuridhiwa na kusifiwa kwa wema.

Bali mwenye kutia shaka juu ya ukafiri wa mtu mfano kama huyu, basi hata yeye ukafiri wake utakuwa umethibitika, kwa sababu madhumuni ya kauli hizi nikuwa walionukuu Qur'ani na Sunna na kutufikishia ni makafiri na waovu, na kwamba aya hii:

﴿كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ ﴿١١٠﴾﴾ [سورة آل عمران: ١١٠].

**"Nyinyi mmekuwa bora ya Umma waliotolewa watu"** [Al-Imran: 110] Na wabora wa Umma huu ni wale wa Karne ya kwanza, ikiwa wengi wao walikuwa makafiri, au waovu, basi makusudio yake nikuwa huu ni Umma wa shari na mbaya kuliko Umma zote"

Na liliulizwa jopo la kudumu la wanachuoni kuhusu vichinjwa vya Shia Ja'faria, wanaomuomba Ali katika shida na raha? Likajibu: "Ikiwa jambo ni kama alivyoeleza muulizaji, kuwa jamaa anaoishi nao ni katika Shia Ja'faria wanaomuomba Ali na Hasan na Husein na watukufu wao, basi hawa ni washirikina, walioritadi na kutoka katika

Uislamu, tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu, ni haramu kula vichinjwa vyao; kwa sababu hiyo ni mizoga, hata kama wataitajia jina la Mwenyezi Mungu wakati wa kuchinja".

**Tahadhari Muhimu:** "Katika mambo ya kuzingatia kulingana na (Manhaji) njia ya watu wa Sunna katika kukufurisha nikuwa "Kauli zote hizi wanazozisema, na zinazojulikana wazi kuwa zinakwenda kinyume na yale aliyokuja nayo Mtume rehema na amani ziwe juu yake hizi ndio ukafiri, na vile vile vitendo vyao ndio viko katika aina ya vitendo vya makafiri kwa Waislamu, na ndio ukafiri pia, lakini kumkufurisha mtu maalum katika watu wanaoelekea kibla na kumhukumu kuwa atakaa milele motoni, hili linasimama katika kuthibitika kwa sharti za ukafiri kwake, kuondoka kwa vizuizi (kama tulivyoeleza mwanzo wa kitabu hiki), kwani sisi tunazungumza hukumu kwa ujumla kuhusu aya za kemeo na ahadi za adhabu, na kukufuru, na mtu kuwa muovu, na wala hapa hahukumiwi mtu maalum kuingia katika ujumla huo, mpaka uthibitike kwake muktadha ambao hauna mpinzani kwake..."

**Sehemu ya pili:** Atakayeficha itikadi za ukafiri na akadhihirisha kinyume chake, huyu ni mnafiki, tutaishi naye kulingana na kile anachodhihirisha, na siri yake Mwenyezi Mungu ndiye atakayeihukumu, lakini ni wajibu kuchukua tahadhari na watu wa namna hii, na kutowapa mamlaka na vyeo ambavyo vinauhusiano na usalama wa

Waislamu, na nafasi zao, na taaluma zao (kuwapa nafasi za kufundisha katika shule za Kiislamu) na afya yao, kwa mujibu wa kauli yake Mtukufu:

﴿هُمُ ٱلْعَدُوُّ فَٱحْذَرْهُمْ ﴿٤﴾﴾ [سورة المنافقون:٤].

**“Hao ni maadui, tahadhari nao”** [Munaafiquun: 4].

**Sehemu ya tatu:** Atakaye jinasibisha nao, na akawa hakusema itikadi kama hizo, na akawa hajui lolote kuhusu itikadi hizo, miongoni mwa watu wasiojua lolote kuhusu itikadi zao za ukafiri, na misingi yao hatari, watu wa aina hii ni wazushi, na wanapata madhambi ya mtu anayeongeza nguvu katika uzushi na upotovu.[120]

[120] Rejea kauli zote hizi katika kitabu: Maqaalaatul-Firaq (Uk. 202-204)

# SEHEMU YA KUMI NA MOJA

## Je, inafaa kuswali nyuma ya Shia au katika misikiti yao?

Aliulizwa Sheikh Fauzan Allah amuhifadhi: Ni ipi hukumu ya kuswali nyuma ya Shia?

Akajibu kwa kusema: "Haifai kuswali nyuma ya Shia, hawa wanaowachukia Maswahaba na kuwatukana na kuwalaani, au wanawaomba maimamu badala ya Mwenyezi Mungu, wanaoabudu makaburi, haifai kuswali nyuma yao, msiswali nyuma ya Shia, ila wao wakija kuswali pamoja nanyi msiwazuie, ama nyinyi msiswali nyuma yao".

Na aliulizwa Sheikh bin Baazi na mtu aliyeswali nyuma ya Shia pasina kujua, akaja kubaini baada ya swala, akajibu kuwa anatakiwa arudie swala yake.

Ama kuswali ndani ya misikiti yao; aghalabu ya Mashia hawana misikiti, bali wana holi (kumbi) za ibada, ambazo wao huziita **Huseiniyya**, na hii hasa kwa Ithna-asheria, na huu si msikiti bali ni ukumbi ambao ndani yake hufanyika vikao, mihadhara ya siku ya Aashuraa, kujipiga, na mikusanyiko ya kidini, na wanaweza kuswalia ndani yake swala za pamoja wakati mwingine, na sehemu nyingine wanaita "**Ma'tam**" na wanakusudia kuwa ni mahali pa matanga

(maombolezo) na mikusanyiko ya kidini, na mahala pengine ni "**Mash-had**" Na sehemu hii wakati mwingine huwa ni mahali palipojengwa pembezoni mwa makaburi ya watu wanaowatukuza, mfano kama Mash-had za maimamu. Na mahala pengine ni "**Ataba**" au "**marqad**" na hii hutumika kwa sehemu kubwa za ziara zao kama: Atabatul-Husein n.k.

Hivyo ikiwa Muislamu ataingia katika msikiti wao na akakuta kaburi ndani ya Msikiti, au mbele ya Msikiti basi akiswali hapo swala yake ni batili, lakini pia akikuta nembo na alama za Husein au Imamu Ali pia asiswali hapo, kama alivyoeleza hilo Sheikh Fauzan Allah amuhifadhi, lakini akiingia humo na asikute chochote katika hayo na akaswali peke yake swala yake ni sahihi, na kilicho bora zaidi ni kuepuka misikiti yao na kutafuta msikiti mwingine uliosalama zaidi.

# SEHEMU YA KUMI NA MBILI

## Njia (Manhaji) ya Ahlus Sunna katika kuamiliana na makundi yanayokwenda kinyume

**Kwanza:** Mtu wa bid'a si kafiri, madam uzushi (Bid'a) aliyoifanya haimtii katika ukafiri, atakayeleta bid'a ya kumtia katika ukafiri basi hapo dalili ya kisheria itasimama kuhukumu kitendo chake kuwa ni ukafiri, na zikithibiti sharti za kumkufurisha yeye mwenyewe, na vizuizi vyake vikaondoka, basi huyu ni kafiri, na atafanyiwa miamala ya makafiri, na atakayeficha basi huyu ni mnafiki, na atakaye jinasibisha nao na akawa hakusema kauli zao za ukafiri basi huyu anapata dhambi za mtu anayeongeza nguvu ya watu wazushi.

**Pili:** Ni kuwabainishia haki kwa kuwafikishia mafundisho sahihi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na kuwaelimisha ubaya wa uzushi, na kuwatahadharisha nao kwa hekima na mawaidha mazuri.

**Tatu:** Ni wajibu kuwafanyia uadilifu na kutowadhulumu, kwani dhuluma ni haramu moja kwa moja, na uadilifu ni wajibu pasina mipaka, na wema waliotangulia walipita katika msingi wa uadilifu na kila kundi la uzushi na mengineyo.

**Nne:** Ni lazima kuweka wazi hali zao kwa Umma (hadharani) -kulingana na masilahi ya kisheria, bila kupunguza wala kuongeza, asiuvuke ukweli, na wala asipunguze uhalisia, na wala asiwazulie uongo, na asiwanasibishie maneno ambayo hawakuyasema, na asiwatuhumu kwa mambo ambayo hawajayafanya.

Anasema Imamu Qarrafi: "Vigogo wa uzushi na kubuni mambo ya upotovu ni lazima watangaziwe watu uovu wao na aibu zao, na kwamba hawako katika usawa, ili watu madhaifu wachukue tahadhari na wasiangukie humo, na wauepuke uovu huo kadiri wawezavyo, kwa sharti asivuke ukweli, na wala asiwazulie uovu na machafu ambayo hawajayafanya, bali aishie tu katika yale mabaya waliyonayo, na asiseme juu ya mtu wa bid'a kuwa anakunywa pombe, na ni mzinifu, na mengineyo ambayo wala hana"[121]

**Tano:** Ni katika sheria kuweka nao mdahalo, pakihitajika kuwa na mdahalo kwa lengo la kutoa nasaha, na si kwa lengo la kuonyeshana vitimbi, na hii aliwahi kuifanya swahaba bin Abbasi baada ya kujadiliana na Makhawariji, wakarudi katika haki (Sunna na Jamaa) miongoni wao watu takriban elfu nne.

[121] Rejea: Al-Furuuq (4/207-208)

**Sita:** Na asisimame kuwajibu (Raddi) watu wa uzushi, na kuweka nao mdahalo isipokuwa mtu mwenye elimu na upeo mkubwa na hoja na maarifa ya kuijua haki kwa ushahidi wake, na kuijua batili na namna ya kujibu hoja zake tata, hivyo kwa mtu asiyekuwa na elimu, na wala hana uwezo wa kusimamisha hoja kwa mtu mzushi na kujibu upotofu wake, na kuporomosha hoja zake tata, hatakiwi kabisa kujiingiza katika mijadala na mtu mzushi au kuweka naye mdahalo.

**Sheria ya kuwahama:**

Kabla sijanukuu maneno ya wanachuoni nitoe nasaha zangu kwa ndugu zangu wote:

Kuna baadhi ya ndugu zetu katika wana Sunna wanaochupa mipaka katika swala la kuwahama watu wa bid'a (Allah awaongoze), na hasa ni kwa sababu ya mihemuko na uchache wa elimu, miongoni mwa mambo wanayofanya ni kumtenga kila anayeswali katika misikiti ya watu wazushi, au kila imamu, ustadhi ama sheikh katika watu wanaoswali au kusimamia misikiti inayofanya mambo ya uzushi, na kwa kiwango kikubwa utakuta watu hao wanafuata mkumbo, au elimu yao ni ndogo, au wana hoja zisizokuwa sahihi ambazo wamezirithi na kuzishikilia, kiasi kwamba wana haja ya kuelimishwa na kufikishiwa haki kwa hekima, tatizo ni wao kutengwa pasina kuwaweka karibu na kuwafikishia haki, kisha waikatae kwa chuki na makusudi ndio watengwe.

Tuna haja kubwa ya kushikamana na Qur'ani na Sunna kwa ufahamu sahihi, nasi mihemuko na misimamo ya kupandikizwa, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu kumwambia Mtume wake rehema na amani ziwe juu yake:

﴿وَإِنْ أَحَدٌ مِّنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ٱسْتَجَارَكَ فَأَجِرْهُ حَتَّىٰ يَسْمَعَ كَلَـٰمَ ٱللَّهِ ثُمَّ أَبْلِغْهُ مَأْمَنَهُۥ ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَعْلَمُونَ ﴿٦﴾﴾ [سورة التوبة:٦].

**"Na ikiwa mmoja wapo katika washirikina akikuomba ulinzi, basi mpe ulinzi apate kusikia maneno ya Mwenyezi Mungu. Kisha mfikishe pahala pake pa amani. Haya ni kwakuwa hao ni watu wasiojua"** [Tauba: 6]

Anasema bin Kathiri katika Aya hii: "Na kwa sababu hii alikuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake akimpa amani kila anayemuijia kwa lengo la kutaka kuelekezwa au akiwa na ujumbe, kama lilivyomjia kundi la wajumbe siku ya vita vya Hudaibia, kutoka kwa Makuraishi, na miongoni mwao ni: Urwa bin Masoud, na Mukariz bin Hafs, na Suhail bin Amri, na wengineo, walimjia mmoja baada ya mwingine, wakipishana katika swala lililopo baina yake na baina ya washirikina, basi wakaona jinsi gani Maswahaba wanamtukuza na kumheshimu Mtume rehema na amani ziwe juu yake, jambo lililowashangaza sana, na hawakuwahi kuliona kwa wafalme wala kwa Kaisari (Mfalme wa Roma) wakarudi kwa jamaa zao

wakawaeleza hilo, na tukio hilo pekee lilikuwa ni miongoni mwa sababu kubwa ya kuongoka wengi wao.

Kisha anasema katika kauli yake Mtukufu: **"Haya ni kwakuwa hao ni watu wasiojua"** Yaani: Hakika tumekupa sheria ya kuwapa amani watu mfano wa hawa, ili wapate kuijua dini ya Mwenyezi Mungu, na ujumbe wa Mwenyezi Mungu usambae kwa waja wake.[122]

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu alipomtuma Musa na ndugu yake Harun amani iwe juu yao, kwenda kwa Firauni aliwaambia:

﴿فَقُولَا لَهُۥ قَوۡلٗا لَّيِّنٗا لَّعَلَّهُۥ يَتَذَكَّرُ أَوۡ يَخۡشَىٰ ٤٤﴾ [سورة طه: ٤٤].

**"Mwambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaongoka"** [Twaha: 44]

Anasema bin Kathiri katika Aya hii kuwa: "Aya hii ndani yake kuna mazingatio makubwa, nayo nikuwa Firauni alikuwa katika upeo wa hali ya juu wa ukaidi na kiburi, na Musa ni mteule wa Mwenyezi Mungu na kipenzi chake katika viumbe wake, kwa wakati ule, lakini pamoja na hivyo aliamrishwa asimsemeshe Firauni isipokuwa kwa huruma na ulaini..".

[122] Rejea: Tafsiir bin Kathiir Surat Tauba: 6

Kisha akasema bin Kathiri: "Nikuwa ujumbe wao kwake uwe kwa maneno yasiyokuwa makali, tena laini yenye ukaribu na wepesi, ili yawe ni mepesi kukita ndani ya nyoyo, na yawe na ufanisi na tija, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿ ٱدۡعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلۡحِكۡمَةِ وَٱلۡمَوۡعِظَةِ ٱلۡحَسَنَةِۖ وَجَٰدِلۡهُم بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُۚ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعۡلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِۦۖ وَهُوَ أَعۡلَمُ بِٱلۡمُهۡتَدِينَ ١٢٥ ﴾ [سورة النحل:١٢٥].

**"Lingania (ita) katika njia ya Mola wako Mlezi, kwa hekima na mawaidha mazuri, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora"** [An-Nahl:125].[123]

Anasema Prof. Naasir Aqifaari: Ama kuwahama kuna namna mbili:

Ya kwanza: Kuuhama uzushi.

Ya pili: Kuwahama wazushi.

Ya kwanza inaingia ndani ya kauli yake Mtukufu:

﴿ وَإِذَا رَأَيۡتَ ٱلَّذِينَ يَخُوضُونَ فِيٓ ءَايَٰتِنَا فَأَعۡرِضۡ عَنۡهُمۡ حَتَّىٰ يَخُوضُواْ فِي حَدِيثٍ غَيۡرِهِۦۚ وَإِمَّا يُنسِيَنَّكَ ٱلشَّيۡطَٰنُ فَلَا تَقۡعُدۡ بَعۡدَ ٱلذِّكۡرَىٰ مَعَ ٱلۡقَوۡمِ ٱلظَّٰلِمِينَ ٦٨ ﴾ [سورة الأنعام:٦٨].

[123] Rejea Tafsiri hiyo hiyo Katika Suratu Twaha: 44

**“Na unapowaona wanao ziingilia (kwa kejeli) Aya zetu, basi jitenge nao mpaka waingilie mazungumzo mengine. Na kama Shetani akikusahaulisha, basi baada ya kutanabahi usikae pamoja na watu madhalimu”** [Al-An’aam: 68]

Na ni pamoja na kauli yake rehema na amani ziwe juu yake: **“Mhamaji ni yule aliyeyahama yale aliyoyakataza Mwenyezi Mungu”**.

Aina ya Pili: Ni kumhama mzushi na hii inachukua nafasi ya Ta’ziir (kumkanya), na onyo hili linakuwa kwa mtu kuliyeonekana kwake kuzua mambo, kama mlinganiaji anayelingania katika uzushi, unaokwenda kinyume na Qur’ani na Sunna na makubaliano ya wema waliotangulia.

Kama ambavyo anatengwa mzushi mpaka aachane na uzushi wake, na hairuhusiwi kuchukua elimu kwake, na wala hatakiwi kuwa shahidi katika jambo, na wala hatangulizwi kuswalisha, na watu wataacha kumtembelea anapougua, wala kusindikiza jeneza lake, bali hazungumzishwi wala kukaa naye pamoja, wala hatolewi salamu, mpaka mwisho wa aina za kumtenga. (Ikumbukwe kuwa Sheikh anaye mkusudia hapa si maamuma, mbumbumbu mzungu wa reli, bali anamkusudia Sheikh wa Kizushi anayewalingania watu katika uzushi, kama alivyoeleza hapo juu).

Na ni lazima pia kuchunga masilahi ya kisheria ya kumtenga mtu; kwa sababu lengo ni kumkemea anayetengwa na kumuadabisha, ili watu wengine warejee kutoka katika hali kama yake, na kutowadhuru wanaokaa naye, na ndio maana hii inatazamwa kwenye kumtenga mtu katika manufaa na madhara, na uwezo na kutoweza, na hii inatofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine, na mzushi mmoja hadi mwingine, na aina ya uzushi pia.[[124]]

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

### Njia fupi ya kukata mjadala katika Swala la haki

**Sheria ya kuapizana laana na mpinzani:** Ikitokea umejadiliana na Shia au mtu yeyote katika watu wa batili, akang'ang'ania batili yake, baada ya kuwa umekwisha mbainishia ukweli na umemsimamishia hoja, basi mtaapizana laana, na hili Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuamrisha Nabii wake rehema na amani ziwe juu yake, aapizane na aliyekaidi haki, kuhusu swala la Issa, rehema na amani ziwe juu yake, baada ya kudhihiri haki, akasema Mtukufu:

[[124]] Rejea: Maqaatul-Firaq (Uk. 51-53)

﴿فَمَنْ حَآجَّكَ فِيهِ مِنۢ بَعْدِ مَا جَآءَكَ مِنَ ٱلْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا۟ نَدْعُ أَبْنَآءَنَا وَأَبْنَآءَكُمْ وَنِسَآءَنَا وَنِسَآءَكُمْ وَأَنفُسَنَا وَأَنفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَل لَّعْنَتَ ٱللَّهِ عَلَى ٱلْكَٰذِبِينَ ﴿٦١﴾﴾ [سورة آل عمران: ٦١].

**“Watakaokuhoji katika haya baada ya kukufikia elimu hii waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo”.** [Al-Imran: 61]

Na kwa hilo imekuja Sunna, kwani imethibiti kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake, alitaka kuapizana laana na Wakristo wa Najran.

Na huo ndio ushahidi wa sheria ya kuapizana laana na mpinzani kama Mayahudi na Wakristo, au Wazushi, au wengineo, amesema bin Hajari: “Na katika kisa cha watu wa Najran kuna faida:...Sheria ya kuapizana laana na mpinzani, atakapong’ang’ania baada ya kudhihiri hoja, na aliita watu bin Abbasi katika hilo, kisha Imamu Auzai, na lilifanyika hilo kwa kundi kubwa la wanachuoni, na katika mambo yaliyowahi kutokea, kulingana na uzoefu wa hilo, nikuwa atakayeapizana laana na akawa yuko katika batili, huwa haupiti mwaka tangu siku ya kuapizana majibu anayaona, na lilitokea hilo kwangu pamoja na mtu mmoja

alikuwa aking'ang'ania itikadi za kipagani, hakuweza kunyanyuka baada ya miezi miwili".[125]

## Sharti za kuapizana laana

1- Kusimamisha hoja kwa mpinzani kabla ya kuapizana naye.

2- Kung'ang'ania kwake juu ya batili yake baada ya kumbainikia haki.

3- Upinzani wake uwe katika jambo la haki lililothibiti bila shaka yoyote ndani yake.

4- Kusiwe na tafsiri zaidi ya moja zinazokubalika zote katika jambo wanalopingana.

# SEHEMU YA KUMI NA NNE

## Mwenye kufa katika itikadi za Ushia

Baada ya kujua kuwa Uislamu unavitenguzi vyake, hivyo, mtu yeyote atakayeshikamana na itikadi za kishia zenye kutengua Uislamu, na akafa kabla ya kurejea katika haki, na kutubia kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu basi atambue kuwa amekufa nje ya dini sahihi ya Uislamu, na mafikio yake yatakuwa sawa sawa na mtu aliyekufa katika dini

[125] Rejea: Fat-hul Baariy (8/95)

isiyokuwa Uislamu, hata kama aliswali swala elfu moja, na akahiji Hija elfu moja, na akasaidia masikini na heri nyingine nyingi basi atambue kuwa Mwenyezi Mungu amali zake zote atazifanya kama alivyosema Mtukufu:

﴿وَقَدِمۡنَآ إِلَىٰ مَا عَمِلُواْ مِنۡ عَمَلٖ فَجَعَلۡنَٰهُ هَبَآءٗ مَّنثُورًا ٢٣﴾ [سورة الفرقان:٢٣].

**"Na tutayaendea yale waliyoyatenda katika vitendo vyao, tuvifanye kama mavumbi yaliyotawanyika."** [Al-Furqaan: 23]

Na atakuwa miongoni mwa watu waliopata hasara kubwa mno, wale waliodhani kuwa wanafanya heri duniani kumbe, wanapoteza mali na umri wao katika batili, kama alivyoeleza Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿قُلۡ هَلۡ نُنَبِّئُكُم بِٱلۡأَخۡسَرِينَ أَعۡمَٰلًا ١٠٣ ٱلَّذِينَ ضَلَّ سَعۡيُهُمۡ فِي ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَا وَهُمۡ يَحۡسَبُونَ أَنَّهُمۡ يُحۡسِنُونَ صُنۡعًا ١٠٤ أُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ بِـَٔايَٰتِ رَبِّهِمۡ وَلِقَآئِهِۦ فَحَبِطَتۡ أَعۡمَٰلُهُمۡ فَلَا نُقِيمُ لَهُمۡ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ وَزۡنٗا ١٠٥ ذَٰلِكَ جَزَآؤُهُمۡ جَهَنَّمُ بِمَا كَفَرُواْ وَٱتَّخَذُوٓاْ ءَايَٰتِي وَرُسُلِي هُزُوًا ١٠٦﴾ [سورة الكهف:١٠٣-١٠٦].

**"Sema: Je, tukutajieni wenye hasara kubwa mno katika vitendo vyao?** [103] **Ni wale ambao juhudi yao katika maisha ya dunia imepotea bure, nao wakidhani kwamba wanafanya kazi nzuri.** [104] **Hao ni wale waliozikufuru Aya za Mola wako Mlezi, na kukutana**

**naye. Kwa hivyo vitendo vyao vimepotea bure, na wala siku ya Kiyama hatutawathamini kitu.** [105] **Hiyo Jahannamu ni malipo yao kwa walivyokufuru na wakafanyia kejeli Ishara zangu na Mitume wangu"** [Kahf: 103-106].

Ndugu zangu, maisha ya dunia ni mafupi, na safari tunayokwenda ni ndefu, na starehe za dunia vyovyote zitakavyokuwa nzuri lazima zitafikia kikomo, tusibaki katika batili kwa sababu masilahi ya muda mfupi, yatakayotufanya kuishi miaka dahari motoni, kwa hivyo, atakayetubia na akarejea katika njia iliyo nyooka, na akaachana na itikadi mbovu hizo, na akafanya mema, kwa kumhofu Mwenyezi Mungu, na kuogopa adhabu zake, basi Mwenyezi Mungu atampokea na atamfutia makosa yake na kumuingiza katika rehema zake, kama alivyoahidi Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِلَّا مَن تَابَ وَءَامَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَٰلِحًا فَأُوْلَٰٓئِكَ يُبَدِّلُ ٱللَّهُ سَيِّـَٔاتِهِمْ حَسَنَٰتٍۗ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ٧٠﴾ [سورة الفرقان: ٧٠].

**"Isipokuwa atakaye tubu, na akaamini, na akatenda matendo mema, basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu"**[Furqaan: 70].

Mwenyezi Mungu kaweka sharti tatu: 1- Kutubu, Yaani kurejea kwake. 2- Kumwamini Yeye na Mtume wake kama alivyoelekeza. 3- Kufanya matendo mema, Yaani: Kurekebisha yale mabaya aliyoyafanya mtu.

# Tamati

Alhamdulillaah -kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu- ambaye kwa neema zake mambo mazuri hutimia, na hapa nimefika mwisho wa kile nilichokusudia kukifikisha kwa Umma wa Kiislamu, ili asiangamie mtu ila akiwa anajua, na apone mtu mbele ya Mwenyezi Mungu kwa elimu iliyomfikia, kwa yale mazuri na ya heri yote niliyoyaandika katika kitabu hiki basi yanatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na pale nilipoteleza au kukosea ni kwa nafsi yangu na Shetani, na ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu anisamehe mimi na wazazi wangu, na Waislamu wote kwa ujumla, walio hai na walio kufa, atujaalie sote mwisho mwema, na aturehemu nasi tutakapofika walipofika, na awalipe heri watu wote watakaoshiriki kukichapisha au kukisambaza, au kushiriki kwa namna yoyote ile katika heri hii.

Na mwisho ninasema:

سبحانك اللّٰهُمَّ وبحمدك أشهد أن لا إله إلا أنت أستغفرك وأتوب إليك

وصلى الله وسلم على نبينا محمد وآله وصحبه وسلم تسليمًا كثيرًا.

Kimekamilika:

Tarehe: 13/12/1447= 30/05/2026